# Nipashe

Jumatano Julai 17, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579972

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper



UCHAMBUZI:

Kitaifa

siasa

HABARI BORA NA KAMILIFU

'Hija' ya Museveni Chato ichagize utengamano EAC

BAADA YA MIAKA 55

Pius Msekwa aeleza misumari ya siri iliyoshikilia Muungano-5

Zuma apinga kuwa 'mfalme wa ufisadi'

Mzozo Syria wapangua utii wa Uturuki NATO

UKURASA 13



## Mchungaji mbaroni kwa madai kubaka, kumpa mimba bintiye

UKURASA 3

# Makamba asema ujumbe umefika

**NI** kuhusu tuhuma dhidi yake na Kinana, asema baraza lijibu, lisijibu wao kazi wameimaliza...

*Endelea ukurasa wa 2*



Kinana



Makamba

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### PPRA YAOKOA FEDHA ZA SERIKALI BIL. 46/-

MAMLAKA ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) imeisaidia serikali kuokoa Sh. bilioni 46.91 ambazo zingepotea kutokana na kutokufuatwa kwa...

UKURASA WA 23

### AELEZA ALIVYOBAKWA NA BABA WA KAMBO

MAHAKAMA ya Mkoa ya Mwera Unguja, imeanza kusikiliza kesi ya mtoto mwenye umri wa miaka 13 anayedaiwa kutoroshwa na kubakwa...



Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wakipita kwenye barabara itumiwayo na magari ya Msimbazi kutokana na kukosa sehemu iliyotengwa maalum kwa ajili ya watembea kwa miguu kuchukuliwa na wafanyabiashara ndogo. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

## HESLB yafuata wakopaji jeshini

UKURASA 3

## Mahabusi amlipua ofisa Magereza mbele ya JPM



UKURASA 2

**MICHEZO** SIMBA SC YASISITIZA KUMKATAA KILOMONI UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

## KESI YA ZITTO:

# Shahidi adai kupokea majeruhi watatu

Na Hellen Mwango

DAKTARI Ernest Kiluhungwa (46), kutoka Kituo cha Afya Nguruka katika Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza, Mkoa wa Kigoma, amedai mahakamani kwamba aliwapokea na kuwapa matibabu majeruhi watatu baada ya kudaiwa kupigwa risasi na askari polisi eneo la Mwanduhubandu.

Kadhalika amedai kuwa baada ya kuwapa matibabu walilazwa katika kituo hicho, lakini alipigiwa simu na askari polisi kwamba wamewachukua majeruhi hao kwa kuwa ni wahalifu na wako salama.

Dk. Kiluhungwa alitoa ushahidi huo jana dhidi ya kesi ya uchochezi inayomkabili Mbunge wa Kigoma Mjini, Zitto Kabwe, inayosikilizwa mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Tumaini Kweka akisaidiana na Mawakili wa Serikali Waandamizi, Nassoro Katuga na Wankyo Simon.

Alidai kuwa alihamishiwa katika kituo hicho mwaka 2017 na kwamba wapo madaktari watatu na wauguzi.

Akiongozwa na Wakili Katuga, shahidi alidai kuwa Oktoba 18, 2018 alikuwa Kituo cha Afya cha Nguruka tangu asubuhi na kwamba alikuwa daktari wa zamu wengine walikuwa na shughuli nyingine nje ya kituo.

"Ilipofika saa 12 jioni nilipokea majeruhi watatu wakiwa mahututi waliosindikizwa na watu wengine wawili, niliwakagua mmoja alikuwa amepigwa risasi sehemu mbili tofauti tumboni, wawili walijeruhiwa kifuani na mabegani walikuwa wakitokwa damu sana hivyo walilalamika maumivu," alidai shahidi na kuongeza:

"Majeruhi hao walitokea Kijiji cha Mpeta kwamba askari polisi walikuwa wakiwahamisha eneo lao la kilimo, niliwawekea maji ya dripu, nikawapa dawa za maumivu na za kutibu majeraha, lakini wakati nikiendelea na matibabu walikuja askari polisi baadhi nilikuwa nawafahamu wengine siwafahamu wakadai kwamba wamekuja kuwachukua wahalifu wamewaua askari wenzao wawili," alidai Dk. Kiluhungwa.

Aliwataja majeruhi hao kuwa ni, Kono Mwandu, Shishi George na Jumanne Jackson na baada ya kuwapa matibabu aliwaacha wodini akarudi ofisini kuhudumia wagonjwa wengine.

Hata hivyo, alisema kwa mujibu wa utendaji wake wa kazi ikitokea majeruhi amefikia hospitali anajimudu anaagizwa kwenda kuchukua fomu namba tatu na kwa hali ya majeruhi aliowapokea alilazimika kuwaagiza ndugu zake kwenda kuchukua fomu hiyo wakati akiendelea kuokoa maisha yao.

Aliendelea kudai kuwa hakuwaona tena wagonjwa hao na kwamba aliwasiliana na ndugu wa majeruhi hao ambao walimthibitishia kuwa ndugu zao wamepelekwa gerezani Kigoma na wako hai.

Upande wa utetezi uliongozwa na wakili, Getrude Beneth.

INAENDELEA UK. 8

# Makamba asema ujumbe umefika

Na Salome Kitomari

KATIBU Mkuu mstaafu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Yusuph Makamba, amesema wanaamini ujumbe wa tamko lao la mwishoni mwa wiki umefika kwa walengwa.

Amesema hata kama Baraza la Ushauri la Viongozi Wakuu Wastaafu wa CCM halitajibu malalamiko yao, tamko lao lililenga kuujulisha umma kuwa hawahusiki kwa namna yoyote na tuhuma zinazotolewa dhidi yao.

Julai 14, mwaka huu, Makamba na Abdulrahman Kinana ambaye pia ni katibu mkuu mstaafu wa CCM, walitoa tamko la kufafanua tuhuma zilizoelekezwa kwao na mtu aliyejitambulisha kuwa ni mwanaharakati.

Katika tamko hilo, wawili hao walisema tathmini ya awali inaonyesha mtu huyo anatumiwa kusambaza taarifa hizo zinazolenga kuwadhalilisha, kuwachafua na kuwashushia heshimu mbele ya jamii.

Akizungumza na Nipashe jana, Makamba alisema walishiriki kumweka madarakani Rais na serikali iliyoko madarakani, hivyo tuhuma zinazoelekezwa kwao hazina mashiko.

"Inawezekana hamjaelewa lengo la tamko letu, hatukulielekeza kwa baraza, bali kutoa taarifa kwao (baraza), umma na wanaCCM kuwa sisi hatuhusiki, ni watu safi," alisema.

Makamba aliongeza: "Sisi ni watu safi, hatuhusiki na jambo lolote, hiyo kazi tumeimaliza, sisi ni watu safi, maneno yanayosemwa juu yetu ni uzushi, hatuhusiki na hizo tuhuma, serikali tuliitafuta sisi na tulishiriki kumweka Rais madarakani, baraza lijibu lisijibu. sisi tumemaliza kazi yetu." Katika tamko lao, Makamba na Kinana walisema walimwandikia barua Katibu Mkuu wa Baraza la Ushauri la Viongozi Wakuu Wastaafu wa CCM, Pius Msekwa, kulishauri litumie busara katika kushughulikia jambo hilo linaloelekea kuhatarisha umoja, mshikamano na utulivu wa chama hicho.

Baraza hilo liko chini ya uenyekiti wa Rais mstaafu wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi ambaye pia ni mwenyekiti mstaafu wa CCM.

Walisema wameamua kutokwenda mahakamani kwa sababu kuu mbili ambazo walizitaja kuwa ni pamoja na jambo lenyewe kuwa na taswira ya kimkakati na lina mtandao wenye malengo ya kisiasa, hivyo linapaswa kushughulikiwa kisiasa.

Walisema sababu ya pili kutoona kiwango cha fedha ambacho kinaweza kulipwa na kikawiana na heshima yao.

Kauli za mwanaharakati huyo, walisema zinaonyesha si zake bali anatumwa kutekeleza maagizo na kutumika kama kipaza sauti na kwamba ni mamluki anayetumika kuivuruga CCM na nchi kwa ujumla.

Katibu wa baraza hilo, Msekwa, alikaririwa jana akisema suala la viongozi hao limeshapelekwa katika ngazi za juu, huku kukisambaa katika mitandao ya kijamii taarifa iliyodaiwa kutolewa na Spika mstaafu huyo kuhusu majibu ya awali ya baraza kwa Kinana na Makamba.

Hata hivyo, Msekwa hakupokea simu alipotafutwa na Nipashe jana kuzungumzia taarifa hiyo.




Rais John Magufuli akitoka katika Gereza Kuu la Butimba, baada ya kuzungumza na wafungwa, mahabusi pamoja na Askari wa Jeshi la Magereza katika gereza hilo, mkoani Mwanza jana. **PICHA: IKULU**

# Mahabusi amlipua ofisa Magereza mbele ya JPM

Na Mary Geofrey

THOMAS Nyagombe, mahabusi katika Gereza Kuu la Butimba jijini Mwanza, amekiweka hatarini kibarua cha Ofisa Usalama wa gereza hilo, baada ya kumweleza Rais John Magufuli mambo mabaya linayoyafanya.

Katika ziara yake ya kushtukiza gerezani huko jana, Rais Magufuli alielezwa na mahabusi huyo na wafungwa wengine kuwa wamekuwa na changamoto mbalimbali zinazowakabili ukiwamo uonevu wanaofanyiwa na viongozi wa gereza.

Nyagombe alimweleza Rais Magufuli kuwa ofisa huyo amekuwa akishindwa kusimamia usalama wa wafungwa na mahabusi na kusababisha mauaji kutokea katika gereza hilo.

"Gereza hili siyo la amani, kuna mauaji yalitokea wakati ofisa huyu wa usalama akiwa amekaa tu bila shughuli yoyote, mwambie mihuri akupe na simu zote akupe kwa sababu amekuwa akitoa taarifa za uongo," mahabusi huyo alisema.

Nyagombe alimwomba Rais Magufuli kuchukulia hatua za kisheria dhidi ya ofisa huyo kwa kuwa yeye na maofisa wengine wa magereza wana mbinu nyingi za kudhuru wafungwa na mahabusi.

Alizitaja baadhi ya mbinu wanazotumia kuwadhuru wafungwa na mahabusi kuwa ni kushirikiana na madaktari kuwachoma sindano za sumu na kusababisha vifo.

"Mheshimiwa Rais Magufuli, tunakuomba ondoka na huyu mkuu, tunakuomba ondoka naye (ofisa usalama) ili amani iendelee kuwapo, ukimwacha atanidhuru," Nyagombe alisema.

"Wana mbinu nyingi hawa, ngoja nikwambie wakikuona mjuaji wanapanga na daktari, wanakuchoma sindano wanakuua, na si mara ya kwanza kuua watu.

"Nilipanga nije nikuambie mambo yote lakini Mungu katukutanisha nikuambie, nikitoka nitakuletea mambo yote ya jela. Lakini huyu usimwache, ukimwacha, utaandika maelezo ya mauaji, uwiiii!"

INAENDELEA UK. 26

## HABARI KITAIFA



Mtuhumiwa raia wa Misri, Hany Ahmed, akiwa chini ya ulinzi wa askari polisi, baada ya kusomewa mashtaka ya kutorosha madini bila kibali, yenye thamani ya Sh. milioni 12, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mchungaji matatani tuhuma za kubaka, kumpa ujauzito bintiye

**Na Gurian Adolf,** KATAVI

POLISI mkoani Katavi wanamshikilia Mchungaji Boaz Yohane (56) wa Kanisa la Free Pentecoste (FPCT), mkazi wa Kijiji cha Keswa, wilayani Mpanda kwa tuhuma za kumbaka na kumpatia ujauzito mtoto wake wa kumzaa mwenye umri wa miaka 17.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi, Benjamin Kuzaga, alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa na polisi juzi majira ya saa 4:00 asubuhi kijijini hapo.

Alisema mchungaji huyo alikuwa akiishi nyumbani mtoto wake huyo wa kike ambaye alikuwa mwanafunzi wa kidato cha kwanza (jina la shule linahifadhiwa).

Kuzaga alisema mtuhumiwa alitumia nafasi hiyo ya kuishi peke yake na mtoto wake huyo na kufanya naye

INAENDELEA UK. 26

# HESLB yawafuata wakopaji jeshini

**Na Romana Mallya**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), imeanza kuendesha programu za elimu kuhusu uombaji mikopo kwa wanafunzi waliomaliza kidato cha sita mwaka huu ambao wapo katika kambi 17 za Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) nchini.

Programu hizo ni mwendelezo wa programu za elimu ya uombaji mikopo kwa usahihi ambazo HESLB iliziendesha mwezi Aprili na Mei, mwaka huu katika shule 119 za sekondari zilizopo kwenye mikoa 17 na kuwafikia wanafunzi 27,913 waliokuwa wanajiandaa na mitihani ya kitaifa ya kidato cha sita iliyomalizika mwishoni mwa mwezi Mei, mwaka huu.

Akizungumza juzi katika kambi ya JKT Ruvu, Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru, alisema lengo la programu hizo ni kuwawezesha wanafunzi kuomba mikopo kwa usahihi na hatimaye wenye sifa wapate mkopo na elimu ya juu.

"Kwa kushirikiana na wadau wetu, likiwamo JKT, tumedhamiria kuwafikia wahitaji wa mikopo pale walipo, ndiyo sababu tupo hapa na wenzetu wapo katika kambi nyingine kama 16. Ikumbukwe tuliendesha programu kama hizi katika Shule ya Sekondari Tanzania Bara na Zanzibar," alisema.

"Kwa mwaka 2019/2020, serikali imeongeza bajeti ya fedha mikopo kutoka Sh. bilioni 427.5 hadi Sh. bilioni 450, zinazotarajia kuwanufaisha jumla ya wanufaika 125,000 wakiwamo wa mwaka wa kwanza zaidi ya 45,000."

Alisema mwaka huu wa masomo unaomalizika Sh. bilioni 427.5 zimewanufaisha jumla ya wanafunzi 123,285 wakiwamo 41,345 wa mwaka wa kwanza.

Alitaja kambi zenye wahitimu wa kidato cha sita kuwa ni Bulombora, Kanembwa na Mtabila, zilizopo mkoani Kigoma, Rwamkoma (Mara), Msange (Tabora), Nachingwea (Lindi), Mpwapwa na Makutupora (Dodoma), Mgambo na Maramba (Tanga).

"Nyingine ni Makuyuni (Arusha), Mafinga (Iringa), Mlale (Ruvuma), Itaka na Luwa (Songwe) na Milundikwa iliyopo mkoani Rukwa," alisema.

Badru alisema uzoefu wa miaka iliyopita ndiyo umeifanya HESLB kuandaa programu hizo kutokana na kuonyesha mafanikio kupitia aina ya maswali yanayoulizwa.

"Tunawaeleza kuhusu nyaraka muhimu zinazotakiwa kuambatishwa, namna sahihi

INAENDELEA UK. 26

# IGP: Mikutano ya ndani vyama vya siasa haijapigwa marufuku

**Na Joseph Mwendapole**

MKUU wa Jeshi la Polisi nchini, (IGP) Simon Sirro, amesema mikutano ya ndani ya vyama vya siasa haijapigwa marufuku kama inavyozungumzwa.

Akizungumza na askari kwenye ziara yake ya kikazi mkoani Tabora jana, IGP Sirro alisema mikutano hiyo inaweza kusitishwa tu pale itakapoonekana kwamba kuna viashiria vya uvunjifu wa amani.

"Mikutano ya ndani halijapigwa marufuku popote ila kama kuna taarifa za tishio la usalama kwenye mkutano huo tunaweza kuzuia kwa faida ya Watanzania," alisema.

IGP Sirro alisema mikutano hiyo inaruhusiwa kunapokuwa na mazingira ya amani na kwamba wahusika wanachotakiwa kuzingatia ni kufuata sheria na taratibu zilizowekwa kila wakati.

"Tunapokuwa tumezuia mikutano ya ndani watu wazingatie sheria na watii kwa sababu askari wanakuwa na taarifa zinazoweza kusababisha vurugu sasa tunawataka wahusika watii amri za polisi," alisema IGP Sirro.

Alisema imekuwa kawaida kwa baadhi ya

INAENDELEA UK. 8


## ABBOTT FUND TANZANIA

(Company No. 58641)
(Certificate of Compliance No. 1828)

**PUBLIC NOTICE MADE PURSUANT TO REGULATION 13 (A) OF THE NON GOVERNMENTAL ORGANISATION ACT (AMENDMENTS) REGULATIONS 2018 MADE UNDER GOVERNMENT NOTICE NO. 609 OF 19TH OCTOBER 2018**

**WHEREAS** Regulation 13 (a) of the abovementioned regulations require that all non-governmental organisations in Tanzania publish bi annually funds received and their expenditure in a widely circulated newspaper which are accessible by the targeted beneficiaries as part of financial transparency and accountability compliance requirements.

**IN VIEW OF THE ABOVE**, we wish to make the following public disclosure for the budget year 2018:

| Project Area Expenditure | Budget (USD) |
|---|---|
| **Muhimbili National Hospital Sustainability Strategy Support:** Includes support to Emergency Medicine; Central Pathology Laboratories; Leadership Capacity-Building | 720,000 |
| **Regional Laboratories and Laboratories IT Projects; Mentorship** | 537,000 |
| **Building Livelihoods**: Includes National Children's Centre Infrastructure Project (Dodoma) | 223,000 |
| **Administration:** Includes travel, office costs and program implementation staff | 1,802,000 |
| **Total Funds received from Abbott Fund, Chicago IL, USA for the year 2018** | **3,282,000** |

ISSUED BY
EXECUTIVE DIRECTOR
ABBOTT FUND TANZANIA

115325602

# 500 wapatiwa miguu bandia

**Na Mary Geofrey**

WATANZANIA 551 wamepata miguu bandia bila malipo katika kambi ya kutoa huduma hiyo iliyofanyika kwenye Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI) kwa kushirikiana na Taasisi ya BMVSS ya India.

Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respicious Boniface, akizungumza wakati wa kufunga kambi hiyo juzi jijini Dar es Salaam, alisema imefanyika kwa mafanikio makubwa.

Alisema kambi hiyo iliendeshwa kwa siku 42 ikiushirikisha pia Ubalozi wa India nchini na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

"Kwa namna ya pekee, niwashukuru wataalamu kutoka India kwa moyo wa upendo wa kujitolea kufanya kazi hii ya kuwasaidia Watanzania wenye uhitaji wa miguu bandia.

"Vilevile, niwashukuru na kuwapongeza wataalamu wa MOI

INAENDELEA UK. 8



Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe (wa tatu kushoto), akikagua vitendea kazi vya kisasa vilivyofungwa katika karakana ya MT. Depot, iliyopo jijini Dar es Salaam inayosimamiwa na wakala wa ufundi na umeme (TEMESA), wakati alipofanya ziara ya kikazi katika karakana hiyo, jana. **PICHA: WUUM**

# Waziri akunwa kampuni kuinua vijana wakulima

**Na Mwandishi Wetu,** KILOSA

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Kazi, Ajira na Watu Wenye Ulemavu), Anthony Mavunde, ameisifu kampuni ya mbolea ya Petrobena East Africa Ltd kwa kuhakikisha wakulima wa Tanzania, hususani vijana, wanapata maendeleo kupitia sekta ya kilimo.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya uzinduzi wa mavuno ya mpunga katika shamba lenye ukubwa wa ekari zaidi ya 50 la vijana wa Agri-Ajira, katika Kijiji cha Mambegwa wilayani Kilosa Mkoa wa Morogoro, Naibu Waziri alisema mchango wa kampuni hiyo katika kuinua sekta ya kilimo ni mkubwa.

"Naipongeza sana kampuni hii chini ya uongozi wa Peter Kumalilwa kwa kutembea kwenye

INAENDELEA UK. 8




# PPRA yaokoa fedha za serikali bil. 46/-

**Na Beatrice Shayo**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) imeisaidia serikali kuokoa Sh. bilioni 46.91 ambazo zingepotea kutokana na kutokufuatwa kwa taratibu za ununuzi na usimamizi wa mikataba.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Ofisa Mtendaji Mkuu wa PPRA, Mhandisi Leonard Kapongo, wakati wa kongamano la saba la Usimamizi wa Manunuzi ya Umma.

Alisema fedha hizo zimeokolewa katika kipindi cha mwaka 2016/17 hadi 2017/18, zilibainika wakati PPRA ikifanya uchunguzi maalum ili kubaini ukiukwaji wa taratibu za manunuzi.

Kapongo alisema fedha zilizookolewa ni malipo ya makandarasi na watoa huduma kinyume na utaratibu na hivyo taasisi hizo zikaelekezwa kurejesha fedha hizo.

Vile vile, alisema PPRA inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo baadhi ya taasisi kutotoa ushirikiano wakati wa ukaguzi. Alisema baadhi ya taasisi kutowasilisha PPRA ripoti na taarifa mbalimbali za zabuni kwa wakati hivyo kuikwamisha mamlaka katika utekekeza majukumu yake.

"Baadhi ya taasisi za serikali kutokusimamia ipasavyo utekelezaji wa mikataba ya manunuzi na kukwamisha upatikanaji wa thamani bora ya fedha," alisema.

Kapongo alisema kuna changamoto ya uhaba wa watumishi wenye taaluma ya manunuzi katika taasisi zinazoshughulikia masuala ya manunuzi ya umma, kuanzia ngazi ya usimamizi hadi utekelezaji na kuathiri utendaji wa taasisi husika.

"Ufanisi mdogo kwa baadhi ya taasisi za serikali katika kuendesha michakato ya zabuni, hivyo kusababisha ongeleko la gharama na muda katika utekelezaji wa miradi," alisema Kapongo. Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, aliagiza yeyote aliyehusika na upotevu wa fedha za serikali kuchukuliwa hatua kali ikiwa ni pamoja na kurejesha fedha za serikali.

"Nilivyosikia kuna fedha za serikali takribani bilioni 46.9 zimeokolewa na chunguzi zilizifanywa na PPRA katika taasisi za umma katika miaka miwili tu kwa kukagua taasisi chache, naagiza waliohusika na upotevu wa fedha za serikali kuchukuliwa hatua kali," alisema. Jafo alisema bodi za wakurugenzi na maofisa masuhuli wa taasisi za serikali wanahusika moja kwa moja katika kuhakikisha sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa katika manunuzi ya umma zinafuatwa kwenye taasisi. Alisema uadilifu ndiyo msingi mkubwa wa uzalendo na huwezi kuwa tishio iwapo uwazi na iwajibikaji utakosekana katika manunuzi ya umma.

"Manunuzi yanaweza kutoa mwanya kwa watendaji wa sekta ya umma na binafsi kutumia fedha za umma kujinufaisha binafsi. Manunuzi ni sehemu kubwa ya shughuli za kiuchumi na hivyo huvutia sana vitendo vya rushwa na udanganyifu jambo ambalo lina athari kubwa kwa fedha za walipa kodi," alisema Jafo. Awali Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya PPRA, Prof. Sufian Bukurura, alisema wana uhaba wa rasilimali watu hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu kwani waliopo ni 74 ikilinganishwa na mahitaji ya wafanyakazi 152. Alisema wanaiomba serikali iwaongezee watumishi kulingana na mahitaji kwa kuwa upungufu huo unaifanya PPRA isiweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu kama vile kukagua taasisi nunuzi za kutosha kila mwaka.

Prof. Bukurura alisema ufinyu wa bajeti ambao unaifanya PPRA ishindwe kutekeleza majukumu yake kikamilifu hususani kwenye eneo la ukaguzi na kila mwaka PPRA hufanya kaguzi kwa wastani wa taasisi 100 tu kati ya taasisi zaidi ya 500 zilizopo.

# HABARI KITAIFA

## Kizimbani kujifanya maofisa Takukuru

**Na Hellen Mwango**

WAKAZI watatu wa jijini Dar es Salaam wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, wakikabiliwa na mashtaka matatu ikiwamo kuomba rushwa ya Sh. milioni 300, kula njama na kujifanya maofisa wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru).

Washtakiwa hao ni, wafanyabiashara Mohammed Sadiq (25), Daniel Ileme (35) na Ofisa Mauzo wa Hoteli ya Ramada, William Mjatta (36).

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Augustina Mmbando.

Katika shtaka la kwanza ilidaiwa kuwa, kati ya Mei Mosi na Juni 10, mwaka huu, katika mikoa ya Dar es Salaam na Arusha, washtakiwa wote watatu walishawishi rushwa ya Sh. milioni 300 kutoka kwa Francis Matunda.

Ilidaiwa kuwa washtakiwa walishawishi rushwa hiyo ili kumsaidia kuzuia deni la Sh. bilioni moja alizokuwa anadaiwa na wafanyakazi wa Ulanga Mine.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa kati ya Mei Mosi na Juni 10, mwaka huu, washtakiwa walikula njama ya kujifanya maofisa wa Takukuru huku wakijua si kweli.

Katika shtaka la tatu ilidaiwa kuwa, Juni 10, mwaka huu kati ya mikoa ya Dar es Salaam na Arusha washtakiwa wote watatu walidanganya kuwa ni maofisa wa Takukuru huku wakijua si kweli.

Washtakiwa walikana mashtaka yote.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa hauna pingamizi la dhamana na kwamba upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika uliomba tarehe nyingine ya kitajwa.

Hakimu aliwataka washtakiwa kujidhamini kwa Sh.milioni 50 taslimu au kuwasilisha hati ya mali isiyohamishika yenye thamani hiyo ya fedha, kuwa na wadhamini wawili watakaotia saini hati ya dhamana yenye thamani hiyo ya fedha.

Kesi hiyo itatajwa Julai 30, mwaka huu washtakiwa wameshindwa kutimiza masharti ya dhamana.

## Waombaji pasi kusafiria sasa kulipa kwa M-Pesa

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Vodacom Tanzania kwa kushirikiana na Idara ya Uhamiaji nchini, wamezindua huduma mpya iitwayo 'Malipo ya Pasipoti kwa M-Pesa'.

Huduma hiyo mpya ilizinduliwa jana katika hafla fupi katika ofisi za makao makuu ya Uhamiaji, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza katika uzinduzi huo Mkurugenzi wa M-Commerce, Epimack Mbeteni, alisema huduma hiyo mpya inalenga kuwawezesha wateja wa kampuni hiyo kufanya malipo kwa haraka na urahisi zaidi.

"Napenda kuwataarifu wateja wetu na Watanzania kwa ujumla kwamba, sasa wanaweza kulipia hati zao uhamiaji kwa kupitia M-Pesa."

"Ili mteja aweze kulipia inabidi aingie kwenye menu ya M-Pesa na kufuata utaratibu wa kulipa malipo ya serikali au kupitia zana (app) M-Pesa. Lengo letu ni kuhamasisha Watanzania wapate hati mpya za kielektroniki, lakini pia kuwasogezea huduma za malipo viganjani kwao, ndio maana tumeona umuhimu wa kushirikiana na Uhamiaji kufanikisha hili," aliongeza Mbeteni.

Huu ni mkakati wa kuwarahisishia waombaji wa hati za kusafiria ulipaji wa malipo kwa Idara ya Uhamiaji, kwa vile walikuwa wakipanga foleni na kusubiria kwa muda mrefu ili kukamilisha malipo hayo.

Kamishna wa Pasipoti wa Uhamiaji, Marry Palmer, alisema: Tuna furaha kuungana na Vodacom Tanzania kuwawezesha wateja kufanya malipo kirahisi, vile vile kuiwezesha idara yetu kufanya kazi kwa urahisi zaidi. Nategemea kuona bunifu nyingi zaidi kutoka Vodacom."

Vodacom imedhamiria kufikia idadi kubwa ya watu ambao hawapo kwenye mifumo rasmi ya kifedha, kuchochea ujumuishwaji, na uwezeshaji kupitia huduma rafiki na salama hivyo hii ni moja ya njia ya kufanikisha lengo hilo.

"Tunaendeleza nia ya kubadili Tanzania kuwa jamii inayofanya malipo kidijitali, tunawekeza katika teknolojia ya simu ambayo itaingiza watu wengi zaidi katika mifumo ya kifedha na hatimaye, kufikia malengo ya kijamii na kiuchumi ya nchi," alisisitiza Mbeteni.

## Wanafunzi wabunifu waomba vifaa vyao kutangazwa

**Na Romana Mallya**

WABUNIFU wa vifaa mbalimbali vyuoni wameiomba serikali na wadau wengine kutoa kipaumbele kwa kuvitumia na kuvitangaza kitaifa na kimataifa vitu walivyobuni ili wanapomaliza masomo yao wasingoje ajira.

Hayo yalisemwa kwa nyakati tofauti na wanafunzi wavumbuzi wa vifaa mbalimbali walivyovitengeneza kupitia mafunzo waliyoyapata Chuo cha Kumbukumbu cha Mwalimu Nyerere (MNMA), kilichopo Kigamboni jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe katika maonyesho ya vyuo vikuu yaliyoandaliwa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), mwanafunzi MNMA kutoka Idara ya Habari, Teknolojia na Mawasiliano (Tehama), kampasi ya Kivukoni, Ramadhan Abushiri, alisema ametengeneza mfumo ambao unasaidia kuzuia ajali zinazotokana na gesi ya majumbani.

"Serikali ndiyo inayoweza kutuwezesha kutambuliwa kimataifa kwa kutumia mifumo tunayobuni vyuoni kwa kuwa wa kwanza kutumia na kututambulisha kimataifa ili badala ya kutegemea ajira tunapomaliza vyuo, tuendeleze kazi za ubunifu," alisema.

Pia aliiomba serikali na wadau wengine wawawezeshe kupata mazingira ya kufanyia shughuli zao wamalizapo vyuo kwa sababu upatikanaji wa vifaa wanavyovitumia kutengeneza vifaa hivyo ni mgumu.

Akielezea kuhusu mfumo huo aliotengeneza, alisema endapo ikitokea gesi imevuja nyumbani, kupitia mfumo wa kifaa hicho alichobuni utafunga mtungi usiendelee kuvuja, utatoa ile iliyovuja na kisha utatuma ujumbe mfupi kwa mhusika kumtaarifu kuna hatari ya gesi imetokea. Mwanafunzi mwingine wa Stashahada ya Tehama chuoni hapo, kampasi ya Zanzibar, Jenifer Liwa, alisema amefika kwenye maonyesho hayo kuonyesha mfumo alioubuni wa sola ambao unasogea wenyewe kufuata mwenendo wa jua tofauti na nyingine zinazokaa sehemu moja.

"Vijana tunaotoka vyuo tunatakiwa tuwe wabunifu elimu tunayopata tusisubiri ajira, tubuni vitu mbalimbali. Rais John Magufuli ametuambia tunaelekea uchumi wa viwanda, lazima tuwe wabunifu tuvumbue vitu ili tuendane na kasi ya Rais wetu," alisema.

Pia aliiomba serikali iwasaidie kupata mikopo ili ubunifu walioubuni vyuoni wauendeleze ili kuliwezesha taifa kuongeza uchumi, kutoa ajira na Tanzania iendelee kushindana na nchi nyingine kwenye ushindani wa masoko.


**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU**

**TAARIFA KWA UMMA**

**FURSA YA MAFUNZO KUKUZA UJUZI KWA NJIA YA UANAGENZI**

1. **Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana Ajira na Wenye Ulemavu** inatekeleza Programu ya Kukuza Ujuzi kwa njia mbali mbali ikiwemo uanagenzi, mafunzo ya vitendo mahali pa kazi na utambuzi wa ujuzi uliyopatikana nje ya mfumo rasmi wa mafunzo. Katika kufanikisha utekelezaji wa Programu hii, Ofisi ya Waziri Mkuu imeingia mkataba na Taasisi ya **Don Bosco Net Tanzania** iliyopo Oysterbay Dar es salaam wa kutoa mafunzo katika fani mbalimbali. Lengo ni kuwezesha vijana kuwa na ujuzi unaohitajika katika soko la ajira na kuongeza wigo mpana wa kujiajiri au kuajiriwa au kuendelea na mafunzo ngazi ya juu. Fani zitakazofundishwa ni . Mafunzo ya kukuza ujuzi yanafanyika Mikoa yote ya Tanzania Bara na yataanza kwa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza itaanza Mwezi Julai inayojumuisha mikoa 12 na Awamu ya pili itaanza Mwezi Agosti, 2019 itakayojumuisha mikoa 14.

**2. Mikoa na Vituo vitakavyotoa Mafunzo**
Vituo vilivyokubalika na Serikali kutoa mafunzo hayo kwa kushirikiana na Taasisi ya Don Bosco Net Tanzania pamoja na fani zitakazotolewa ni:

| | ENEO | CHUO | FANI |
|---|---|---|---|
| 1 | MUSOMA - MARA | ST. ANTHONY VTC | Ufundi umeme |
| | | | Kubuni mitindo ya mavazi na Ushonaji |
| | | | Uashi |
| | | | Mapishi ya vyakula |
| 2 | GEITA (Location: Moringe sokoine & Sophia Town) | GEITA VOCATIONAL TRAINING CENTER | Ufundi magari |
| | | | Ufundi umeme |
| | | | Ufundi umeme wa magari |
| | | | Kubuni mitindo ya mavazi na ushonaji |
| | | | Utengenezaji wa kompyuta |
| | | | Uashi |
| | | | Ufundi bomba |
| | | | Useremala |
| | | | Kuweka terrazzo na vigae |
| 3 | DAR ES SALAAM | DON BOSCO OYSTERBAY VTC | Ufundi wa magari |
| | | | Useremala |
| | | | Uchomeleaji vyuma |
| | | | Uchongaji vipuri |
| | | | Terrazo na Vigae |
| | | | Kutengeneza Kompyuta |
| | | | Ufundi umeme |
| | | | Ufundi umeme wa jua (solar) |
| | | | Kubuni mitindo ya mavazi na ushonaji |
| | | MATUMAINI YOUTH TRAINING CENTRE | Mapishi ya vyakula |
| | | | Utengenezaji wa kompyuta |
| | | | Kubuni Mitindo ya Mavazi na Ushonaji |
| | | DON BOSCO YOUTH CENTRE UPANGA | Kutengeneza Kompyuta |
| | | | Kubuni mitindo ya Mavazi na Ushonaji |
| 4 | DODOMA | DON BOSCO DODOMA TECHNICAL INSTITUTE | Ufundi magari |
| | | | Useremala |
| | | | Ufundi Bomba |
| | | | Uashi |
| | | | Terrazo na Vigae |
| | | | Mapishi ya vyakula |
| | | | Kutengeneza kompyuta |
| | | | Kuhudumia vyakula na vinywaji |
| | | | Uchomeleaji vyuma |
| | | | Uchongaji vipuri |
| | | | Ufundi umeme |
| | | | Ufundi umeme wa jua (solar) |
| | | | Kubuni Mitindo ya mavazi na Ushonaji |
| 5 | IRINGA | DON BOSCO YOUTH TRAINING CENTRE IRINGA | Ufundi magari |
| | | | Useremala |
| | | | Ufundi Bomba |
| | | | Uashi |
| | | | Utengenezaji Kompyuta |
| | | | Uchomeleaji Vyuma |
| | | | Ufundi Umeme |
| | | | Ufundi umeme wa Jua |
| | | | Kubuni Mitindo ya mavazi na ushonaji |
| | | DON BOSCO MAFINGA | Utengenezaji wa Kompyuta |
| | | | Kubuni Mitindo ya Mavazi na Ushonaji |
| 6 | SHINYANGA | OLA SISTERS VTC-BUGISU | Kutengeneza Kompyuta |
| | | | Ufundi Umeme |
| | | | Uchakataji wa vyakula ( food processing) |
| | | | Kubuni mitindo ya mavazi na ushonaji |
| | | ST. FRANCIS DE SALES TECHNICAL INSTITUTE- MWAKATA-ISAKA | Kubuni Mitindo ya Mavazi na Ushonaji |
| 7 | ARUSHA | KIITEC-MOSHONO | Ufundi Umeme wa Jua (solar) |
| | | | Kutengeneza Kompyuta |
| | | | Ufundi umeme |
| 8 | MOSHI - KILIMANJARO | DON BOSCO MOSHI | Kutenegeneza Kompyuta |
| | | | Mafunzo ya ufugaji |
| | | | Kilimo cha matunda, maua (horticulture crops) |
| 9 | BUKOBA - KAGERA | KASHOZI HOME CRAFT VTC | Kubuni mitindo ya mavazi na Ushonaji |
| | | | Mapishi ya vyakula |
| 10 | SINGIDA | RC MISSION VTC MANYONI | Kubuni mitindo ya mavazi na ushonaji |
| | | | Mapishi ya vyakula |
| 11 | LINDI | LINDI RVTSC - VETA | Uchomeleaji Vyuma |
| | | | Ufundi umeme |
| | | | useremala |
| | | | Uashi |
| | | | Ufundi magari |
| 12 | RUVUMA | PERAMIO VOCATIONAL TRAINING CENTRE | Kubuni Mitindo ya Mavazi na Ushonaji |
| | | | Ufundi magari<br>Ufundi bomba |
| | | | Ufundi umeme |
| | | | Kuchapa vitabu, Makala na nyaraka |
| | | | Uashi |
| | | | Ufugaji |
| | | | Useremala |
| | | | Utengenezaji wa Komyuta |
| 13 | MOROGORO | HOLY CROSS SOCIAL TRAINING CENTRE | Kubuni mitindo ya mavazi na ushonaji |
| | | | Utenegenezaji wa kompyuta |
| | | | Mapishi ya Vyakula |

**3. Sifa za Kujiunga na Mafunzo**

Kwa wote wanaopenda kujiunga na mafunzo wanapaswa kuwa na sifa zilizoainishwa hapa chini :
(a) Elimu ya Msingi au zaidi kwa fani za Nguo, Mitindo na Ushonaji, Ufundi bomba, Ujenzi, Useremala, Uchomeleaji na Uungaji vyuma;
(b) Elimu ya kidato cha nne kwa fani ya Utengenezaji wa vipuri vya mitambo, Ufundi magari, umeme wa majumbani na viwandani, TEHAMA, Umeme wa magari, Umeme wa jua (Solar) na kuchapa vitabu;
(c) Awe Mtanzania;
(d) Awe na umri kati ya miaka 18 – 35; na
(e) Awe mwenye Afya njema

4. Fomu zitatolewa bila malipo katika vyuo husika kuanzia tarehe tarehe 17 hadi 23 Julai, 2019. Mwombaji anatakiwa kurudisha fomu kuanzia tarehe 24-26 Julai ikiambatana na:
(a) Barua ya maombi yenye anuani kamili ikiwa na namba za simu pamoja na barua pepe (kama anayo);
(b) Nakala ya Cheti cha Elimu uliyohitimu;
(c) Nakala ya Cheti cha kuzaliwa au Kitambulisho cha uraia au kadi ya mpiga kura;
(d) Barua ya utambulisho kutoka Serikali ya Mtaa anaoishi mwombaji (lazima); na
(e) Picha nne za paspoti zenye rangi ya bluu kwa nyuma.

5. Vijana watakao kidhi vigezo watafadhiliwa na Serikali kwa asilimia 100 kwa kulipiwa ada ya mafunzo yatakayofanyika katika vyuo vilivyotajwa hapo juu kwa muda wa miezi sita. Kijana atakayechaguliwa atagharamiwa kiasi cha **Tsh. 100,000/-** kwa mwezi kama nauli ya kwenda chuoni na kurudi nyumbani. Mafunzo ni ya kutwa na yataanza rasmi tarehe **19 Agosti, 2019.** Hivyo, inashauriwa kwamba kijana kuomba mafunzo haya katika kituo kilicho karibu au ambapo atapata pa kuishi. Mwombaji atatakiwa kurejesha fomu ya maombi yeye mwenyewe katika chuo husika kabla ya tarehe **26 Julai, 2019.** Tangazo la mafunzo katika mikoa mingine ya awamu ya pili litatolewa kuanzia tarehe **22 Julai, 2019.**

**Imetolewa na :**
**Katibu Mkuu,**
**17.07.2019**

215326462

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Elimu ya mikopo sawa, lakini HESLB ipanue wigo wanufaika

**TAARIFA** kwamba Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), imeanza kuendesha programu za elimu kuhusu uombaji wa mikopo kwa wanafunzi waliomaliza kidato cha sita mwaka huu ambao wapo katika kambi 17 za Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) nchini, ni hatua ya kuungwa mkono.

Programu hizo ni mwendelezo wa programu za elimu ya uombaji mikopo kwa usahihi ambazo HESLB iliziendesha mwezi Aprili na Mei, mwaka huu katika shule 119 za sekondari zilizopo kwenye mikoa 17 na kuwafikia wanafunzi 27,913 waliokuwa wanajiandaa na mitihani ya kitaifa ya kidato cha sita iliyomalizika mwishoni mwa mwezi Mei, mwaka huu.

Akizungumza juzi katika kambi ya JKT Ruvu, Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru, alisema lengo la programu hizo ni kuwawezesha wanafunzi kuomba mikopo kwa usahihi na hatimaye wenye sifa wapate mkopo na elimu ya juu.

Alisema kwa kushirikiana na wadau wao, likiwamo JKT, HESLB imedhamiria kuwafikia wahitaji wa mikopo pale walipo, ndiyo sababu walikwenda kambini hapo na kambi nyingine kama 16.

Mkakati huo wa HESLB tunaona kuwa una lengo zuri kutokana na huko nyuma mchakato wa uombaji wa mikopo kuonekana na vikwazo kwa waombaji wengi hususan vijana ambao wanakuwa wamehitimu kidato cha sita.

Kukosekana kwa elimu katika mchakato wa uombaji wa mikopo kumekuwa kukisababisha vijana hao kukosa kwa sababu tu waliomba bila kufuata taratibu sahihi, hivyo wengi kujikuta mwisho wa siku wakikosa kujiunga na vyuo vya elimu ya juu.

Bodi ya Mikopo iliweka vigezo mbalimbali ambavyo kila mwombaji anatakiwa kuvikidhi, hivyo kuanzisha na kutekeleza programu ya elimu ya kuomba mikopo ni ishara kwamba imedhamiria kuwasaidia waombaji ili wasikwazike.

Pia hatua ya kuwafuata wahitimu wa kidato cha sita ambao wako kwenye kambi za jeshi, unawarahisishia kuomba mikopo kwa usahihi. Hii ni kwa sababu wasingepata msaada kulinganisha na wale waliohitimu masomo bila kupita JKT.

Mbali na kuipongeza HESLB kwa kubuni na kutekeleza programu hiyo, tunashauri elimu hiyo iwe endelevu shuleni kwa wanafunzi ambao wanatarajia kuhitimu na waliopitia kwenye kambi za JKT.

Wahitimu ambao hawapitii JKT angalau wanakuwa na fursa ya kupata msaada kwa watu wengine wenye uelewa katika kujaza fomu za maombi kwa usahihi.

Kwa mwaka ujao wa masomo tunaishauri Bodi ya Mikopo iendelee kuboresha mazingira ya utoaji wa mikopo ili walengwa wengi wanufaike na kusoma bila changamoto.

Kumekuwapo na dhana kuwa vijana waliosoma shule za binafsi hawana haki ya kupata mikopo kwa madai kuwa wazazi na walezi wao wana uwezo kiuchumi.


Hata hivyo, kiuhalisia dhana hii haina ukweli kwa kuwa kuna wazazi na walezi ambao baadaye wanaathirika kiuchumi, hivyo kukosa uwezo wa kuwasomesha wategemezi wao.

Aidha, wapo baadhi ya wazazi na walezi ambao wanawasomesha wategemezi wao katika shule binafsi, lakini wanapostaafu nguvu zinapungua sambamba na kipato, hivyo, kuwa vigumu kwao kugharamia elimu ya juu.

Katika mazingira haya, tunaona kuwa kuna sababu za msingi kwa HESLB kuachana na dhana hii, badala yake ifuatilie kwa karibu ili waombaji wa aina hii wapatiwe mikopo kwa kuwa ni haki yao kama Watanzania wengine.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Watanzania ni wakati wa kuvuna mafanikio SADC

Na Beatrice Moses

**MKUTANO** wa 39 wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) unafanyika jijini Dar es Salaam ukitanguliwa na maadhimisho ya awamu ya nne ya Wiki ya Maonyesho ya Viwanda ya SADC yaani '4th SADC Industrialization Week'.

Tanzania ndiyo mwenyeji na Rais John Magufuli, anatarajiwa kukabidhiwa uenyekiti wa SADC katika mkutano huo, ambao utakutanisha marais 16 wa nchi wanachama utafanyika Agosti mwaka huu jijini Dar es salaam.

Wahenga walisema 'mgeni njoo mwenyeji apone' hivyo hii ni nafasi mujarabu kwa Watanzania kuitumia fursa hiyo kujinufaisha kiuchumi, biashara na kisiasa.

Yawezekana wapo ambao wanafikiria kuwa jambo hili haliwahusu bali ni la wafanyabiashara, wajasiriamali na maofisa kadhaa wa serikali, la si hivyo, ukweli ni kwamba linawahusu wote kwa pamoja kama Watanzania.

Kila mmoja anawajibika katika hili lakini kulingana na kazi yake anayoifanya lakini pia kama raia mwema, kwa pamoja wanapaswa kushiriki kikamilifu ili kulinda heshima ya nchi.

Ni wazi kwamba wafanyabiashara, wamiliki wa kampuni, wajasiriamali na maofisa wa serikali wamejipanga kwa namna yao wamekubaliana, lakini pia hata wananchi wengine wanapaswa kushiriki kikamilifu kuhakikisha wageni hao wanaishi kwa amani.

Tanzania ni kisiwa cha amani ndivyo ambavyo imekuwa ikijulikana, kwa hiyo ni wazi kwamba wageni wataikuta amani hiyo, ndiyo maana nimeeleza kuwa ni ugeni wa wote wakiwamo wanajamii wote.

Nasema hivyo kwa kuwa haitaleta picha nzuri kama mitaa itakuwa na uchafu wageni wakastaajabu katika hilo, tuamini kwamba wanapaswa kufurahia mazingira ya nchi na wasihofu kuwa watakumbwa na magonjwa kama vile kipindupindu na dengue.

Tunatambua kwamba kuna polisi ambao wanawajibika katika kuhakikisha ulinzi na usalama wa raia na wageni lakini ikumbukwe haipaswi kuwaachia pekee yao bali kama jamii nayo inapaswa kushiriki kwenye ulinzi (ulinzi shirikishi) katika maeneo yote ili kudhibiti vitendo vya uhalifu kwa ujumla.

Mfano katika eneo ambapo maonyesho hayo yanatarajiwa kufanyika kwenye ukumbi wa Mlimani City, kuanzia Julai 22 hadi 26 mwaka huu, halipaswi kuachia mwanya kwa vibaka.

Polisi wakishirikiana na walinzi wa jamii wa maeneo hayo wanapaswa kuhakikisha wanadhibiti uhalifu ukiwamo wizi wa kukwapua kwa kutumia usafiri wa pikipiki, pia wenyeji ambao watakuwa na jukumu la kuongozana na wageni hao wawe na tahadhali na vibaka.

Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ndiyo waratibu wa maandalizi ya mkutano huo.


Kwa upande wake serikali imechukulia umuhimu wa aina yake kwa kuchukua hatua kadhaa za maandalizi ikiwa ni pamoja na Waziri wa Mambo ya Nje, Profesa Palamagamba Kabudi, kuzungumzia ugeni huo na kutoa wito kwa wafanyabiashara na wajasiriamali kutumia fursa hiyo vyema.

Profesa Kabudi amekaririwa na vyombo vya habari akieleza kuwa wageni wameonyesha nia ya kufanywa kumbukizi ya Mwalimu Julius Nyerere ambaye ni miongoni mwa wanaharakati wa ukombozi wa nchi za Afrika wanaokumbukwa kwa juhudi zao.


Pia Idara ya Habari Maelezo kwa kutambua umuhimu wa vyombo vya habari kushiriki katika jambo hili, kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya wanandaa warsha maalum ya kuwanoa wanahabari kuwajengea uwezo wa kuhabarisha jamii.

Mkurugenzi wa Habari Maelezo na Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbas, anawataka waandishi kutoa habari sahihi ili isaidie jamii kutumia vyema na fursa zitokanazo na mkutano huo wa SADC.

MJADALA




# Ufaulu huu unarudisha hadhi shule za serikali




**Na Sabato Kasika**

WAKATI serikali ya awamu ya nne inaingia madarakani, ilikuja na mkakati wa kuinua elimu nchini kwa kuhakikisha wanafunzi wote wanaofaulu kutoka elimu ya msingi wanaingia sekondari.

Mkakati uliobuniwa ni kuanzisha shule za sekondari kila kata, ambapo hatua hiyo ilisababisha kuongezeka kwa idadi ya walimu, vifaa vya kufundishia, maabara na samani katika shule hizo mpya.

Mbali na hayo, mkakati huo ulikwenda sambamba na kuajiri walimu wa diploma na hata kuwachukua wengine wenye diploma waliokuwa wakifundisha katika shule za msingi ya kuwapeleka sekondari za kata.

Hatua hiyo ilikuwa ni kukabiliana na uhaba wa walimu katika sekondari hizo za kata, kutokana na ukweli kwamba shule hizo zilikuwa nyingi, hali iliyosababisha serikali kuajiri walimu wa leseni (crash program).

Walimu hawa walibandikwa jina la 'Voda Fasta', kwa vile wengi walikuwa ni wale waliohitimu kidato cha sita, ambao kimsingi inawezekana walikuwa hawajafundishwa kanuni na taratibu za ualimu.

Kwa ujumla, mara baada ya shule hizo kufunguliwa zilikabiliwa na matatizo lukuki kuanzia kwenye uhaba wa vitabu, madarasa na walimu wa masomo mbalimbali hasa ya sayansi.

Upungufu wa vyumba vya madarasa ulisababisha baadhi ya shule kubuni utaratibu wa kuwagawa wanafunzi katika mikondo, ambapo baadhi walikuwa wakianza masomo asubuhi na wengine mchana.

Yote hayo yalifanyika lengo kuu likiwa ni kuhakikisha kwamba watoto wote waliofaulu kwenda sekondari wanapata elimu kuliko kukaa nyumbani, ingawa shule hizo ziliendelea kudharaulika.

Baadhi ya wazazi na walezi walizikwepa shule hizo na kupeleka watoto wao katika shule za sekondari za binafsi, wakiamini kwamba ndizo pekee zinazotoa elimu nzuri kuliko zingine.

Lakini jambo la msingi kutambua hapa ni kwamba matatizo ambayo yalikuwa yakizikabili shule hizo hayawezi kutatuliwa kwa mara moja kama ambavyo baadhi ya watu walivyotegemea.

Kwa mtazamo huo watu wenye mawazo hayo walisahau kwamba hata Roma haikujengwa kwa siku moja, ilipitia changamoto nyingi hadi kukamilika kwake.

Hivyo hata sekondari za kata zimepitia hatua hiyo hadi sasa kufikia hatua ya kuanza kufanya vizuri.

Nikirejea kwenye 'Voda Fasta' wakati serikali ilipokuwa ikuchukua wanafunzi waliohitimu kidato cha sita na kuwapeleka kwenye mafunzo ya wiki nne katika vyuo mbalimbali vya ualimu, ninaweza kusema ilichangia shule hizi kutofanya vizuri.

Hiyo ni kwa sababu kutoa mafunzo ya muda mfupi ya ualimu na kisha kutoa ajira kwa maana ya leseni ya ualimu hakutoshi kabisa kufundisha mwanafunzi na akapata kile kilicholengwa.

Na ndiyo maana shule nyingi za kata hazikufanya vizuri, hali iliyosababisha baadhi ya watu kuziona sekondari za kata kana kwamba hazina lolote na kuzibandika majina mbalimbali ya kejeli ikiwamo 'yeboyebo' na mengine mengi.

Hadi leo inawezekana wapo wazazi na walezi, ambao hawataki kupeleka watoto wao katika shule hizo kila wanapofaulu na kupangiwa huko, kwa vile bado wanaamini kwamba hazina lolote.

Lakini sasa watu ambao bado wanaendelea kudharau shule hizo wanapaswa kuzinduliwa na Matokeo ya Kidato cha Sita ya mwaka huu 2029, wakikumbuka kisa Roma kwamba haikujengwa mara moja.

Ninasema hivyo, kwasababu katika shule 100 bora mwaka huu shule 64 ni za serikali, na miongoni mwa hizo 52 ni za kata, shule ambazo kwa muda mrefu zimekuwa zikidharauliwa na baadhi ya watu kana kwamba hazina maana.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Seleman Jafo anawataka wazazi kutosumbua watoto wao kuwahamisha kutoka shule za serikali na kuwapeleka shule binafsi.

Hiyo inatokana na jinsi, ambavyo shule hizo sasa zinaanza kufanya vizuri baada ya changamoto za muda mrefu zilizosababisha zionekane hazifai na kumbe zilikuwa katika kipindi cha mpito tu.

Kwa mujibu wa Waziri Jafo, uwekezaji uliofanywa kwenye sekta ya elimu umechangia ufaulu kupanda ukiwamo wa sekondari za kata ambazo kama nilivyosema zimekuwa zikidharauliwa.

"Shule za serikali zimefanya vizuri ikilinganishwa na ufaulu wa kipindi cha nyuma ambapo kila mtu alizibeza," anasema Jafo.

Siku hizi kuna msemo wa wanasiasa kwamba 'rudini nyumbani kumenoga,' hivyo matokeo ya mwaka huu, yawe chachu kwa wale wanaodharau sekondari za kata ili wawapeleke watoto wao katika shule hizo.

Jambo la msingi kutambua ni kwamba tatizo la shule hizo kutofanya vizuri awali lilikuwa ni changamoto, ambazo sasa zimeanza kutatuliwa, hivyo hakuna sababu ya kuendelea kuzibeza.

TAIFA STARS VS KENYA
JULAI 28, 2019 • UWANJA WA TAIFA
HAIUZWI KWA WALIO NA UMRI CHINI YA MIAKA 18. TAFADHALI KUNYWA KISTAARABU.

# Waziri akunwa kampuni kuinua vijana wakulima

INATOKA UK. 4

barabara ya malengo ya serikali. Mnatekeleza azma ya taifa ya uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025," alieleza.

Mavunde alisema Tanzania haiwezi kufikia azma ya uchumi wa viwanda kama sekta ya kilimo haitafanyiwa mabadiliko makubwa, na kuongeza kwamba wadau wa kilimo, kama Petrobena lazima wajitoe na kuweka nguvu zao zote ili uzalishaji wa malighafi uwe mkubwa na wakutosheleza mahitaji ya viwanda nchini.

Amekisifu kikundi cha Agri-Ajira kwa kuwa na shamba zuri la mpunga.

"Hiki ni kielelezo kwamba vijana wakiaminiwa wanakuwa katika nafasi kubwa ya kuleta matokeo chanya nchini," alisema Mavunde na kuongeza kuwa vijana hao wanatoa funzo kubwa kwa wahitimu wa vyuo nchini ambao wamekuwa na changamoto kubwa katika kupata ajira.

Pia alitoa wito kwa vijana kuacha kusaka kazi na wengine kuchagua kazi katika soko la ajira. Badala yake waitafsiri kwa vitendo elimu wanayoipata vyuoni ili wajijengee kipato na kuchangia pato la taifa.

Mkurugenzi wa Petrobena, Peter Kumalilwa, alimshukuru Naibu Waziri kwa kutembelea shamba hilo na kusema kitendo hicho kitahamasisha vijana kupenda kilimo na kuchochea upatikanaji wa malighafi za viwanda.

"Tunakushuru waziri kwa kuungana na vijana hawa. Kitendo hiki kinawapa hamasa vijana hawa na pia kitawachochea vijana wengine nchini kuanza kuweka nguvu zao katika sekta ya kilimo ambayo ni kiunganishi muhimu kwa uchumi wa viwanda," alisema Kumalilwa.

Kumalilwa alimshukuru Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Steven Kebwe, kwa kuwaongoza vijana hao ambao walihangaika kwa muda mrefu bila mafanikio.

"Tunamshukuru sana Mkuu wa Mkoa kwa kutupatia eneo hili. Lakini pia jitihada zake ndizo zilizotengeneza mazingira ya Petrobena na Agri-Ajira kukutana na leo hii tunashuhudia tukio hili lenye kutia moyo vijana hawa baada ya kuhangaika kwa muda," alieleza.

Samweli Kitila, mwanachama wa Agri-Ajira, alisema haikuwa kazi rahisi kufikia mafanikio hayo kwa sababu vijana wamekumbana na changamoto nyingi.

"Haikuwa kazi rahisi hata kidogo kuziacha shahada zetu na kuamini katika kufanya kazi, uzalendo na weledi mpaka pale tulipokutana na Petrobena East Africa ambao walibadili ndoto zetu na kuwa kitu halisi na kinachowezekana, hakika tunawashukuru sana," alisema Kitila ambaye ni mhitimu wa shahada ya kwanza Chuo Kikuu Kilimo cha Sokoine (SUA).

Petrobena East Africa Ltd, msambazaji mkubwa wa mbolea ya YARA na imekuwa ikiwasaidia kifedha na elimu wakulima wadogo.

## IGP: Mikutano ya ndani vyama vya siasa haijapigwa marufuku

INATOKA UK. 3

wanachama wa vyama vya upinzani kupiga kelele na kupinga hatua ya askari kuzuia mikutano ya ndani hali inayosababisha amani kutoweka kwenye eneo husika.

"Usipotii tunakushughulikia kwasababu hapo unakuwa umesababisha vurugu kwa kujua au kwa kutokujua, lakini sisi tunakushughulikia kama mhalifu tu kwasababu umefanya fujo na hapo usililaumu jeshi," alisema Sirro.

Kuhusu mikutano ya hadhara, IGP Sirro alisema Rais John Magufuli, alisharuhusu wabunge wafanye mikutano kwenye majimbo yao kwa sharti la kutoa taarifa kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya.

Juzi Jeshi la Polisi Mkoa wa Simiyu, lilisambaratisha kwa mabomu ya machozi semina ya kuwajengea uwezo wanawake wa Baraza la Wanawake Chadema (BAWACHA).

Julai 14, Mwenyekiti wa Bawacha, Halima Mdee, alikamatwa na polisi mkoani Kagera wakati wa ziara yake ya kukutana na wanachama wa Bawacha Mkoa wa Kagera.

Hata hivyo, juzi Mdee aliachiwa kwa kudhaminiwa na watu wawili na ametakiwa kuripoti polisi mkoani humo baada ya mwezi mmoja.

AFRICAN CAPITAL

TANGAZO KWA UMMA

Kampuni ya **AFRICAN CAPITAL LTD,** inapenda kutaarifu umma kwamba kuna watu wanatumia jina letu ili kutoa mikopo kwa jina la **AFRICAN CAPITAL MICROFINANCE LTD** wakiwalaghai wananchi kwa kuchukua fedha zao kwa kuwadanganya wanatoa mikopo na baadae kutokomea bila kuwapatia wananchi mikopo walioomba.

Kampuni yetu inapenda kutoa tahadhari kwa wananchi kutoa taarifa endapo watakutana na hao watu ili tuwachukulie hatua ya kisheria. Na tunapenda kuwataarifu wateja wetu na wananchi Kampuni yetu ya **AFRICAN CAPITAL LTD** tunatoa huduma ya mikopo kwa njia halali bila kupokea malipo yoyote kwa wananchi.

215325802

## Shahidi adai kupokea majeruhi watatu

INATOKA UK. 2

Ifuatayo ni sehemu ya mahojiano kati ya wakili wa utetezi na shahidi:

**Wakili:** Shahidi umesema uliambiwa wale watu wako hai ulijiridhisha vipi?

**Shahidi:** Sikuwa na uhakika kama wako hai au la kwa sababu sikuwaona.

**Wakili:** Tukisema kuwa wamefariki tutakuwa tunakosea?

**Shahidi:** Mimi sijui kama wamekufa au la.

**Wakili:** Askari walipofika waliongea chochote kuhusu kuwapiga risasi?

**Shahidi:** Hapana.

**Wakili:** Hali waliyokuwa nayo wangeweza kuruhusiwa kwenda nyumbani?

**Shahidi:** Hapana, ndiyo sababu niliwalaza wodini, Polisi waliwachukuwa wakiwa wodini wakati mimi nikiwahudumia wagonjwa wengine.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa unaomba tarehe nyingine ya kuita mashahidi wengine.

Hakimu Shaidi alisema kesi hiyo itaendelea kusikilizwa ushahidi wa Jamhuri Agosti 13 na 14, mwaka huu.

Katika kesi ya msingi, Zitto anadaiwa kuwa Oktoba 28, 2018, Zitto akiwa katika mkutano na waandishi wa habari, uliofanyika katika Makao Mkuu ya ofisi ya chama cha ACT-Wazalendo, alidaiwa kutoa maneno ya uchochezi yenye kuleta hisia ya hofu na chuki.

Inadaiwa alisema: "Watu ambao walikuwa ni majeruni katika tukio la mapambano baina ya wananchi na polisi wakiwa wamekwenda hospitali kupata matibabu katika Kituo cha Afya Nguruka, Polisi wakapata taarifa kuwa kuna watu wanne wamekwenda hospitali kupata matibabu wakawafuata kule wakawaua".

TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

MASETO AUCTIONEER & DEBT COLLECTOR LTD

Kutakuwepo na mnada wa hadhara wa kuuza dhamana za wadaiwa sugu kwa tarehe kama ilivyopangwa katika jedwali na muda ni kuanzia saa nne asubuhi. Mnada huo utaendeshwa na Dalali tajwa hapo juu kwa niaba ya **TUJIJENGE TANZANIA LTD**

| JINA LA MDAIWA/ MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA | TAREHE YA MNADA | JINA LA DALALI |
|---|---|---|---|---|
| Annastazia T. Masunga | NYUMBA | LAMADI | 25/07/2019 | Maseto D/Collector |
| Lucas J. Cikahand | KIWANJA | LAMADI | 24/07/2019 | Maseto D/Collector |
| Malulu M.B. Daniel | NYUMBA | LAMADI | 24/07/2019 | Maseto D/Collector |
| Mariana Joseph Koronga | NYUMBA | Nyasura – Bunda | 26/07/2019 | Maseto D/Collector |
| Rainas Ndaro Masini | NYUMBA | Karukekere-Bunda | 23/07/2019 | Maseto D/Collector |
| January Mafuru Masini | NYUMBA | Karukekere-Bunda | 23/07/2019 | Maseto D/Collector |
| Salawa M. Shilingo | KIWANJA | LAMADI | 24/07/2019 | Maseto D/Collector |
| Pendo Mwandiki Ngeleja | NYUMBA | LAMADI | 25/07/2019 | Maseto D/Collector |

MASHARTI YA MNADA

1. Dhamana zitauzwa kama zilivyo, Mnunuzi atalipia 25% ya bei itakayofikiwa siku ya mnada, 75% italipwa ndani ya siku 14 kutoka siku ya mnada. Akishindwa kulipa,malipo ya awali hayatarudishwa.
2. Gharama za kubadilisha Hati za Umiliki zitakuwa juu ya mnunuzi
3. Ukaguzi wa mali zinazouzwa utaanza siku moja kabla ya mnada na gharama za kumpeleka mteja kwenye dhamana zitakuwa juu ya mteja

Kwa maelezo zaidi wasiliana na;- TUJIJENGE TANZANIA LTD
Maseto D/Collector: 0744 594358; MOB: 0718276859/0718068335 (HQ).

215326302

## 500 wapatiwa miguu bandia

INATOKA UK. 4

ambao wameshirikiana na wataalamu kutoka India kuendesha zoezi hili," Dk. Boniface alisema.

Alisema sababu za watu kupoteza viungo ni ajali za barabarani na ugonjwa wa kisukari, huku akiweka wazi kuwa kumekuwa na ongezeko la wahitaji wa miguu bandia.

"Vyanzo vikuu vya watu wengi kupoteza viungo vyao ni ajali za barabarani pamoja na ugonjwa wa kisukari, natoa wito kwa jamii kufuata sheria za barabarani ili kuepusha ajali.

"Pia kuepuka mtindo wa maisha unaoweza kupelekea kupata magonjwa ya kisukari, ni muhimu tukafanya mazoezi ili kulinda afya zetu," Dk. Boniface alisema.

Katika hatua nyingine, MOI imeingia mkataba wa ushirikiano wa mafunzo, kubadilishana wataalamu na utaalamu na Taasisi ya BMVSS Jaipur ya India kwa lengo la kuboresha utoaji huduma za miguu bandia nchini.

Mkataba huo ulitiwa saini na Dk. Boniface wa MOI na mwanzilishi na mlezi wa Taasisi ya BMVSS, Dk. Devedra Raj Mehta na kushuhudiwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya MOI, Prof. Charles Mkonyi na Mkurugenzi wa Uendeshaji na Ushirikiano wa Kimataifa wa BMVSS, Satich Mehta.

"Mkataba huu utasaidia sana kwani lengo letu ni kuhakikisha Watanzania wanapata huduma hizi za viungo saidizi na bandia kwa ubora wa hali ya juu ili kuwasaidia hususani wa kipato cha chini ili waendelee na shughuli zao za ujenzi wa taifa," Dk. Boniface alisema.

Mkurugenzi wa Uendeshaji na Uhusiano wa Kimataifa BMVSS, Satich Mehta, alisema BMVSS itatoa fursa kwa wataalamu wa MOI kupata mafunzo India bila malipo.

"Tutatoa fursa kwa wataalamu wa MOI kuja kujifunza kwa miezi miwili au zaidi, lengo letu ni kuhakikisha ujuzi zaidi unapatikana hapa MOI na wananchi wengi zaidi wananufaike, hasa wale wa kipato cha chini," Mehta alisema.

MOI imekuwa ikianzisha ushirikiano na taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuendelea kuboresha huduma za matibabu inazotoa.

# Mbunge: Wakulima msiuze pamba yenu kwa walanguzi

**Na Mwandishi Maalum**

MBUNGE wa Geita Mjini ambaye pia ni Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, amewashauri wakulima wa pamba wawe wavumilivu badala ya kuuza pamba hiyo kwa walanguzi kwa bei ya chini, huku serikali ikiendelea kuwatafutia soko zuri.

Amesema serikali ilishaahidi kuwa kama pamba hiyo haitanunuliwa kwa bei elekezi ya kilo moja kwa shilingi 800 hadi Agosti mwaka huu, serikali itainunua pamba hiyo ili kuwafidia wakulima hao.

Hatua hiyo imetokana na wafanyabiashara wengi kushindwa kununua kwa bei hiyo kutokana na bei ya soko la pamba duniani kuporoka.

Akizungumza kwenye mkutano uliofanyika katika eneo la Kasamwa mkoani Geita, Kanyasu alisema wafanyabiashara wameshindwa kukopa pesa benki kwa ajili ya kuinunua pamba hiyo kutokana na kukosekana kwa soko la kuiuza.

Kanyasu alisema kufuatia hali hiyo, baadhi ya wakulima wamekuwa wakiiuza pamba hiyo kwa shilingi 500 kwa kilo moja kwa walanguzi hali, inayowadidimiza kiuchumi.

Alitaja mikakati ambayo serikali imeshaichukua ikiwamo kuzungumza na Serikali ya Vietnam ambao tayari wameonyesha nia ya kununua pamba hiyo kwa wakulima. Aidha, Kanyasu aliwaeleza wakulima hao kuwa Waziri wa Kilimo anatambua tatizo hilo na aliahidi kutembelea mkoa huo kwa ajili ya kuzungumza na wakulima hao.

Naye Juma Kaludushi, mkulima wa zao la pamba, alisema wakulima wengi akiwamo na yeye wamekuwa wakiuza pamba hiyo kwa walanguzi kwa bei ya chini kwa hofu kuwa pamba hiyo itaharibikia mikononi mwao.

"Pamba ipo majumbani mwetu muda unakwenda bora tuuze tu kwa walanguzi ili isiharibike kuliko tukapata hasara kabisa," alisema mkulima huyo.

Kwa upande wake, Ester Nalamo, mkulima wa pamba alisema amelazimika kuuza pamba kwa bei ya chini ili aweze kuwalipia ada watoto wake kwa vile hana chanzo kingine cha mapato zaidi ya kuuza pamba.



Mchuuzi akiwa amesheheni bidhaa zake kwenye baiskeli, wakati akisaka wateja katika eneo la Tegeta, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# DED ahimiza wananchi kuacha utegemezi

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

JAMII imetakiwa kuwaandaa watoto kwa kufanya kazi ili baadaye waweze kushiriki katika uzalishaji na kuachana na tabia ya kuwa tegemezi.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, Mshamu Munde, katika mkutano uliowashirikisha wajumbe wa vijiji vipya vya Kata ya Njia Nne na Yavayavya kujadili mradi wa maendeleo uliofadhiliwa kwa miaka 10 na serikali ya Korea Kusini. Katika mkutano huo, wajumbe watano walipatiwa tiketi kwenda Korea Kusini kujifunza miradi ya maendeleo ambayo itakuwa mkombozi katika vijiji hivyo.

Munde alisema mafanikio yanatokana na kujituma kufanya kazi na sio kutegemea wafadhili pekee.

"Inatakiwa wazazi na walezi kuwaelimisha watoto juu ya kuachana na utegemezi. Ukiendekezwa utegemezi utaleta ugonjwa," alisema.

Aliishukuru Korea Kusini kwa kuvisaidia vijiji hivyo ambayo awali vilikuwa na changamoto za kimaendeleo. Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa SAEMAUL nchini, Henry Vlemence, neno SAEMAUL ni neno la Kikorea tafsiri yake ni kijiji kipya.

Alisema kuwa Kata ya Njianne na kijiji chaYavayava ni vijiji ambavyo vilikuwa na changamoto ya kimaendeleo, ambapo kwa sasa changamoto hizo zimeisha baada ya kupatiwa miradi ya maendeleo kwa kipindi cha miaka 10.

"Miradi hiyo ni pamoja na kutengenezewa barabara Doko, kujengewa kisima cha maji, ufugaji wa mbuzi, maduka ya vifaa vya ujenzi pamoja na kuanzishiwa Saccos.

Aliongeza kuwa kutokana na Korea Kusini kuwa na mahusiano mazuri na Tanzania, wametoa mwaliko wa wiki mbili kwa wajumbe watano wa vijiji vipya kwenda nchini humo kujifunza mikakati ya kimaendeleo ili iweze kutumiwa katika vijiji hivyo ili maendeleo yazidi kupatikana.

# Jiko kupunguza matumizi mkaa

**Na Beatrice Philemon**

CHUO cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) cha Moshi mkoani Kilimanjaro kimetengeneza jiko linalotumia gesi ili kupunguza matumizi ya mkaa.

Malengo mengine ni kupunguza uharibifu wa uoto wa asili, kulinda afya za wapishi, kuongeza ufanisi wa upikaji na kutumia gesi ndogo kuliko kuni.

Akizungumza na Nipashe hivi karibuni katika maonyesho ya Sababasa, Mwalimu wa Ufundi, John Nathan, alisema wameamua kutengeneza jiko hili ili kwendana na mpango wa serikali kuondoa vitu vinavyoharibu hali ya hewa na kuharibu uoto wa asili.

Hadi sasa chuo hicho kimetengeneza majiko manne yanayotumia gesi yenye uwezo wa kupika kilo 20-25 za wali, ambao waliupeleka kama sampo katika maonyesho ya mwaka huu, ili kutangaza bidhaa hiyo, na pia kusaidia wananchi kupunguza matumizi ya mkaa, hivyo kuanza kutumia gesi katika shughuli zao za mapishi.

"Tunashukuru Mungu mwitikio wa matumizi ya majiko haya umekuwa mzuri, tumepata oda nyingi kwenye shule na taasisi mbalimbali kutoka mkoa wa Dar es Salaam, Shinyanga ikiwamo wakala wa gesi," alisema.

Alisema majiko haya yametengenezwa na wanafunzi kwa kushirikiana na walimu kupitia programu ya mafunzo.

"Majiko haya yanapunguza gharama ya kupika kwa mfano, unaweza kutumia kilo 1.5 ya gesi kwa ajili ya kupika chakula ambacho ni gharama ndogo," alisema. Pia chuo hicho kina mpango wa kusambaza majiko hayo nchi nzima kwenye shule, magereza, hotelini, hosptalini ili watumie gesi badala ya kuendelea kutumia mkaa ambao unachangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

"Ukizunguka katika maeneo mbalimbali nchini, tatizo linalokabili suala la mazingira, ni matatizo ya mabadiliko ya tabianchi na tatizo mojawapo ni ukataji wa misitu kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo uchomaji mkaa, shughuli za kilimo, upasuaji mbao na utafutaji kuni kwa ajili ya matumizi ya nyumbani."

Matumizi ya mkaa yameongezeka sana na takwimu zinaonyesha kuwa Tanzania inatumia tani milioni 2.5 kwa mwaka na asilimia 60 ya mkaa huo unatumika Dar es Salaam.

# Jafo atoa miezi sita ujenzi wa hospitali kukamilishwa

**Na Augusta Njoji,** CHAMWINO

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amesisitiza Hospitali ya Uhuru wilayani Chamwino kujengwa na kukabidhiwa kwa serikali ndani ya miezi sita kuanzia sasa.

Hospitali hiyo inajengwa na Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi (SUMA JKT). Jafo aliyasema hayo baada ya kutembelea eneo la ujenzi wa hospitali hiyo ikiwa ni mara ya pili kutembelea eneo hilo.

"Juni 16, mwaka huu nilitembelea eneo hili na kukuta pori kukiwa hakuna kitu kinachoendelea, kutokana na hali hiyo nilitoa maagizo ya kuanza mara moja ujenzi na ufanywe na moja ya vikosi vya majeshi na ukamilike ndani ya miezi sita,

"Kwa kweli kwa hatua za awali nimeridhishwa na kazi hii, nimekagua eneo la ekari 40 limesafishwa vizuri, mabati yamezungushwa, eneo la kuhifadhia vifaa limejengwa... hii inaonyesha maandalizi ya awali ya ujenzi huu yameanza, kwa kweli mmenifurahisha, wiki yangu imeanza vizuri," alisema Jafo. Alisema anataka hospitali hiyo ikamilike Januari mwanzoni mwaka 2020 kwa ubora unaotakiwa. Jafo aliwataka watendaji walio chini ya wizara yake kuacha tabia ya kufanya kazi kwa mazoea, na kutaka kutekeleza wajibu wao bila kusukumwa sukumwa.

"Niwaombe wataalamu wangu kuacha kufanya kazi kwa mazoea na tunapotoa maagizo basi wayatekeleze kwa wakati, ni matarajio yetu hadi kufikia Januari, 2020 tutakuwa tumeshakamilisha ujenzi huu." Alieleza kukamilika kwa ujenzi wa hospitali hiyo itakuwa ni kutimiza azma ya Rais John Magufuli katika kutoa huduma bora za afya karibu na wananchi.

Naye msanifu Daneil Mwakasungura kutoka Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ambao ndio washauri na wasimamizi wa mradi huo, alisema mkataba wa awamu ya kwanza ya ujenzi walioingia na SUMA JKT unagharama ya Sh. bilioni 3.

Alisema awamu hii itahusisha ujenzi wa jengo hilo litakalokuwa la ghorofa moja utajumuisha majengo ya wagonjwa wa nje, X-ray, maabara, kliniki ya mama na mtoto, meno na macho. "Tunachosubiri hapa ni SUMA JKT kutupa ratiba ya kazi ambayo ndiyo itatuongoza nini cha kufuata, ila makubaliano yetu ni kuwa ujenzi wa awamu ya kwanza unafanyika kwa mwezi sita na Januari 10 mwakani, jeshi linatakiwa kukabidhiwa kwa serikali.

"Tayari mkandarasi aliyepewa kazi amenza maandalizi ya awali ya ujenzi, ikiwa ni kujenga ofisi, uzio, eneo la mradi limesafishwa kwa kuondoa miti na udongo umeshachukuliwa na kupimwa."

Mwakasungura alisema mchoro unaotumika ni ule wa Tunduma, lakini wataalamu wa wizara ya Tamisemi na Wizara ya Afya na mkoa wamefanya maboresho kwa baadhi ya huduma kwa kuzishusha chini na utawala kuwekwa juu.

Pia Mwakasungura alisema awamu ya pili ya ujenzi wa hospitali hiyo ambao utafanyika baada ya fedha zingine kupanikana utahusu jengo la dharura, chumba cha wagonjwa wanaohitaji uangalizi wa karibu (ICU) na wodi.

Naye msimamizi wa ujenzi wa SUMA JKT kutoka Kanda ya Ziwa, Luten Kanali, Onesmo Njau, alisema wamekabidhiwa kazi Juni 19 mwaka huu, na kwa sasa wameshaanza maandalizi ya awali.

"Niwahakikishie kuwa sisi hatuna shida tutatekeleza mradi huu kwa wakati na kwa ubora, jambo la msingi hapa ni fedha kutolewa kwa wakati."



Mkazi wa Chifutuka wilayani Bahi, Mkoa wa Dodoma, Anna Mathonya (55), akipepeta mbegu za alizeti kwa ajili ya kuzihifadhi kwenye magunia, juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Kasi kisukari yatisha Masasi

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

KASI ya ugonjwa wa kisukari pamoja na shinikizo la damu wilayani Masasi mkoani Mtwara, yameonekana kushika kasi kutokana na watu wengi kuwa na mfumo hasi wa ulaji wa vyakula visivyozingatia mahitaji ya mwili.

Kutokana na hali hiyo, wanapokwenda kupima magonjwa hayo hubainika kuwa na kisukari na shinikizo la damu.

Aidha, kutokana na hali hiyo, jamii wilayani humo imeshauriwa kuwa ni vema ikaachana na mfumo hasi wa ulaji wa vyakula vya aina moja kwa muda mrefu ikiwamo kula wanga kupita kiasi, vinywaji vya sukari nyingi kama vile soda, juisi pamoja na vyakula vyenye mafuta mengi.

Hayo yalibainishwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Mkomaindo wilayani Masasi, Dk. Rashidi Musa, alipokuwa akizungumza na gazeti hili kuhusu magonjwa ya kisukari na shinikizo la damu kwa Wilaya ya Masasi.

Alisema katika Wilaya ya Masasi kumekuwa na kasi ya kubwa ya makundi ya watu wenye umri tofauti tofauti likiwamo kundi la wazee wanaokwenda kupima ugonjwa wa kisukari pamoja na shinikizo la damu wengi wao kubainika kuwa na magonjwa hayo mawili.

Alisema kutokana na hali hiyo kuwa tishio wilayani hapo, uongozi wa hospitali hiyo inatafuta wadau mbalimbali ambapo wataandaa kampeni ya uhamasishaji jamii kwa kuwa na utamaduni wa kupima afya zao mara kwa mara.

Pia watahamasishwa kuzingatia kula vyakula vya asili badala ya vyakula vya kusindika vya viwandani ili kuepesha kupata magonjwa hayo.

Dk. Rashidi alisema moja ya sababu ambayo inapelekea idadi kubwa ya wananchi wilayani humo kukumbwa na ugonjwa wa kisukari ni mfumo wa maisha wanayoishi hasa ulaji wa vyakula na kutokuwa na utamaduni wa kufanya mazoezi ili kuyeyusha kiwango cha sukari kilichozidi mwilini.

Alisema ugonjwa wa kisukari ni hali ambayo hutokea wakati sukari kwenye damu inapokuwa nyingi kupita kiwango cha kawaida kwa muda mrefu.

# Serikali yaziondoa wasiwasi NGO

**Na Mwandishi Wetu**

MSAJILI na Mkurugenzi wa Idara ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Vickness Mayao, amewatoa hofu wadau wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGO) kuwa serikali haina nia mbaya na mashirika hayo ila inataka uwapo utaratibu mzuri wa kuyaratibu.

Aliyasema hayo jijini Dar Es Salaam wakati alipozungumza na waandishi wa habari kuhusiana na zoezi la usajili wa mashirika yasiyo ya kiserikali linaloendelea jijini Dar es Salaam kwa Kanda ya Mashariki. Alisema kuwa utaratibu wa usajili umerahisishwa sana hasa ule wa mashirika yaliyokuwa yamesajiliwa katika sheria nyingine.

Aliongeza kuwa wadau wameridhishwa na huduma zinazotolewa na ofisi yake na kusema wanapata mrejesho mzuri kutoka kwa wadau kupitia fomu za mrejesho wa zoezi hilo.

Mdau kutoka Taasisi ya Solidame Ifakara, Ali Mzava, alitoa rai kwa wadau wa mashirika yasiyo ya kiserikali yaliyosajiliwa chini ya sheria nyingine kujitokeza kwa wingi kujisajili chini ya Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali kwa kuwa usajili umeboreshwa na hakuna tatizo lolote katika zoezi hilo. Naye Mkurugenzi wa Shirika la Tanzania Community Development Assistant, Denis Muchunguzi, alisema wadau wameyapokea vizuri mabadiliko ya Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali Na. 3 ya Mwaka 2019 kwa kuwa wameitikia wito na kujitokeza kwa wingi na hawana tatizo na utekelezaji wa marekebisho ya sheria hiyo.

# Mwenyekiti Wazazi apania kuanzisha miradi

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Wazazi Mkoa wa Arusha, Hezron Mbise, amesema anatarajia kukabidhi mizinga 150 ya nyuki, mashine ya kusaga na mashine ya kufyatulia matofali vitakavyogharimu zaidi ya Sh. milioni 19 kwa jumuiya hiyo ngazi za wilaya mkoani hapa, ili kuziwezesha kujiendesha.

Mbise aliyasema hayo jana wakati akizungumzia mikakati mbalimbali aliyojiwekea katika kuhakikisha jumuiya hiyo inakuwa ya mfano.

Alisema mizinga na mashine atakazotoa ni sehemu ya miradi ambayo itasaidia kuimarisha jumuiya katika wilaya za mkoani Arusha na hatimaye kuondokana na changamoto mbalimbali zinazowakabili.

"Baada ya kuchaguliwa kuwa mwenyekiti nilipata fursa ya kuzungumza na baadhi ya viongozi wa jumuiya katika wilaya. Walinieleza mahitaji yao katika Jumuiya ya Halmashauri ya Arusha DC na nitakabidhi mizinga 50 ya nyuki, Wilaya ya Monduli nikikabidhi mizinga 100 na mashine ya kusaga nitaikabidhi Wilaya ya Ngorongoro, pamoja na mashine ya kufyatulia matofali nitaikabidhi Wilaya ya Longido," alisema Mbise.

Aliongeza kuwa jumuiya nyingi zinakabiliwa na ukosefu wa miradi ya kujiendesha, hivyo kutokana na changamoto hizo atahakikisha jumuiya katika kila wilaya inakuwa na mradi wake kulingana na mahitaji yao.

Mbise alisema katika kufanikisha hilo, atashirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo ili kuhakikisha jumuiya inakuwa ya mfano na ya kuigwa.

Aidha, Mbise aliwataka viongozi mbalimbali kwa pamoja kushirikianakatika kuchangia maendeleo ndani ya jumuiya hiyo na Chama Cha Mapinduzi kwa ujumla.



Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally (kushoto), akizungumza baada ya kukagua ujenzi wa hospitali mpya ya Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara juzi. Katikati ni Mkuu wa Wilaya hiyo, Zephania Chaula na Mganga Mkuu wa Halmashauri ya hiyo, Jesca Lebba. **PICHA: GIFT THADEY**

# Raia Burundi wafungua kesi Afrika Mashariki

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

RAIA 19 wa Burundi wamefungua kesi katika Mahakama ya Afrika Mashariki dhidi ya serikali yao, kupinga vitendo vya unyanyasaji wa haki za binadamu unaoendelea nchini humo.

Wakizungumza jana na waandishi wa habari jijini Arusha baada ykusajiliwa kwa kesi yao, mmoja wa mawakili kutoka Chama cha Wanasheria Afrika (PALU), wanaosimamia kesi hiyo, Evelyn Chijorira kutoka Zimbabwe, alisema wananchi hao wamefungua shauri la kudai haki ya ardhi Julai 12, mwaka huu, lenye namba 16/2019 katika mahakama hiyo.

Alisema mwaka jana serikali ya Burundi iliwashtaki mahakamani nchini mwao wananchi 32 waliokuwa wakipinga Rais wa Burundi kushika madaraka kwa awamu ya tatu na kukiuka katiba yao, lakini cha kushangaza kabla ya kesi hiyo kumalizika, walisikia ardhi yao, nyumba zimetaifishwa na serikali ya Burundi.

"Tumekuja hapa katika Mahakama ya Afrika Mashariki kuwakilisha wananchi 19 wa Burundi kufungua kesi dhidi ya serikali yao, wakilalamikia manyanyaso na kupokonywa ardhi na nyumba zao na serikali. Tunaomba mahakama itusaidie kuhusu Burundi isitusahau," alisema.

Alisema mwaka jana kulitokea vurugu kwa wananchi kupinga Pierre Nkuruzinza kujiongezea muda wa kiuchaguliwa kwa awamu ya tatu, jambo lililosababisha baadhi yao kukamatwa na wengine kuikimbia nchi yao na kukimbilia mafichoni katika nchi mbalimbali.

Hata hivyo wakiwa nje ya nchi yao, walisikia ardhi zao na nyumba vimechukuliwa na serikali ya Burundi, jambo lililowalazimu kufungua kesi katika Mahakama ya Afrika Mashariki, kudai haki zao na kupinga manyanyaso yanayotokea dhidi ya raia na nchi hiyo, ikiwamo kunyimwauhuru wa kujieleza hali ambayo imechangia baadhi yao kuikimbia nchi yao.

"Kutokana na unyanyasaji huo, kati ya wananchi hao 32, wananchi 19 wamekuja kufungua kesi katika mahakama hii ili kudai haki zao za kunyang'anywa ardhi, nyumba na kutopewa uhuru wa kujieleza na kuamua kukimbilia nchi mbalimbali kujificha," alisema wakili huyo.

Wakili mwingine anayewatetea walalamikaji hao, Gustave Niyonzima kutoka Burundi, alisema yeye na mawakili wenzake wanne, ambao wanawatetea wananchi hao 19 wa Burundi wamefungua kesi hiyo wakiwa na matumaini ya kupata haki kwa wananchi hao.

Alisema wanaiomba mahakama hiyo iwasaidie watu wa Burundi wapate haki zao kutokana na kunyang'anywa ardhi yao, nyumba na hata kunyimwa uhuru wa kuzungumza wakati hiyo ni haki ya kila mmoja.

"Tunamatumaini makubwa na hii mahakama kuwa haki itatendeka, ili raia wa Burundi wapate amani na uhuru na hatimaye kumiliki mali zao," alisema Wakili Niyonzima.

## Maofisa maendeleo wahimizwa kutoa elimu kuweka akiba

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MAOFISA Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Arusha, wameagizwa kutoa elimu zaidi kwa kaya maskini, ili kujiwekea akiba na kujikwamua kiuchumi.

Agizo hilo lilitolewa jana jijini hapa na Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Arusha, David Lyamongi, wakati akifungua mafunzo ya siku tano, yanayotolewa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Awamu ya Tatu (TASAF III) kupitia mpango wake wa kunusuru kaya maskini na mradi wa kupunguza umaskini (OPEC III).

Alisema maofisa maendeleo wanapaswa kutoa elimu kwa kaya maskini kila kata, ili kujiwekea akiba ya fedha pale wanapopewa fedha za kaya maskini kwa ajili ya kuibua miradi yao.

Lyamongi alisema mpango huo katika Halmashauri ya Jiji la Arusha, unatekelezwa katika mitaa 70 kati ya 154 yenye walengwa 4,652 na katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha mpango huo unatekelezwa katika vijiji 45 kati ya 71 yenye walengwa 9,071.

"Mpango huu umekuwa mkombozi mkubwa kwani kaya hizi zimemudu gharama za kuendesha familia zao na hata kupeleka watoto shuleni. Lakini inatakiwa maofisa wetu hawa waongeze kutoa elimu kwa kaya hizi ili kujiwekea akiba zitakazowawezesha kukabiliana na dharura," alisema.

Alisema vikundi 20 vya kuweka akiba vimeundwa na kupatiwa vitendea kazi kama masanduku ya kuhifadhia fedha, shajala mbalimbali na vikundi 136 vimejiwekea akiba ya zaidi ya Sh. milioni 74.8.

Naye mwezeshaji wa mafunzo ya mapango wa vikundi vya Tasaf, kuweka na kuwekeza, Julius Katieloh, alisema mafunzo hayo ni m yana lengo la kukuza utamaduni wa kujiwekea akiba kwa kaya maskini, ili kuwezesha kukabiliana na dharura na mahitaji ya msingi.

Washiriki 49 wameshiriki mafunzo hayo na kati yao wawezeshaji 40 kutoka mitaa ya jiji na vijiji vya mkoa huo.



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Yohana Sintoo (kulia), akiwa katika semina ya kuboresha daftari la kudumu la wapigakura pamoja na wakurugenzi wenzake, mkoani humo jana. Waziri Mkuu Kasim Majaliwa anatarajia kuzindua zoezi hilo kitaifa kesho katika viwanja vya Mandela vilivyoko katika Kata ya Bomambuzi, Manispaa ya Moshi. **PICHA: JAMES LANKA**

# Ujio wa treni Kanda ya Kaskazini wafurahiwa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

UJIO wa treni ya mizigo katika mikoa ya Kanda ya Kaskazini (Kilimanjaro, Arusha na Tanga) umepokelewa kwa hisia tofauti, huku idadi kubwa ya wenye viwanda na kampuni za uzalishaji wa bidhaa wakifurahia na wafanyabiashara wachache wa malori ya mizigo, wakidai kuja kwa treni hiyo ni changamoto kwao kiuchumi.

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa anatarajiwa kuzindua safari hizo Julai 20, mwaka huu katika mji wa Moshi, baada ya kusimama kwa zaidi ya miaka 13.

Kwa nyakati tofauti, baadhi ya wafanyabiashara wameeleza kuwa hivi sasa malori ni mengi barabarani na yanachangia kuharibika kwa barabara na kusababisha foleni, hivyo ujio wa treni hiyo ni ukombozi kwa wafanyabiashara wanaozalisha viwandani, mashamba makubwa ya kilimo na usafirishaji wa vifaa vya ujenzi.

"Ni kweli kuja kwa hiyo treni kuna madhara kwa wafanyabiashara wenye malori ambao walitumia fursa vizuri kwa miaka zaidi ya 13 kusafirisha mizigo kwa njia ya barabara, sasa ni wazi kwamba wafanyabiashara wengi wataitumia na hivyo malori kupungua," alisema Steven Ngoti, mmoja wa wafanyabiashara. Mfanyabiashara mwingine, Keddymond Olotu, ameeleza kufurahishwa kwake na ujio wa treni hiyo katika mikoa ya kaskazini akisema, uamuzi huo wa serikali utasaidia kupunguza ajali za barabarani.

"Moja ya vyanzo vya ajali nyingi kwenye barabara kuu hasa Moshi/Arusha ni kuwapo kwa malori ambayo husimama ovyo baada ya kuharibika na baadhi ya madereva huwa hawaweki alama, hivyo kusababisha maafa na uharibifu wa mali.

"Sasa kuja kwa treni hii ya mizigo kutaondoa au kupunguza tatizo hili, ingawa kwetu sisi ni faida kubwa, kwa sababu tunatumia gharama kubwa kusafirisha mizigo kwa njia ya barabara," alisema Olotu.

Jana, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, alisema treni hiyo itaanza kazi baada ya Waziri Mkuu kuizindua ikiwa na mabehewa 20 ya mifuko ya saruji iliyobeba.

Kwa zaidi ya miaka 13 safari za treni hizo zilisimama kufanya kazi katika mikoa ya Tanga na Kilimanjaro kutokana na sababu mbalimbali.

Katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo, kazi ya kuzibua njia ya reli na kufanya matengenezo inaendelea kwa kasi.

Jana usiku kichwa cha treni kilipoonekana kikipita katika baadhi ya maeneo mjini Moshi wananchi mkoani humo walianza kushangilia kwa furaha huku wengine wakipiga kelele za furaha.

# Wahisani waombwa uboreshaji makazi ya wazee

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

HALMASHAURI ya Manispaa ya Moshi, imefungua milango kwa wahisani na taasisi mbalimbali za umma na binafsi, kuunga mkono mkakati wake maalum wa uboreshaji wa makazi ya wazee wasiojiweza ambao wanatunzwa na serikali katika kambi ya Njoro.

Meya wa Manispaa hiyo, Raymond Mboya, alisema kutokana na uchakavu wa majengo, miundombinu na kukosekana kwa baadhi ya huduma muhimu, halmashauri hiyo inataka kukifanyia ukarabati mkubwa ambao utafanana na mchango uliotolewa na wazee hao kwa taifa wakati wa ujana wao.

Mboya aliweka wazi mpango huo jana, baada ya serikali kutumia zaidi ya Sh. milioni 74 kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa kambi ya wazee hao wasiojiweza iliyopo katika Kata ya Mji Mpya.

"Nia yetu ni kuona kwamba kambi hii, inakuwa bora zaidi nchini ambayo itakuwa na zahanati yake ndani ikihudumia wazee, lakini pia inakuwa na majengo ya malazi, bwalo na miundombinu iliyoboreshwa ili kuendana na mahitaji ya sasa," alisema.

Diwani wa Kata ya Mji Mpya, Abuu Shayo, alisema uamuzi wa serikali wa kujenga uzio huo utakuwa umesaidia kumaliza tatizo la kambi hiyo kuvamiwa na vibaka wanaoiba vitu mbalimbali pamoja na misaada inayoelekezwa na wasamaria wema kwa wazee hao.

Kwa miaka zaidi ya 15 serikali haijapeleka bungeni Muswada wa Sera ya Taifa ya Wazee, kutungwa na kuwa sheria.

Mkwamo huo unaelezwa na baadhi ya wanaharakati kwamba ndio kiini kinachochangia kushamiri kwa matukio ya ukatili na kutojumuishwa katika ajenda ya maendeleo.

Akizungumzia changamoto ya kukwama kwa sera ya wazee, ofisa ufuatiliaji na mratibu wa mradi wa kusaidia wasaidizi wa kisheria wa Shirika la Kwieco, Peter Mashingia, alisema serikali inapaswa kutekeleza kwa vitendo dhamira yake ya kusaidia wazee kwa kuhakikisha inaupeleka haraka bungeni muswada huo ili kundi hilo lijiondoe kwenye changamoto za afya na kunufaika na mipango endelevu ya kitaifa.

# Wachangamkia fursa ya upimaji ardhi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WANANCHI zaidi ya 1,400 wanaoishi Kata ya Mji Mpya katika Manispaa ya Moshi, wameanza kuchangamkia fursa ya upimaji wa ardhi na urasimishaji wa makazi, kuepuka mkono wa dola kutwaa ardhi yao kutokana na kukosa umiliki.

Licha ya kuwapo kwa hamasa hiyo, wako wananchi 900 ambao wameshindwa kumudu kulipa gharama ya Sh. 150,000 za utekelezaji wa zoezi hilo kama ilivyotangazwa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, Aprili 17, mwaka huu.

Akielezea maendeleo ya zoezi hilo jana, Diwani wa kata hiyo, Abuu Shayo, alisema mpaka sasa robo tatu ya wananchi wake tayari wameshajitokeza kutaka kupimiwa ardhi yao na kurasimisha makazi, lakini limekuwa likisuasua kutokana na wananchi wengi kutokamilisha malipo ya kupimiwa ardhi. Alikuwa akizungumza katika mkutano wa hadhara wa kuhamasisha zoezi hilo ambao ulifanyikia katika ofisi za kata hiyo.

"Katika zoezi la kupima ardhi, mpaka kufikia sasa, wananchi 900 bado hawajaweza kulipa malipo ya kupimiwa ardhi. Hata hivyo, tumekubaliana kwamba baada ya wiki moja tutaanza kuweka alama za mipaka kwa wananchi waliolipia ili idara husika iwajibike kuwatengenezea hati za umiliki na kulipa kodi stahiki ya serikali," alisema.

Wakati serikali ikitangaza kushusha gharama za upimaji na urasimishaji wa makazi, Waziri Lukuvi alinukuliwa akisema serikali imeshusha gharama hizo baada ya kupokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi wanaodai kutozwa gharama wakati wakitaka kupimiwa ardhi.

Lukuvi alisema: "Kutokana na gharama za urasimishaji ardhi, asilimia 70 ya watu wanaomiliki hawatambuliki na serikali na kusababisha kuikosesha mapato. "Nimefanya hesabu na kubaini kuwa Sh. 150,000 inatosha kupima na kurasimisha ardhi hivyo wanaotaka kumiliki ardhi kisheria wajitokeze kupata huduma hiyo kwa bei rahisi."

Ukurasa 18



Ethiopia yaishangaza dunia kwa kufaulu katika usuluhishi Sudan

**UCHAMBUZI:**

Bavicha: Chadema ilihusika kesi ya wakurugenzi kutosimamia uchaguzi



Ukurasa 19

**Kitaifa**



'Hija' ya Museveni Chato ichagize utengamano EAC

Ukurasa 14


# siasa

JUMATANO JULAI 17, 2019

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU




Zuma apinga kuwa 'mfalme wa ufisadi'

Ukurasa 17

## BAADA YA MIAKA 55

# Pius Msekwa aeleza misumari ya siri iliyoshikilia Muungano-5

MZEE Pius Msekwa (84), ni miongoni mwa wakongwe waliobeba wasifu mkubwa katika kulitumikia taifa, ikiwamo kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Katibu Mtendaji wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), pia mshauri muhimu wa serikali na chama (TANU na CCM) kwa mengi.

Pia, Mzee Msekwa ana sifa nyingine ya kipekee, kuwa mdau anayefahamu fika picha kamili ya dhana ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, ambao mzizi wake kwa hatua, wengi hawaufahamu kwa kina kutokana na umri na si yote yaliyokuwa bayana.

Ili kuliweka hilo wazi kwa kina tangu vuguvugu na kuundwa Muungano huo, ameamua kuandika kitabu alichokizindua siku chache zilizopita, kiitwacho Historia YA Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, kinachoweka undani wa historia kwa hatua. Gazeti hili limeamua kuchapisha maudhui yake kwa hatua, kila siku kama ya leo katika jarida hili la Siasa na leo hii tunaendelea kutokea tulipoishia wiki iliyopita. Endelea na sehemu hii ya tano ya kitabu hicho.

**4.2.3 Sababu za kuwekwa kwa Kipindi cha Mpito**

Sababu kubwa ya kutaka vifungu hivyo vitumike katika kipindi cha mpito tu ilikuwa ni kuwapo kwa hayo matumaini kwamba hadi kufikia wakati wa kutunga Katiba ya kudumu, ile hofu ya Zanzibar kumezwa itakuwa imeondoka, kwa hiyo, itawezekana kuwa na katiba ya serikali moja.

Endelea 16



Spika wa Bunge mstaafu, Pius Msekwa. **PICHA: MTANDAO**

Mzozo Syria wapangua utii wa Uturuki NATO

Ukurasa 20

# 'Hija' ya Museveni Chato ichagize utengamano EAC

Na Mashaka Mgeta

ALIPOFIKA Chato mkoani Geita kwa ziara ya siku moja nchini, Rais Yoweri Kaguta Museveni wa Uganda akasema 'nimekuja kuhiji', bila shaka akimaanisha nia njema ya ujio uliomfikisha kukutana na mwenyeji wake, Rais John Magufuli.

"Wakati Wakristu wakienda Roma, Waislamu wakienda Mecca, nimekuja Tanzania kama sehemu ya hija yangu. Ninafurahi sana kuwa hapa. Nina historia pana inayofungana na nchi hii, ni kama nyumbani kwangu," Rais Museveni amekaririwa akisema kwa Kiswahili sanifu.

Aliyasema hayo Jumamosi iliyopita alipokuwa akizungumza na wakazi wa Chato katika mkoa wa Geita uliopo Kaskazini Magharibi mwa nchi.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Ikulu, Gerson Msigwa, nia ya ziara hiyo ilikuwa kuongeza udugu miongoni mwa viongozi hao, wakiangazia zaidi masuala ya kibiashara hususani katika jamii ya Afrika Mashariki.

Rais Museveni alikuwa kiongozi wa pili kutoka miongoni mwa nchi wanachama wa EAC kumtembelea Rais Magufuli huko Chato, ikiwa ni wiki moja tu baada ya Rais wa Kenya Uhuru Kenyatta kufanya hivyo.

Alipokuwa kwenye ziara yake nchini, Rais Kenyatta alisema dhamira ya ziara hiyo ilikuwa kuimarisha uhusiano wa kijirani baina ya Kenya na Tanzania.

Rais Kenyatta akasema kuna umuhimu wa viongozi kuwajibika ili kuondosha vikwazo vinavyozuia biashara, kuruhusu mzunguko huru wa watu na kuzidi kuimarisha uhusiano na kusisitiza umuhimu wa mataifa ya Afrika Mashariki kushikana kama kitu kimoja.

Naye Rais Museveni alipowasili Chato, akarejea kauli yake ya mara kwa mara kuhusu historia ya Tanzania kwa ustawi wa Uganda, na kusema sababu za ujio wake ndizo zinazomfanya aione ziara yake kama hija kwenye ardhi ya Tanzania.

Tukio kubwa la kihistoria kwa Tanzania na Uganda ni vita vilivyopiganwa kati ya mataifa hayo mwaka 1979 na majeshi shupavu yaliyokuwa chini ya Amiri Jeshi Mkuu, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere yakuangamiza uliokuwa utawala wa Idi Amin nchini Uganda.

Wakati fulani, Rais Museveni aliwahi kusoma hapa nchini, lakini pia kuratibu mikakati ya kuingia kwenye utawala wa nchi hiyo kupitia FRONASA iliyobadilika baadaye kuwa, NRM/A ikipigana `vita ya ukombozi' kati ya miaka ya 1981 na 1985.

Wakati huo, Tanzania ilikuwa chini ya utawala wa Mwalimu Julius ambao Rais Museveni anatambua kwamba ulishiriki kikamilifu kutumia hekima na busara katika kuzisaidia nchi nyingine za Afrika kuwa huru.



Rais John Magufuli (kushoto), akiwa na mwenyeji wake Yoweri Museveni. **PICHA: MTANDAO**

**MAENDELEO**

Ajenda kubwa katika ushirikiano wa nchi kama Tanzania na Uganda, ama jumuiya za kikanda kama ilivyo Afrika Mashariki (EAC) ni maendeleo na ustawi wa watu.

Na kwa mukhtadha huo, Rais Museveni anahimiza wananchi kushiriki na kuunga mkono jitihada hizo kama inavyofanyika pia nchini kwake.

Rais Museveni anasema utajirisho na ajira ni miongoni nyanja zinazokabiliwa na changamoto nyingi, lakini katika jambo lenye maana zaidi ni mazingira mazuri ya kuzitatua changamoto hizo kupitia ushirikiano kati ya mataifa kama ilivyo kwa Tanzania na Uganda.

Anasema maendeleo ni miundombinu kwa ajili ya watu wote lakini utajirisho unagusa ngazi ya kaya na kusema, "kama Rais Magufuli anatengeneza barabara, hauwezi kuja ukalala hapo kuyafurahia maendeleo hayo..."

Badala yake, Rais Museveni anawahimiza watu kushiriki huduma za uzalishaji kama ufugaji unaoongeza utajiri kwa ngazi ya kaya.

Naye Rais Magufuli anatambua umuhimu wa ujio wa Rais Museveni aliyetokea Angola, na kusema ni heshima kubwa kuzipita takribani nchi tatu na kuwasili hapa nchini.

Kama ilivyokuwa kwa Rais Museveni, Rais Magufuli pia anakumbushia namna utawala wa Mwalimu Nyerere ulivyofanikisha kumuondoa madarakani aliyekuwa Rais dikteta wa Uganda, Idi Amin Dada.

Rais Magufuli anasema uhusiano mwema kati ya Tanzania na Uganda unapaswa kuendelezwa, huku akishukuru namna serikali ya Uganda ilivyofanikisha matibabu ya Mama Maria Nyerere, mjane wa Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere.

Mama Maria alikuwa nchini Uganda hivi karibuni akishiriki hija na misa ya kumuombea Mwalimu Nyerere aliye katika mchakato wa Kanisa Katoliki ili atangazwe kuwa Mtakatifu. Mwalimu Nyerere ameshatangazwa kuwa Mtumishi wa Mungu.

**UCHUMI**

Marais hao walizungumzia pia ushirikiano wa kiuchumi kati ya nchi hizo ikiwamo kulitumia ziwa Viktoria kuchagiza kasi ya biashara kwa nchi wanachama wa EAC na matumizi ya uwanja wa ndege wa Chato na reli ya kisasa (SGR).

Rais Magufuli anasema ushirikiano wa Tanzania na Uganda, pamoja na Kenya 'zinazounganishwa' na Ziwa Viktoria, zimepanga kutengeneza meli kubwa zitakazotumika kwa usafiri na usafirishaji mizigo kupitia kwenye ziwa hilo.

> "Tukio kubwa la kihistoria kwa Tanzania na Uganda ni vita vilivyopiganwa kati ya mataifa hayo mwaka 1979 na majeshi shupavu yaliyokuwa chini ya Amiri Jeshi Mkuu, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere yakuangamiza uliokuwa utawala wa Idi Amin nchini Uganda.

**UMUHIMU WA ZIARA**

Mazungumzo ya Rais Museveni na Rais Magufuli yakafuatiwa na taarifa za kukutana kwake (Museveni) na hasimu wake wa kidiplomasia katika ukanda wa EAC, Rais Paul Kagame huko Luanda, Angola.

Viongozi hao wawili wamekuwa kwenye mgogoro wa kidiplomasia kwa miaka kadhaa kiasi cha kutishia utekelezaji wa mipango, mikakati, miradi na malengo ya EAC.

Hivi majuzi Rais Kagame alielezea kuwa chimbuko la mgogoro baina ya nchi yake na Uganda kwamba lilianza miaka 20 iliyopita wakati majirani zake wa Uganda walipotaka kuangusha utawala wake.

Akasema mgogoro huo ulishika kasi katika miaka ya hivi karibuni kutokana na serikali ya Uganda kuunga mkono kundi la RNC linalopinga Rwanda na ambalo linadaiwa kutumiwa na Uganda kuwanyanyasa raia wa Rwanda wanaotembelea au wanaoishi nchini humo (Uganda).

Lakini, Uganda nayo imekuwa ikiishutumu Rwanda kwamba inawatuma majasusi kwenye ardhi yake, shutuma ambazo Rwanda inakanusha.

Wachambuzi wa masuala ya kisiasa wanaielezea ziara ya Rais Museveni kama sehemu ya kuhuisha umuhimu wa EAC na kuhakikisha vikwazo kama migogoro iliyopo vinapatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Kenedy Benedict, mtaalama wa usuluhishi wa migogoro anasema, hatua iliyofikiwa na marais Kenyatta na Museveni kumtembelea Rais Magufuli, ikiwa ni katikati ya mizozo ya kiuchumi iliyopo kati ya mataifa hayo, inapaswa kufanyika kwa nchi nyingine za EAC.

"Tunajua kuna wakati kulikuwa na mzozo kati ya Kenya na Tanzania, na wakati fulani ikaonekana kama Tanzania inachukua fursa ya kiuchumi za Kenya kama ilivyokuwa kwenye bomba la mafuta kutoka Hoima, lakini kupitia mazungumzo ya marais, changamoto zilizopo zinapatiwa ufumbuzi wa kina," anasema.

Naye Dafroza Mathias, mtaalamu wa masuala ya diplomasia anasema kama ziara zilizofanywa na marais Kenyatta na Museveni zitafanyika kwa nchi zilizo katika mzozo wa kidiplomasia hususani Rwanda na Burundi dhidi ya Uganda, kutakuwa na mafanikio yatakayochochea kuiimarisha EAC.

***Makala haya yameandikwa kwa msaada wa vyanzo mbalimbali. Mwandishi wake anapatikana kupitia simu 0754691540 ama barua pepe:mgeta2000@yahoo.com.***

UCHAMBUZI

# Wananchi waitumie vyema fursa hii iliyotolewa na NEC

**Na Reubeni Lumbagala**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi hapa nchini (NEC) ipo kazini kuhakikisha kila mwananchi mwenye sifa za kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura anapata haki ya kujiandikisha ili baadaye ashiriki siku ya uchaguzi kuwachagua viongozi bora kwa maendeleo.

Mkoa wa Kilimanjaro umepata heshima ya kuwa mkoa wa kwanza nchini ambapo kesho Julai 18, kutafanyika uzinduzi wa shughuli ya uandikishaji wananchi katika Daftari la Kudumu la Wapigakura.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi wa shughuli hiyo inayotarajiwa kufanyika katika uwanja wa Mandela, Manispaa ya Moshi.

Kazi hiyo ya kuboresha Daftari la Kudumu la Wapigakura itaendelea hadi Julai 24, ili kutoa nafasi kwa wananchi kujiandikisha na hivyo kuwawezesha kushiriki katika uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu na uchaguzi mkuu Oktoba mwakani.

Hii ni nafasi muhimu kwa wananchi kuchagua viongozi wanaowataka ambao watashirikiana nao katika juhudi za kuleta maendeleo nchini.

Kimsingi, wananchi wanapaswa kuthamini fursa hiyo ya kutumia haki yao ya kuchagua viongozi watakaowaongoza kwa miaka mitano ijayo.

Zoezi la kuwachagua viongozi hao linaanzia kwenye kujiandikisha ili kuweza kupiga kura siku ya uchaguzi.

Hivyo, kujiandikisha ndiyo mwanzo wa kupata viongozi bora. NEC inatumia vyombo mbalimbali vya habari kuwahamasisha wananchi kujiandikisha katika daftari hilo la kudumu la wapigakura.

Hivyo basi, ni vyema wananchi kuitumia elimu kwa umma inayotolewa na NEC pamoja na wasanii mbalimbali ili kuona umuhimu wa kujiandikisha.

Wananchi wa Kilimanjaro wazitumie vizuri siku saba za kujiandikisha ili muda ukifika wachague viongozi wao.

Kila mwananchi anayepata elimu ya kujiandikisha katika daftari hilo ahakikishe anaitumia elimu atakayoipata katika kuwahamasisha wengine kwenda kwenye vituo vilivyoainishwa na NEC kujiandikisha.

Hatua hiyo itawezesha kupatikana viongozi bora wa serikali za mitaa na mwakani madiwani, wabunge na Rais bora kwa ustawi wa maendeleo.

Pamoja na wananachi kuwa na shughuli nyingi za uzalishaji mali, wanapaswa kuhakikisha hawaiachi fursa hii adhimu ya kujiandikisha kupigakura.

Wananchi wahakikishe kuwa wanatenga muda wa kazi na muda wa kwenda katika vituo vya kujiandikisha.

Upo utamaduni mbaya miongoni mwa wananchi ambao inapotokea fursa kama hii huzembea kwenda kujiandikisha katika siku za mwanzoni na hatimaye kusubiria siku ya mwisho ndipo hujitokeza.

Ni vyema wananchi wa Kilimanjaro kuzitumia vizuri siku hizo saba kujiandikisha ipasavyo pasipo kusubiri huruma za tume ya uchaguzi kuongeza siku.

**UANDIKISHAJI WANANCHI KATIKA MIKOA MINGINE**

Baada ya kumalizika zoezi la uandikishaji wananchi katika daftari la kudumu la wapigakura mkoani Kilimanjaro, zoezi hilo litaendelea katika mikoa mingine ya Tanzania.

Hivyo basi, wananchi wa mikoa mingine wajiandae kisaikolojia katika kuhakikisha muda utakapofika katika mikoa, wilaya na kata zao, wajitokeze kwa wingi kujiandikisha.

Wananchi kubaki nyumbani bila kujiandikisha, hakutawasaidia kutatua kero zao zinazowasibu.

Kura zao zina maana kubwa katika kuchangia kutatua kero zao kupitia kupata viongozi bora watakaokuwa chachu ya kutatua kero za wananchi.

Aidha, Tume ya Uchaguzi ina wajibu si tu kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura, lakini pia kuhusu nguvu ya kura zao katika maendeleo.

Baadhi ya wananchi hujiandikisha ili kupata vitambulisho kwa matumizi yao binafsi na si kwa kipaumbele cha kushiriki kuwachagua viongozi katika uchaguzi. Tathmini ya chaguzi nyingi hapa nchini zinaonyesha uwiano usioendana kati ya wanaojiandikisha katika daftari la kudumu la wapiga kura na wanaojitokeza siku ya uchaguzi kupiga kura.

inayotolewa na NEC kuhusiana na kujiandikisha, isisitize pia agenda ya nguvu ya kura za wananchi katika kupata viongozi bora na makini.



Wananchi wakijipanga tayari kuboresha taarifa zao kwenye Daftari la Kudumu la Wapigakura. **PICHA: MTANDAO**

> Kila mwananchi anayepata elimu ya kujiandikisha katika daftari hilo ahakikishe anaitumia elimu atakayoipata katika kuwahamasisha wengine kwenda kwenye vituo vilivyoainishwa na NEC kujiandikisha.

Wananchi waelimishwe kuwa wasiishie tu kujiandikisha, lakini pia washiriki kupiga kura siku ya uchaguzi. Muhimu ni NEC kuwekeza katika elimu kwa umma ili kuwaelimisha zaidi wananchi kuhusu umuhimu wa ushiriki wao katika uchaguzi.

Kwa mujibu wa katiba yetu, uchaguzi wa serikali za mitaa na ule uchaguzi mkuu unafanyika kila baada ya miaka mitano.

Hii inaonyesha kuwa uchaguzi si tukio la kila siku, ni tukio linalojitokeza mara moja ndani ya miaka mitano, achilia mbali chaguzi ndogo za kujaza nafasi zilizo wazi.

Kutokana na upekee wake, wananchi watumie fursa hii katika kujiandikisha, kuwasikiliza wagombea wa nafasi mbalimbali za uongozi na mwishoni kuwachagua viongozi bora wanaokidhi matarajio yao.

Jambo jingine la msingi ni wananchi kutunza shahada zao za kupigia kura ili wazitumie siku ya tukio lenyewe. Kadi yako, kura yako, kajiandikishe na kuboreshe taarifa zako.

Mimi nipo tayari kujiandikisha na kupiga kura, Wewe je? Tafakari.

**Mwandishi ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa Jijini Dodoma.**
**Maoni: (+255) 764 666349.**

UCHAMBUZI

BAADA YA MIAKA 55

# Pius Msekwa aeleza misumari ya siri iliyoshikilia Muungano-5

**Inatoka Uk. 13**

Tumekwishakuona kwamba, kipindi hicho cha mpito baadaye kiliongezwa kwa sheria ya Bunge iliyotungwa mwezi Machi 1965, ambayo iliondoa kikomo cha mwaka mmoja. Madhumuni ya kuondoa kikomo hicho yalikuwa ni kujipa muda zaidi ili kuwezesha Muungano kutengamaa zaidi, na faida zake kuonekana wazi zaidi; hali ambayo ilitegemewa kuwa ingesaidia kuondoa hofu hiyo ya Zanzibar kumezwa, na kwahiyo, kutuwezesha kurejea kwenye muundo wa serikali moja.

Lakini, hata hivyo, hatimaye Katiba ya kudumu ilitungwa mwaka 1977, (yaani, miaka 13 baadaye), kwa kuwa hofu hiyo ilikuwa bado haijaondoka, ilibidi Katiba ya Kudumu iendeleze muundo huu wa serikali mbili.

(a)Kuzaliwa kwa Chama Cha Mapinduzi

Hatua ya kuzaliwa kwa Chama Cha Mapinduzi mwaka 1977 pia, ilileta matumaini mapya kwa upande wa Mwalimu Nyerere, ya kwamba chama hiki kipya kingeweza kufanikisha upatikanaji wa muundo wa serikali moja. Matumaini haya mapya yalitokana na kutambua kwamba, Chama hiki kipya kilikuwa na madaraka kamili ya kufanya maamuzi makubwa yanayohusu pande zote mbili za Muungano. Hii inathibitishwa na kitabu chake kiitwacho "Uongozi wetu na Hatima ya Tanzania" (Zimbabwe Publishing House). Mwalimu aliandika hivi:

"Muundo wa Muungano ni suala la sera, siyo amri ya Mungu. Vyama vya siasa mbalimbali vinaweza kuwa na maoni mbalimbali kuhusu muundo unaofaa wa Muungano…muundo wa serikali mbili ni Sera ya TANU na ASP, na kwa sasa CCM. Lakini, Chama Cha Mapinduzi kikipenda kinaweza kubadili sera hiyo ya muundo wa serikali mbili…kinaweza kufanya hivyo kwa kuhisi kwamba, hivyo ndivyo wananchi wengi watakavyo, lakini pia kinaweza kufanya hivyo kwa sababu ya kuamini chenyewe kuwa inafaa kufanya hivyo, hata kama wananchi wengi hawakudai mabadiliko … Chama Cha Mapinduzi kitakapobadili sera yake ya muundo wa Muungano wa serikali mbili, sera yake mpya itakuwa ni muundo wa Muungano wa serikali moja."

**4.3 Mwisho wa matumaini ya kupata serikali moja**

Hata hivyo, matumaini hayo vilevile hayakufanikiwa kutimizwa, kwani siyo tu kwamba hofu ya Zanzibar kumezwa na Tanganyika ilikuwa bado ipo, lakini, pia, ilikuwa imeongezeka na kupata nguvu zaidi kuliko ilivyokuwa hapo awali. Ndiyo maana Utawala wa Rais Aboud Jumbe ulianzisha madai ya muundo wa serikali tatu. Ripoti ya Tume ya Warioba inaeleza kwamba, kumekuwapo na malalamiko kutoka Zanzibar yanayodai kwamba, "Tanganyika imevaa koti la Muungano." Madai hayo yalianza kujitokeza wakati huo, yakifuatiwa na madai mengine ya kudai "usawa wa nchi zetu mbili zilizoungana."

Bila shaka ni katika jitihada za kutafuta huo usawa wa nchi mbili zilizoungana, ndipo Rais Aboud Jumbe alipoibua mkakati wa kutengeneza Katiba mpya ya serikali tatu mnamo mwaka 1983. Lengo lake lilikuwa ni kuirejesha Serikali ya Tanganyika ambayo ilidhaniwa kuwa imejificha kwenye koti la Muungano. Juhudi hizo za Rais Aboud Jumbe zitaelezwa baadaye. Huo ndio ulikuwa mwisho kabisa wa matumaini yaliyokuwapo ya kupata muundo wa serikali moja. Badala yake, sasa zikaanza juhudi kubwa za kudai muundo wa serikali tatu. Tutarejea kuzungumzia juhudi hizo katika Sura ya Sita. Ushahidi unathibitisha kuwa matumaini ya kuwa na muundo wa serikali moja hayapo tena, upo katika takwimu za Tume ya Warioba iliyokusanya maoni ya wananchi kuhusu muundo wa Muungano, ambapo inaonesha wazi kwamba, kwa upande wa Tanzania Bara, katika jumla ya maoni 684,303 yaliyopokelewa, ni maoni 3,564, au asilimia 0.5 tu, ndiyo yaliyopendekeza muundo wa serikali moja. Na kwa upande wa Zanzibar, katika jumla ya maoni 49,671 yaliyopokelewa, ni maoni 25, au asilimia 0.05 tu, ndiyo yaliyopendekeza muundo wa serikali moja!



Mmoja wa makomandoo wa Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania (JWTZ), akiwa katika moja ya maonyesho ya kumbukumbu ya Siku ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar. **PICHA: MTANDAO**

"Muundo wa Muungano ni suala la sera, siyo amri ya Mungu. Vyama vya siasa mbalimbali vinaweza kuwa na maoni mbalimbali kuhusu muundo unaofaa wa Muungano…muundo wa serikali mbili ni Sera ya TANU na ASP, na kwa sasa CCM….

**SURA YA 5 CHANGAMOTO ZA MUUNGANO**

Katika nyakati tofauti za uhai wake, Muungano wetu umekumbwa na changamoto nyingi za aina mbalimbali, kuanzia changamoto za kidiplomasia; zikifuatiwa na changamoto za kifedha; changamoto za hujuma kutoka kwa maadui wa Muungano; na changamoto kubwa zaidi ya ubishi usiokwisha juu ya muundo uliopo wa serikali mbili, ambao unaendelea hadi sasa.

**5.1 Changamoto za kidiplomasia**

**5.1.1 Kuathirika kwa Uhusiano na Ujerumani**

Kufuatia kuundwa kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, mwezi Januari 1964, nchi ya Ujerumani Mashariki (ilivyokuwapo wakati huo), ilifungua ubalozi wake Zanzibar. Kabla ya Muungano, Ujerumani Magharibi (kama ilivyokuwa wakati huo) ilikuwa na ubalozi wake nchini Tanganyika. Katika kipindi hicho kulikuwa na uhasama mkubwa baina ya Ujerumani Mashariki na Ujerumani Magharibi, kiasi kwamba, ilikuwa haiwezekani kwa nchi hizo mbili kuwa na Mabalozi wao katika nchi yoyote ya kigeni. Kutokana na Muungano wa Tanganyika na Zanzibar uliozifanya kuwa ni nchi moja, nchi hizo zote mbili za Ujerumani zikajikuta zina Balozi zao nchini Tanzania, jambo ambalo kumbe lilikuwa ni mwiko kwao. Ujerumani Magharibi ikajaribu kumshinikiza Rais Nyerere afunge ubalozi wa Ujerumani Mashariki uliokuwa Zanzibar. Rais Nyerere alikataa shinikizo hilo. Matokeo yake yakawa ni kwamba, kwa hasira zake, Ujerumani Magharibi ikasimamisha utoaji wa msaada waliokuwa wanaendelea kuutoa kwa Tanganyika kwa ajili ya kuunda Kikosi cha Anga cha Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Mashinikizo hayo yalimuudhi sana Rais Nyerere. Akaitaka Ujerumani Magharibi iondoe mara moja misaada yake mingine yote iliyokuwa ikiitoa kwa Tanzania, na siyo kuondoa msaada kwa jeshi peke yake. Tukio hilo liliathiri mahusiano baina ya Tanzania na Ujerumani Magharibi.



Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere (kushoto), akiwa na Mzee Abeid Aman Karume.

**5.1.2 Kuathirika kwa Uhusiano na Marekani**

Baadaye tena mnamo mwezi Novemba 1964, Waziri wa Mambo ya Nje Oscar Kambona alitangaza kugunduliwa kwa njama aliyodai kuwa ilikuwa inasukwa na Marekani kwa lengo la kuipindua Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kambona alidai kwamba, sababu ya Marekani ya kutaka kufanya hivyo ni kutokana na hofu yao kwamba, kwa kupitia Zanzibar, nchi za kikomunisti zilikuwa zinajiandaa kuongeza nguvu zake katika eneo lote la Afrika Mashariki na Rais Nyerere alikuwa anaelekea kuwanyamazia!

Serikali ya Marekani ilikanusha madai hayo, lakini, tukio hilo liliathiri mahusiano ya nchi yetu na Marekani.

**5.2 Changamoto za ndani (Kero za Muungano)**

Changamoto za ndani ya nchi zinajulikana zaidi kwa jina la "kero za Muungano," ambazo zimesababisha malalamiko mengi kutoka pande zote mbili za Muungano, hali ambayo imeweka doa katika Muungano wetu. Zifuatazo ni baadhi ya kero hizo. Tayari nimekwishakuelezea ile changamoto ya ubishi uliojitokeza kwamba, Zanzibar haijawahi kuridhia Mkataba wa Makubaliano ya Muungano. Hii ilikuwa ni changamoto kubwa, kwa sababu, kama nilivyokwishaeleza, kutoridhia Mkataba huo, ni jambo linalobatilisha kuwapo kwa Muungano wenyewe.

Ni jambo la kushukuru sana kwamba, hatukufika kwenye hatua hiyo. Changamoto nyingine zilizowahi kujitokeza, ni pamoja na hizi zifuatazo:

**5.2.1 Zanzibar kukosa uhusiano wa kiuchumi na nchi za nje**

Malalamiko yanayoitwa 'kero za Muungano' yamekuwa yakitolewa na pande zote mbili za Muungano. Kubwa zaidi, kwa upande wa Zanzibar, ni madai kwamba, kuwapo kwake katika Muungano huu kumeikosesha Zanzibar fursa ya kuwa na mahusiano ya moja kwa moja na nchi za nje katika masuala ya kiuchumi; kama vile fursa ya kupata misaada na mikopo kutoka nchi za nje, au kutoka katika mashirika ya kimataifa. Lalamilo hili lilijitokeza kwa nguvu sana wakati Zanzibar ilipozuiwa kujiunga na chombo kinachoitwa Organization of Islamic Conference (OIC). Maelezo yake ni kama ifuatavyo:

Mnamo mwezi Desemba mwaka 1992, vyombo vya habari vilitangaza kwamba, Zanzibar ilikuwa imejiunga na chombo hicho cha kimataifa, kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Tatizo la kikatiba lilitokana na kwamba, Zanzibar, ikiwa ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, haikuwa na sifa ya kujiunga na chombo hicho, ambacho uanachama wake uko wazi kwa nchi zile tu ambazo zinawakilishwa katika Umoja wa Mataifa (Sovereign States). Ndiyo sababu Zanzibar haikuwa na sifa ya kujiunga na OIC.

Kwa upande wake, Serikali ya Zanzibar haikuridhishwa na hoja hiyo, ikidai kupitia kwa Waziri Kiongozi wa Serikali hiyo, Dk. Omar Ali Juma, kwamba, Zanzibar ni nchi kamili ambayo ina Rais wake, Serikali yake, Bunge lake na pia, Mahakama zake. Haioni kwa nini isiwe na sifa za kujiunga na OIC. Kutokana na msimamo wake huo, ilikuwa ni kazi ngumu kuishawishi Serikali ya Zanzibar ijiondoe katika uwanachama wa chombo hicho. Lakini, hatimaye Serikali ya Zanzibar ilikubali kujiondoa; kwa mategemeo kwamba, Serikali ya Muungano ingejiunga na chombo hicho. Lakini, Serikali ya Muungano haikupeleka maombi ya kujiunga na OIC.

**ITAENDELEA WIKI IJAYO…**



Rais wa zamani wa Afrika Kusini, Jacob Zuma. **PICHA: MTANDAO**

## Zuma apinga kuwa 'mfalme wa ufisadi'

ALIYEKUWA Rais wa Afrika Kusini, Jacob Zuma, ameliambia jopo la mahakama linalochunguza madai ya rushwa dhidi yake kuwa "kuna njama" inayolenga kumwangamiza kisiasa.

Alikuwa anafika mbele ya jopo hilo kwa mara ya kwanza huku wafuasi wake wakimshangilia alipoingia katika jengo hilo.

Zuma (77), alilazimishwa kujiuzulu wadhifa wa urais Februari mwaka 2018.

Wakati akijitetea, Zuma amesema kuwa madai hayo ya ufisadi ni njama ambayo imekuweko kwa muda mrefu ili kumwaharibia jina, mpango ambao umetekelezwa na wasimamizi wa chama cha African National Congress (ANC) ili kumwondoa kwenye siasa za Afrika Kusini.

Alipoulizwa ni kwanini anatoa madai hayo, anasema kuwa wenye kumpiga vita walidhani alikuwa na habari dhidi ya watu fulani, ambazo zingewazuia kutwaa nafasi za juu katika chama hicho.

Nafasi yake ilichukuliwa na aliyekuwa makamu wake wakati huo Cyril Ramaphosa, ambaye aliahidi kukabiliana vikali na suala la rushwa nchini Afrika Kusini.

Ramaphosa ambaye kwa sasa ni rais aliueleza utawala wa miaka tisa ya Zuma kama "kupoteza muda."

Mashtaka dhidi ya Zuma yanaangazia uhusiano wake na familia inayokabiliwa na utata ya Gupta, ambayo inatuhumiwa kutumia vibaya ukaribu wao na Rais kuingilia uteuzi wa mawaziri na kujipatia zabuni za serikali kwa njia za kifisadi.

Pia anakabiliwa na tuhuma ya kupokea rushwa kutoka kwa kampuni ya Bosasa, ambayo inamilikiwa na familia ya Watson.

Zuma amekanusha madai hayo yote.

" Nimeonewa na kutuhumiwa kuwa mfalme wa watu mafisadi… watu wamenibandika majina yote na sijawahi kujibizana nao kuhusiana na suala hilo," Zuma aliliambia jopo hilo linaloongozwa na Jaji Ray Zondo.

**'HUJUMA' DHIDI YAKE**

Alielezea kwa kina na kwa hasira kile alichotaja kuwa miongo kadhaa ya hujuma dhidi yake.

Alidai kuwa mataifa ya Uingereza na Marekani, bado ni washirika wa sehemu ya mpango wa kumkosoa japo amejaribu kuleta mabadiliko ya kisiasa na kiuchumi nchini Afrika Kusini.

Zuma alidai kuwa waziri wa zamani wa serikali Ngoako Ramatlhodi, aliyetoa ushahidi wa kumdalilisha ni sehemu ya njama hizo.

Zuma alisema, maajenti wengine wa kigeni walijaribu kumtilia sumu, bila kuwataja majina.

**ZUMA NA FAMILIA YA GUPTA**

Akiizungumzia familia ya Gupta, Zuma alisema aliiona familia hiyo ya wazaliwa wa Kihindi kuwa "marafiki zake."

"Sikufanya jambo lolote kinyume cha sheria nao…walikuwa marafiki zangu tu, sawa na jinsi walivyokuwa marafiki wa watu wengine," Zuma alisema na kuongeza kwamba walikuwa marafiki wa rais wa kwanza wa nchi hiyo Nelson Mandela na Thabo Mbeki.

Alipinga madai kwamba aliruhusu familia hiyo kuingilia kati uongozi kwa "kuteka nyara" na kuipiga mnada nchi hiyo.

Kitu kimoja kinachojitokeza katika ushahidi uliyowasilishwa na Zuma kufikia sasa ni kuwa ikiwa ataporomoka, hatakubali kwenda peke yake.

Ametoa taswira ya picha anayodai kuwa kuna njama ambayo imekuwa ikipangwa dhidi yake kwa zaidi ya miongo miwili.

"Nimechokozwa," alisema, huku akitishia kutaja majina ya wale anaodai kuwa majasusi waliohujumu harakati za uhuru wa watu weusi nchini Afrika Kusini na ambao anasema bado wanaendelea kumhujumu.

Wakati mmoja Zuma alikuwa kiongozi wa upelelezi wa ANC, vuguvugu la zamani la kupigania uhuru ambalo limekuwa madarakani tangu utawala wa weupe ulipoondolewa madarakani mwaka 1994.

Akiamua kufichua siri kama alivyotishia, huenda akatikisa siasa za Afrika Kusini, hali ambayo itasababisha mpasuko mkubwa ndani ya chama cha ANC.

Lakini hali itakapotulia, bila shaka watu wa Afrika Kusini wanataka kujua ikiwa alihujumu kiapo cha ofisi yake alipoingia madarakani mwaka 2004 kwa kujihusisha na suala la ulaji rushwa kwa kiwango kikubwa. **BBC**

# Ethiopia yaishangaza dunia kwa kufaulu katika usuluhishi Sudan

**Na Anil Kija**

ETHIOPIA imekuwa nchi ya kwanza Afrika kusimamia usuluhishi katika mzozo nchi jirani na kufaulu kufikia makubaliano yanayoelekea kuanza kutekelezwa na Baraza la Kijeshi la Mpito linalotawala nchini humo kwa sasa.

Halikuwa jambo la kawaida kwani ni nadra kwa juhudi za msuluhishi kufaulu katika mizozo barani Afrika, na hata inapotokea kufaulu, siyo nchi ya jirani inayoingia na kuziita pande mbili zikae mezani, na hata kupokea maelekezo au kuhitaji madai yao kuthibitishwa na msuluhishi.

Ndiyo maana sauti za tahadhari zilikuwa zinasikika zaidi wakati Waziri Mkuu wa Ethiopia Abiy Ahmed alipofika nchini Sudan kuanza shughuli hiyo.

Waziri Mkuu Abiy alianza juhudi hizo siku moja baada ya Umoja wa Afrika (AU) kusimamisha uanachama wa Sudan kutokana na utawala wa kijeshi kutumia risasi dhidi ya waandamanaji waliokuwa wanaendelea na madai kuwa utawala wa mpito uongozwe na raia.

Abiy ni kiongozi wa mageuzi ya dhati nchini Ethiopia ambayo yameondoa harufu za udikteta katika uendeshaji wa nchi hiyo, na kwa maana hiyo ni mtu anayekubalika bila kipingamizi chochote na viongozi wa waandamanaji nchini Sudan, na haaminiwi na viongozi wa Baraza la Kijeshi.

Jambo la kushangaza ni kuwa majenerali wenye rekodi ya 'mti mkavu' walikwama, wakamsikiliza.

Hilo likawa ni somo la kwanza kwa wachambuzi wa siasa na wataalamu wa masuala ya vita na amani barani Afrika na kwingineko, waliokuwa bado wanaweka sawa nadharia zao kuwa nini hasa kinahitajika katika usuluhishi ili uweze kufaulu.

Moja ya vihadharisho mazoea ni kuwa msuluhishi anatakiwa asiwe kabisa anaunga mkono au kufungamana na upande wowote katika mzozo husika, nadharia ambayo ilikwama kujidhihirisha kwani hakuna ubishi wowote au shaka Abiy yuko upande gani katika mzozo huo.

Halikuwa suala la diplomasia ila kuukubali ukweli kwa upande wa majenerali 'mti mkavu;' walikuwa tayari kuiingiza Sudan katika umwagaji damu.

Abiy alipata sifa kubwa kimataifa alipoondoa uadui wa miaka mingi kati ya Ethiopia na Eritrea, nchi ambayo ilipambana kwa miaka 29 (1962-1991) kujiondoa Ethiopia, baada ya Mfalme Haile Selassie kuondoa uhuru wa kujiamulia wa eneo hilo akalifanya liwe jimbo la kawaida.

Kwa hali hiyo Abiy alikuwa ni mtu wa kuaminiwa moja kwa moja na AU na Umoja wa Mataifa (UN), ambao bado haukuwa umeamua kulijadili suala la Sudan katika Baraza la Usalama.

Hata katika shambulio lililoua zaidi ya watu 60 kambi ya wakimbizi Tripoli, baraza hilo halikuweza kutoa tamko la pamoja; wajumbe wake wa kudumu walihitilafiana kwa undani nani alaumiwe.

Wakati viongozi wa waandamanaji walikuwa wakifurahia juhudi za Abiy kama vile ni mkono wao wa ziada na sauti inayosikika kwa ufasaha zaidi anga za kimataifa nini kifanyike Sudan, Baraza la Kijeshi lilikuwa linamwona Abiy kama nuksi, aliyekuja kuvuruga mipango yao.

Tofauti na baadhi ya wataalamu walivyokuwa wakisema, kuwa ni jambo la msingi kukubaliwa na pande zote mbili, Abiy aliingia Sudan kwa kuitaarifu tu serikali hiyo ya kijeshi kuwa anaenda huko na waweke mazingira stahili ya kufanya mkutano.

Kwanza alifaulu kufikia makubaliano ya awali lakini majenerali wakatangaza tamati tofauti ya mazungumzo, yaani watoe jibu lao la mwisho.

Abiy akarudi tena kwa majadiliano, majenerali wakawakamata wapinzani walioshiriki.



Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed (kushoto) na kiongozi wa kijeshi nchini Sudan, Jenerali Abdel Fattah al-Burhan walipokutana jijini Khartoum nchini Sudan mwezi Juni mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**

Hapo ukaanza mgomo nchi nzima wa kutoitii serikali, na bila kufanya fujo zozote au kutwaa silaha, kwani kosa hilo likifanyika majenerali watakuwa wamepata wanachokitafuta, yaani kurudisha 'utawala wa sharia' na kupambana na wahalifu.

Ilipoonekana kuwa mgomo huo umefaulu na unafuatwa bila kipingamizi licha ya majenerali kuwaambia watu wapuuze tangazo hilo waendelee na shughuli zao za kawaida, ikabidi warudi mezani.

Abiy akasimamia kufikia makubaliano ya kuachiliwa viongozi wa upinzani waliokamatwa baada ya mkutano wake na kukubaliwa kipindi cha mpito cha miaka mitatu, miezi 18 ya mwanzo ikiongozwa na jeshi na miezi 18 ya mwisho ikiongozwa na raia.

Ndipo hapo linakuja swali la kufaulu kwa Abiy wakati alikuwa anaaminiwa na upande mmoja kutokana na alichokifanya nchini mwake, na bila kusema hivyo hadharani majenerali Sudan wangefurahi kama angekaa kwake Addis Ababa ashughulikie mioto ya hapa na pale kama uasi wa hivi karibuni jimbo muhimu la Amhara.

Jambo la kushangaza ni kuwa uasi huu uliokuwa na vianzio katika ngazi za juu za Jeshi la Ethiopia na kuchukua maisha ya mkuu wa majeshi, jenerali mstaafu aliyekuwa akimtembelea, na gavana wa Amhara, lilizimwa mara moja.

Abiy, akitokwa na machozi wakati wa mazishi ya wasaidizi wake hao, akaibuka mshindi na kiongozi thabiti.

Kwa maana hiyo hapakuwa na hata jambo moja katika uongozi wa Abiy na mwelekeo wake nchini kwake wa kutiliwa shaka, hali ambayo iliimarisha mkono wake katika majadiliano nchini Sudan.

Ila siyo uthabiti wa msuluhishi unaoeleza kwanini akafaulu ila umoja wa dhati na dhamira ya watu wa Sudan kutaka serikali ya kiraia inayoongozwa na wakuu wa makundi tofauti ya wanataaluma wanaoongoza maandamano.

Utawala wa kijeshi chini ya Jenerali Omar el Bashir ambaye waliopo madarakani ni watu wake wa karibu, kimsingi ulikuwa unasimamia maslahi ya jeshi lenyewe, utawala uliojaa 'nipe nikupe' kwa wanaofahamika serikalini, na mahafidhina maridhawa wanaosimamia haki zao za kunyang'anya mali kibaguzi, ili wajitanue.

Si rahisi kuelewa kilichokuwa kinapita katika vichwa vya majenerali 'mti mkavu' ila ni wazi walichelea kuendeleza sera za umwagaji damu kwani wangeongezwa katika orodha ya wahalifu wanaotakiwa na Mahakama ya Kimataifa ya Jinai kama Jenerali al Bashir mwenyewe.

Marekani tangu kuingia madarakani kwa utawala wa Rais Donald Trump iliweka tahadhari ya kutotaka kuingia nchini humo kwa watu wanaotoka katika nchi za kijihadi kama Somalia, Iran, Sudan, Libya, Afghanistan, Yemen, Syria, n.k.

Endapo majenerali wangeanza kumwaga damu halafu mwishowe waondolewe madarakani kwa njia moja au nyingine, wapinzani wangewakabidhi The Hague pamoja na mpinduliwa al Bashir, hivyo walitoa vitisho, wakaua watu wachache, kuweka ndani viongozi wa upinzani, lakini mgomo ulipofuatwa na nchi ikaanza kukwama, walinywea.

Jambo ambalo limefanikisha kazi ya Waziri Mkuu Abiy ni kukwama kwa majenerali kutumia vianzio vya kuungwa mkono serikali ya kijeshi tangu mwaka 1989 ikusanye waandamanaji tofauti kuitetea.

Kimsingi serikali ya kijeshi imebaki inaungwa mkono na matabaka ya wahodhi ardhi na mifugo wanaochelea mabadiliko na utawala wa sheria, lakini hizo ni familia ambazo zimetapakaa katika maeneo mengi nchini humo, hasa upande wa Kaskazini na waliojitumbukiza Darfur na kwingineko kwa kupora, n.k.

Ambacho hawawezi kufanikisha ni kuungwa mkono kikabila kwa upande mmoja na kidini kwa upande wa pili, kwani mwamko wa mabadiliko unatawala katika makabila yote na suala la dini ni sehemu tu ya suala la ukabila, yaani utii kwa wakuu wa jumuiya maeneo tofauti zinazoongozwa kwa jadi, mila fulani. Ni demokrasia tu sasa.

> Abiy alipata sifa kubwa kimataifa alipoondoa uadui wa miaka mingi kati ya Ethiopia na Eritrea, nchi ambayo ilipambana kwa miaka 29 (1962-1991) kujiondoa Ethiopia, baada ya Mfalme Haile Selassie kuondoa uhuru wa kujiamulia wa eneo hilo akalifanya liwe jimbo la kawaida.

UCHAMBUZI

# Bavicha: Chadema ilihusika kesi ya wakurugenzi kutosimamia uchaguzi

## Ilifanya kwa kificho baada ya kugundua kwamba serikali hufuatilia sana mlalamikaji akiwa Chadema

**Na Enock Chaulema**

TANZANIA inaelekea kwenye uchaguzi mkuu mwakani, ikianza na uchaguzi wa serikali za mitaa mwishoni mwa mwaka huu.

Vyama vya siasa ambavyo kwa kawaida huwa ndiyo vinavyotoa wanachama wa kugombea nafasi mbalimbali kuanzia wenyeviti wa serikali za mitaa, madiwani, wabunge na rais viko katika maandalizi kabambe vikisubiri kipenga tu kipulizwe na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Mwandishi wetu alipata fursa ya kufanya mahojiano na Mwenyekiti wa Baraza la Vijana la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Bavicha), Patrick Ole Sosopi kuhusiana na masuala mbalimbali likiwamo la uchaguzi.

**Fuatilia mahojiano hayo:**

**SWALI:** Baraza la Vijana la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAVICHA) limejiandaa vipi kwa uchaguzi ujao tukianza na uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu?

**JIBU:** Wajibu wa taasisi yoyote ya vijana katika vyama vyetu vya siasa, Afrika na Tanzania na mahali popote duniani, vijana ndio nguzo ya taasisi yoyote ile hata nje ya vyama vya siasa. Kama ilivyo kawaida, uti wa mgongo wa Chadema ni Bavicha. Hivyo uimara wa Bavicha ni uimara wa chama chetu kama chama kikuu cha upinzani. Ukitizama safu ya viongozi mpaka ngazi ya Taifa unaona kwamba zipo sura za ujana.

**SWALI:** Kwa maana ipi?

**JIBU:** Naibu Katibu Mkuu Bara, John Mnyika, Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Salum Mwalimu, Makamu Mwenyekiti wa Chadema Taifa- Zanzibar, Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake la Chadema, Halima James Mdee hajazidi miaka 40. Mostly ni youth age (Hasa ni umri wa ujana). Kwa hiyo kama Mwenyekiti wa Baraza na Msemaji Mkuu wa Baraza, tunawajibu wa kuhakikisha kuwa chama kinashinda. Tunawajibu wa kuhakikisha kinapata wagombea weather (wawe) ni vijana au age (umri) nyingine yoyote ile, bila kujali jinsia kushiriki uchaguzi,

kufanya kampeni na kushinda. Tumejiandaa, tumefanya training (mafunzo) ya vijana, tumekuwa na Bavicha Leadership Awards 2017, 2018 na tunatarajia tena kuwa nayo mwaka huu ambapo kila mwaka wanagraduate (hitimu) vijana zaidi ya 100 kwa mafunzo ya zaidi ya miezi sita.

**SWALI:** Kimsingi uchaguzi huambatana na 'fitina' za siasa. Sasa Baraza lako limejiandaa vipi kuzikabili fitna za aina hii iwapo zitajitokea kwenye uchaguzi?

**JIBU:** Sisi hatufikiri kupambana kwa fitna bali kwa hoja na zinapokuja fitna tutazimudu kutokana na mazingira. Lakini hatufundishi vijana wetu namna ya kufanya fitna wala baraza langu halijajiandaa kufanya fitna. Hata hivyo, tunajua kuna vyama vinavyofanya siasa chafu hususan CCM (Chama Cha Mapinduzi). Sisi tutawakabili kwa namna watakavyokuja, kwani tuna vijana ambao wana capacity (uwezo) wa kutosha kufanya siasa katika mazingira yoyote yale.

**SWALI:** Kwa nini unasema hivyo?

**JIBU:** Tumeona mwaka huu



Mwenyekiti wa Baraza la Vijana la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Bavicha), Patrick Ole Sosopi. **PICHA: CHARLES CHAULEMA**

kuna vitimbi vingi vinafanyika. Tunakumbuka kwenye uchaguzi mdogo kule Korogwe Wakurugenzi walipokimbia ili mgombea wetu asirejeshe fomu, kufutwa ama kuondolewa kwa wagombea wetu. Kwa hiyo tumejiandaa kuhakikisha kwamba procedures (taratibu) zote tunazifuata na watu wetu wanakuwa well trained (wanafundishwa vizuri). Tuna mawakili karibia kila wilaya ili kuhakikisha kwamba fomu zetu zinajazwa sawasawa. Lakini pia tuna viongozi wetu ambao watakuwa trained (watafundishwa) kuhakikisha kwamba kila kata, kila kijiji tutapata watu ambao they are well trained (wamefundishwa vizuri) kuhakikisha kwamba hatufanyi mistake (makosa) katika kujaza fomu. Kwa hiyo tunasubiri kanuni za uchaguzi zitoke ambazo kikawaida hutolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi). Na sheria inasema miezi mitatu kabla ili tuanze maandalizi ya uchaguzi.

**SWALI:** Pamekuwa na wimbi kubwa la viongozi mbalimbali hasa wabunge na madiwani kutoka vyama vya upinzani, Chadema ikiwamo kuhamia CCM. Je, ni dalili kuwa upinzani unaishiwa nguvu?

**JIBU:** Kurudi kwa watu CCM ni historia tu inajirudia kwa sababu hakuna utafiti uliofanyika kuonyesha kwamba watu wanaporudi au wanapojiunga na CCM, upinzani unaishiwa nguvu. Nguvu inayotumika kudhibiti upinzani ni kubwa sana. Ingekuwa ni kweli upinzani

unaishiwa nguvu ama ni dhaifu, tusingeona matumizi ya nguvu kubwa ya serikali na Jeshi la Polisi wasingekuwa wanajishughulisha na upinzani wala Rais asingezuia mikutano ya hadhara. Leo karibia viongozi wote wa upinzani wana kesi mahakamani. Kila siku tunakamatwa, hata kufanya vikao vya ndani tu inaonekana ni jinai. Mimi nilikamatwa Morogoro nikiwa hotelini, naambiwa nafanya kampeni kabla ya wakati. Nikawaambia wanieleze kama ni hivyo ninamnadi nani! Naibu Katibu Mkuu wetu Salum Mwalimu alikamatwa kule Mufindi Iringa na kudhalilishwa

kwenye kikao cha kufanya chaguzi za ndani ya chama. Kule Singida, Kamanda wetu Lazaro Nyalandu alikamatwa na kupewa kesi ya rushwa. Wabunge wetu bungeni wanabanwa vikali na wengine kusoteshwa rumande. Tumeona kilichowakuta wabunge (Peter) Lijualikali, Mdee, (Godbless) Lema, (Suzan) Kiwanga, (Koseph Mbilinyi) Sugu, (Joshua) Nassari na hivi karibuni Tundu Lissu. Kwa hiyo nguvu yetu inaonekana kwa namna Serikali inavyojishughulisha na sisi.

**SWALI:** Pamekuwa na maazimio mbalimbali ya Chadema kukabili serikali na CCM, lakini hayatekelezeki. Je, mnakwama wapi?

**JIBU:** Hakuna maazimio ya vikao vyetu yanayokuwa hayatekelezeki bali tunapokuwa tunaazimia kutekeleza jambo fulani kama chama cha siasa, haiwi msahafu au biblia kwa sababu katika kutekeleza jambo na katika kuweka mkakati, yapo yanayoibuka na tunaweza ku-change (badili) mbinu ya vita au ya mapambano. Na ndio maana bado tupo kwenye game (mchezo), hatuja-move (ondoka). Maazimio yaliyofanyika Zanzibar kwa mfano hayakuwa maazimio ya Bavicha, lakini viongozi wakuu wa vyama ambao walikaa Zanzibar takriban vyama saba, waliazimia kuwa mwaka huu ni mwaka wa kudai demokrasia. Na moja ya maazimio ilikuwa ni kufungua kesi katika Mahakama zetu, kwa sababu tunaamini katika sheria. Sisi kama vijana tuna vikao vyetu tunaweza kuazimia na kusema kitu bila consultation (ushauri) wa chama, tuna hiyo mandate (mamlaka). We can speak (tunaweza kuongea) lakini kuna wakati tunaweza tukafanya ili chama kitukosoe ama chama kiturekebishe.

**SWALI:** Ni kipi unajivunia katika kipindi cha uongozi wako?

**JIBU:** Kwanza najivunia kwamba naongoza vijana ambao wana uwezo mkubwa sana, vijana ambao wapo determined, focused (wanauthubutu) na wanaelewa nini wanachokifanya. Hawapo ili kufungwa na fikra za mwenyekiti, they can sometimes challenge me (wanaweza nyakati zingine kunikosoa), hapana Mwenyekiti hiyo si right track (njia sahihi ya kwenda), tunapaswa kwenda this way (njia hii). Lakini ukienda pia kwenye taasisi za wasomi, ushiriki wa vijana katika siasa wengi ni Chadema kwa sababu ya namna ambavyo tunawashirikisha na imani yao kwa Baraza.

**SWALI:** Ni upi mkakati wako baada ya uongozi katika chama?

**JIBU:** Nina ndoto ya kuwa rais wa nchi hii, aah nina ndoto ya kuwa mbunge hiyo ndoto ya kuwa mbunge nimeshaianza, ndio maana chama kiliniamini 2015 kugombea Jimbo la Isimani (Iringa). Nina hiyo ndoto ya kuwa Rais iwapo chama changu siku moja kitaniamini. Kwa sasa umri sijafikisha, ila si dhambi kuwa na ndoto. Lakini kwa sasa baada ya uchaguzi ndani ya chama, nitakapokuwa si kiongozi ndani ya chama ninaamini kwamba si lazima nifanye siasa nikiwa mwenyekiti wa baraza. Chama hiki kina majukumu mengi, unaweza ukawa si kiongozi na bado ukakisaidia chama na wapo wanaofanya hivyo.

**SWALI:** Kuna suala ambalo lilikuwa linalalamikiwa muda mrefu kuhusu wakurugenzi kusimamia uchaguzi kabla ya uamuzi wa karibuni wa Mahakama Kuu. Hata hivyo, watu wanajiuliza Chadema ilikuwa wapi kufungua kesi kuhusu wakurugenzi kusimamia chaguzi?

**JIBU:** Chadema ilikuwa ya kwanza kufungua kesi Arusha, ikapigwa PO (ikatupwa). Tukafungua Mwanza ikapigwa PO. Kwanini? Tulipokuja baadaye kutafakari na kujua kwamba tatizo lililopo ni kwamba kesi ikifunguliwa na Chadema seriously (haswa), ikaonekana applicant wa petition (mlalamikaji) ni Chadema concentration (ufuatiliaji) mkubwa wa Serikali ku-deal (shughulikia) hiyo kesi na kufanya sabotage (hujumu) hata kwa mhimili wa Mahakama ni mkubwa sana. Kwa hiyo chama tulijua na hatukuwahi kuacha kufungua kesi mahakamani hata Dar es Salaam hapa tulifungua. Lakini katika mbinu tuliyoitumia hawakuweza kujua mimi kama Mwenyekiti katika Umoja wa Demokrasia wa kudai demokrasia tuko watu takribani 29. Hiyo ni pamoja na wanaharakati wasiokuwa wanachama wa vyama vya siasa, asasi za kiraia na wanaharakati wengine tuliweza kutengeneza hiyo movement (harakati) ambayo tulifanya na mwenyekiti wetu ni Makongoro Mahanga. kwa hiyo tuliamua kufanya in away (kwa namna) kutokutengeneza tension (mvutano) kwa watawala. Lakini we were part and parcel (sehemu) ya kila hatua ya kesi iliyokuwa ikifanyika na tulishiriki kwenda mahakamani wakati wote.

**SWALI:** Unaweza ukatueleza historia yako japo kwa ufupi?

**JIBU:** Mimi ni baba katika familia ya watoto wawili na mke mmoja. Nimezaliwa Aprili 10, 1987 Iringa, Wilaya ya Iringa, Jimbo la Isimani. Ni Mmasai ambaye nimesoma Iringa Primary, Moshi Technical, Mbalizi High School Mbeya na shahada yangu ya kwanza nimesoma Chuo Kikuu cha Kikatoliki (Ruaha Catholic University- Iringa). Nimefanya kazi na Kanisa la Anglikana hadi nilipochaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bavicha.



Kombora bora la kutungulia ndege kutoka Russia ambalo Uturuki imelinunua kinyume na matarajio ya Rais Donald Trump wa Marekani. **PICHA: MTANDAO**

# Mzozo Syria wapangua utii wa Uturuki NATO

## • Yanunua silaha bora S-400 za Russia

**Na Ani Jozeni**

WAKATI malumbano yanaendelea kuhusu hatua ya Uturuki kununua mifumo ya kutambua ndege au kombora linalokuja umbali wa kilomita 400 na kulisambaratisha kabla halijasogea zaidi, wachunguzi wa habari bado wanatafuta Uturuki imefikaje hapo kwani ni nchi mwanachama wa NATO, umoja wa kujihami wa nchi za Magharibi.

Siyo rahisi kusema kama kinachotokea ni Uturuki kupoteza sifa ya kuendelea kuwa mwanachama wa NATO, au ni mkasa wa jumla wa umoja huo na ushindi mwingine wa Rais Vladimir Putin wa Russia kuupangua, pamoja na ule wa kiuchumi wa Umoja wa Ulaya.

Marekani inachukua hatua za hapa na pale, kuitenga Uturuki.

Taarifa mojawapo ya hivi karibuni ilimnukuu Waziri wa Ulinzi wa Uturuki akimweleza mwenzake wa Marekani kuwa ununuzi wa mfumo wa ulinzi wa anga wa S-400 haukuwa wa kupendelea, ila wa lazima.

Alisema kuwa Uturuki iko katika hatari kubwa, hivyo ikaona haina njia ila kutumia kiasi cha dola za Marekani bilioni mbili kununua mfumo huo, na huku utawala wa Rais Donald Trump ukionya Uturuki kuwa iko mbioni kuwekewa vikwazo vya uchumi.

Licha ya umuhimu wa kununua mfumo huo wa ulinzi wa anga, Uturuki inasema bado ni sehemu ya mfumo wa ulinzi wa nchi za Magharibi, wakati hasimu mkuu wa NATO ni hiyo hiyo Russia.

Cha kushangaza katika wasiwasi wa Marekani kuhusu ununuzi huo wa mfumo wa ulinzi wa anga siyo urafiki kati ya Uturuki na Russia ila kuchanganya mifumo ya utumiaji wa ndege za F-35 ambao ni za kisasa zaidi za Marekani, zilizopo Uturuki, halafu mfumo huo mpya.

Marekani inasema kuwa mifumo ya uendeshaji wa F-35 ukichanganywa na S-400 ni wazi kuwa vielelezo maridhawa vya muundo wa F-35 vitatiririka kwa mashirika ya Russia ya ujasusi na teknolojia, jambo ambalo halikubaliki Marekani.

Nje ya kusitisha kufundisha marubani wa Uturuki juu ya utumiaji wa F-35, Marekani inatafakari hatua, ila kuiuzia Uturuki mifumo ya Patriot kuko hatarini.

Ni serikali ya Uturuki iliyoagiza ndege za F-35 kutoka kampuni ya Marekani ya Lockheed Martin, halafu na mfumo huo wa ulinzi wa anga, kana kwamba ni kuwa na ndege bora za ushambuliaji na safu bora ya ulinzi.

Tatizo ni kuwa wanaotoa mifumo hiyo miwili kimsingi hawachanganyikani, lakini Uturuki ilionyesha dalili za kujali zaidi maslahi yake na siyo kuoanisha na mifumo ya kimkakati na mahusiano mapana kiulinzi yaliyopo.

Ni kuamua ni mfumo upi au ni kambi ipi ya ulinzi ambayo Uturuki inataka kuhusishwa, NATO au Russia.

Kwa vitendo vyake na siyo hasa kwa maneno yake, Uturuki inaonyesha wazi kuwa ina imani zaidi na mfumo wa Russia na siyo ule wa NATO kwani Rais Recep Tayyip Erdogan amekuwa akipata hitilafu nyingi kupitisha mambo yake katika ushirikiano na Marekani.

Bado kuna mvutano kati ya nchi hizo kuhusu kutorudishwa Uturuki kwa mwanazuoni Fethullah Gulan ambaye kiongozi huyo wa Uturuki anadai aliongoza jaribio la kuipindua serikali yake 2016.

> Ndiyo hapo mfumo wa utawala na mwelekeo wa kiitikadi, na hivyo kimkakati wa Rais Erdogan siyo rahisi kuoanishwa na utii au ushirika kwa NATO, kwani haoni tatizo kuwa na mifumo ya kisasa kutoka Russia, halafu aongezee tena ya Marekani.

La maana zaidi ni Marekani kuhusika na wapiganaji wa ki-Kurdi huko Syria, kinyume na Uturuki.

Suala ambalo halionekani vyema katika baadhi ya mijadala ya vyombo vya habari na mitandao ni hatari ambayo Uturuki inasema inahofia, kwani maadui zake halisi wanaofahamika ni wapiganaji wa ki-Kurdi kwa upande mmoja na wale wa dola ya Kiislam (ISIS) kwa upande mwingine.

Hawa hasa ni wapiganaji wanaotumia bunduki nzito, mizinga na roketi za kubeba begani, n.k. na siyo kurusha ndege au makombora kutoka kilomita 1000 dhidi ya Uturuki.

Ina maana kuna nchi ambazo Uturuki inajenga mifumo ya kujihami ili kujilinda nazo, na si hayo makundi ya kigaidi.

Ndiyo hapo mfumo wa utawala na mwelekeo wa kiitikadi, na hivyo kimkakati wa Rais Erdogan siyo rahisi kuoanishwa na utii au ushirika kwa NATO, kwani haoni tatizo kuwa na mifumo ya kisasa kutoka Russia, halafu aongezee tena ya Marekani.

Isitoshwe, wakati nchi kadhaa na wengi kati ya wajumbe wa mabaraza ya uwakilishi na senate nchini Marekani waliunga mkono hali ya Misri kudhibitiwa baada ya mabadiliko ya kikatiba ya aliyekuwa Rais wa Misri, hayati Mohamed Morsi, Uturuki imeomboleza kifo cha mwanaharakati huyo wa Muslim Brotherhood ya Misri kama mfia haki. Ina maana Uturuki inazihofia Misri na Jordan, sahaba wa Marekani.

Siyo rahisi kusema kama Rais Erdogan anajitambua kama mwenza wa mfumo wa kujihami wa ukanda wa Mashariki ukiongozwa na Russia au bado 'anapima,' lakini dalili zinaonyesha kuwa tofauti zake na Russia ni chache, wakati maeneo ya ugomvi na Marekani yamesheheni.

Kuanzia demokrasia na haki za binadamu nchini Uturuki, kupambana, kuwasaka wapiganaji wa ki-Kurdi wenye uhusiano mzuri na Marekani, kuelewana kuhusu hali ya Syria, na sasa kununua mitambo ya ulinzi wa anga, zote ni hatua kinyume na Marekani. Zinaoana kabisa na mikakati ya Russia.

Uturuki inaelekea kudhania kuwa ununuzi wa silaha kutoka Marekani ni suala la kiuchumi hivyo inaweza kununua mfumo wa ulinzi wa anga kutoka Russia na bado ikaendelea na mipango ya kununua ndege za F-35 na makombora ya ulinzi, Patriot.

Tofauti na kuandika tu hundi, Marekani inaangalia suala hilo kama la mfumo wa ulinzi kwa jumla na kujua nani washirika katika mfumo wa ulinzi wa NATO, na ni wazi kuwa hivi sasa uanachama wa Uturuki NATO unaning'inia kwa kamba rojorojo. Ambacho hakipo kwa Erdogan na kwa Putin vile vile ni kujali sana demokrasia.

Uturuki inasema kuwa Marekani tayari ilishakataa kuiuzia mifumo ya ulinzi wa anga kwa makombora ya Patriot, hivyo ikabidi itafute kwingine, na ofa ya Russia ilikuwa ni pamoja na kuhamishia teknolojia ya uendeshaji wake kwa haraka zaidi.

Baada ya mpango wa kununua mfumo wa S-400 kutoka Russia kukamilika, Marekani imesema Uturuki haitaruhusiwa kushiriki katika utengenezaji wa ndege za F-35 au kuzinunua, kwani S-400 ni hatarishi kwa F-35.

Tayari Marekani iliiwekea vikwazo Uturuki wakati Erdogan alipomkamata kasisi mmoja wa Marekani ili abadilishane na Gulen, vikwazo vikasababisha sarafu ya Uturuki kuporomoka.

Ilimwachia kasisi na vikwazo vikaondolewa, sarafu ikatengemaa, lakini sasa Erdogan anatumia akiba ya fedha za nje kununulia mtambo wa ulinzi wa anga ambao si rahisi kuona matumizi yake halisi kwa sasa.

Uturuki ikiwekewa tena vikwazo kutokana na kuwa tishio kwa maslahi ya Marekani na washirika wake katika ukanda wa Mashariki ya Kati, haitakuwa rahisi kujinasua katika mtego huo.

Faida za uhasama na Marekani kwa utawala wa Erdogan ni hamasa ya kisiasa, kukwepa kuachia wafungwa, wa-Kurdi, kutazamia kuwa uwekezaji wa Russia, China utatosha mahitaji.

# Atoa wiki moja upanuzi chumba cha maiti

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ametoa muda wa wiki moja kwa uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, kukamilisha ujenzi wa upanuzi wa chumba cha kuhifadhia maiti pamoja na jengo la kufulia nguo kwenye Kituo cha Afya cha Ikuti.

Chalamila alitoa kauli hiyo hivi karibuni wakati wa ziara yake ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa chumba cha kuhifadhia maiti katika Kituo cha Afya cha Ikuti alionyesha kutoridhishwa na hatua ilipofikia na kuamuru ndani ya wiki moja ujenzi huo ukamilike.

Alisema zipo sababu mbalimbali ambazo zimesababisha ujenzi huo kukamilika kwa wakati licha ya serikali kutoa fedha na kumwagiza Mkurugenzi wa Wilaya hiyo, Loema Peter, kufuatilia kwa makini kama mafundi wanaojenga tayari walipatiwa fedha zao.

"Sioni sababu ya kusuasua kwa ujenzi wa jengo la kuhifadhia maiti katika kituo hiki, serikali ilijitahidi kutoa fedha tena kwa wakati, lakini kinachoendelea hapa ni madudu matupu sasa natoa muda wa wiki moja halmashauri mnasimamia na kukamilisha ujenzi huo vinginevyo mtaona," alisema Chalamila.

Alisisitiza kukamilika kwa ujenzi huo haraka ili huduma zianze kutolewa kwa madai kuwa vifaa vilivyotolewa ikiwamo mashine zimekaa nje kwa muda wa miezi mitatu na upo uwezo wa kuharibika.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Julius Chalya, alikiri ujenzi huo kusua na kudai ni uzembe na usimamizi mbovu wa wataalamu.

Alidai mkurugenzi alipewa jukumu la kusimamia ujenzi huo badala ya kuwaachia wataalamu na mafundi ambao walifanya kazi kiholela.

# Takukuru yaonya wagombea kutumia rushwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Mkoa wa Mbeya imetoa onyo kwa wagombea wakiwamo wenyeviti katika uchaguzi wa serikali za mitaa na wananchi kutojihusisha na vitendo vyovyote vya rushwa kwa kuwa watashughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

Onyo hilo limetolewa jana na Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Mbeya, Julieth Matechi, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema zinapofika nyakati za uchaguzi baadhi ya watu wasiokuwa na maadili hutumia mwanya huo kuomba na kupokea rushwa ili kupata nafasi ya uongozi.

Alisema katika uchaguzi ujao wa serikali za mitaa, ambao unatarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu, taasisi hiyo imejipanga kutokuwa na mianya yoyote ya rushwa kuanzia kwenye michakato ya ndani ya chama na kwenye kupiga kura.

"Niwahakikishie wagombea na wananchi kuwa Takukuru hatutalala kwenye uchaguzi huo, hatutakubali kuona vitendo vya rushwa tunahitaji uchaguzi huo ufanyike kwa uhuru na haki ili wagombea watakaopita wawe ni chaguo la wananchi, naomba muepukane na rushwa," alisema Julieth.

Alisema kinapofikia kipindi cha uchaguzi, wagombea wasiokuwa na maadili hutumia fedha zao kuwashawishi wananchi kwa kuwapa fedha au zawadi ili wachaguliwe.

Aliwaomba wananchi kutoa taarifa za viashiria vya rushwa kwa Takukuru ili washughulikiwe na itasaidia kudhibiti vitendo hivyo.

Vile vile, Julieth alieleza kuwa Takukuru Mkoa wa Mbeya katika kipindi cha mwezi Aprili hadi Juni, mwaka huu, wamefanya ufuatiliaji na ukaguzi na ilibaini kasoro ndogondogo zilizoonekana katika hatua za mipango, usanifu na nyaraka za zabuni na hatua za ununuzi na utunzaji wa nyaraka.

Alisema katika taarifa hiyo ya robo ya mwaka, jumla ya matukio 78 ya tuhuma za rushwa na makosa mengine yalipokelewa na kati ya hizo, Halmashauri taarifa (25), Mahakama (13), Sekta binafsi (13), Polisi (4), Idara ya Ardhi (3), Vyama vya Ushirika (2), Mashirika ya Umma (6), Idara ya Afya (2), Maliasili (1), Magereza (1) na Idara ya Ardhi (3).

Alisema kati ya taarifa hizo 48, zilifanyiwa kazi na kukamilika kwa kutolewa uamuzi mbalimbali kulingana na tuhuma pia kesi mpya nane zilifunguliwa katika Mahakama za Wilaya ya Chunya, Rungwe, Kyela na Mbeya.



Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga (wa tatu kushoto), akiwa na uongozi wa mkoa wa Shinyanga, wakikagua ununuaji wa zao la pamba kwenye kiwanda cha Afrishani Shinyanga mjini jana, baada ya vyama vya msingi vya ushirika AMCOS kukosa fedha za kukunua zao hilo. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Hospitali yajengwa miaka 6 bila kukamilika

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dk. Mary Mwanjelwa, amesikitishwa na ujenzi Zahanati ya Mkola Kongolo, iliyopo Kijiji cha Mswiswi, ulioanza tangu mwaka 2013 kushindwa kukamilika kwa wakati licha ya wananchi kuchangia zaidi ya Sh. milioni 15.

Aliyasema hayo akiwa kwenye ziara ya kutembelea miradi ya maendeleo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya.

Alisema licha ya wananchi kuchangia Sh. milioni 15 kwa ajili ya ujenzi wa zahanati, mpaka sasa haijakamilika.

Aliongeza kuwa katika ujenzi huo Rais Dk. John Magufuli, alichangia Sh. milioni tano ili kuhakikisha zahanati hiyo inajengwa na kukamilika kwa wakati wananchi waanze kupata huduma za matibabu.

Sijafurahishwa na hali halisi ya zahanati hii ilivyo kwa sasa, fedha zilitolewa na wananchi, lakini pia serikali sijui zimeliwa au la, nakuagiza mkurugenzi unipe taarifa kwa maandishi lini zahanati hiyo itakamilika," alisema Dk. Mwanjelwa.

Aliagiza wataalamu na mkandarasi aliyepewa tenda ya kujenga zahanati hiyo aikamilishe haraka ikiwa imejengwa katika ubora unaotakiwa ili kuwaokoa wananchi waliokuwa wanatumia gharama kufuata huduma za matibabu mahali kwingine.

Pia alishauri zahanati hiyo izungushiwe uzio kwa ajili ya usalama kwa kuwa imezungukwa na makazi ya watu.


Aliwasisitiza watumishi wa umma wanaopewa dhamana ya kusimamia miradi ya maendeleo kuwa wazalendo kwa kuhakikisha ujenzi wa miradi inakamilika kwa wakati ili kuwanufaisha wananchi badala ya kuchelewa kwa maslahi yao binafsi.

Alisema ukaguzi huo wa zahanati ni utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), ambayo inatembelea miradi mbalimbali kwa ajili ya kukagua hatua mbalimbali zilipofikia na kuangalia changamoto zinazokwamisha.

Kadhalika Dk. Mwanjelwa katika ziara yake pia alikagua ujenzi wa madarasa mawili ya Shule ya Msingi Mkola na kufurahishwa kukamilika kwa ujenzi huo ambao utasaidia kuondokana na changamoto ya uhaba wa vyumba vya madarasa.

Alisema Shule ya Msingi Mkola inakabiliwa na changamoto ya madarasa na kwa sasa shule ina jumla ya madarasa sita pekee.

Hata hivyo, Kaimu Ofisa Elimu Takwimu na vifaa wilayani Mbarali, Fausto Mwinuka, alimweleza Dk. Mwanjelwa kuwa ujenzi utakamilika kwa wakati kwa kuwa mpaka sasa wamefikia asilimia 40.





# Zimamoto kujenga vituo saba vipya

**Na Renatha Msungu,**

DODOMA

KATIKA kurahisisha huduma ya zimamoto na uokoaji, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, linatarajia kuanza ujenzi wa vituo vya zimamoto katika mikoa saba ikiwamo Dodoma.

Aidha, jeshi hilo limezitaka mamlaka husika kuwahimiza wananchi kuwasilisha ramani za ujenzi wa nyumba kabla ya kuanza ujenzi, ili kuona uwezekano wa kuwashauri kuweka milango ya dharura.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamishna wa Fedha na Utawala wa Zimamoto na Uokoaji, Baraka Semwanza, aliitaja mikoa ambayo wanatarajia kujenga vituo hivyo ni Singida katika Wilaya ya Manyoni, Iringa (Kilolo) na Tabora katika wilaya za Urambo na Nzega.

Semwanza alisema mikoa mingine ambayo inatarajia kujengwa vituo pamoja na wilaya zake ni Kagera (Karagwe) na Manyara wilayani Babati.

Alisema katika mikoa hiyo kuna baadhi ya halmashauri tayari zimetoa maeneo kwa ajili ya jeshi hilo kuanza ujenzi wa vituo kwa kushirikiana na wananchi wa maeneo husika.

"Katika mikoa niliyotaja tayari tumepata maeneo na tunatarajia kuanza ujenzi wa vituo hivyo haraka iwezekanavyo," alisema Kamishna Semwanza.

Alisema katika mkoa wa Dodoma alizitaja baadhi ya wilaya ambazo zinatarajiwa kujengwa vituo hivyo ni pamoja na Chemba, Mpwapwa, Chamwino na Bahi na kwamba watajenga kituo katika mji wa serikali ulioko eneo la Mtumba.

Semwanza pia alisema katika mkoa wa Njombe, jeshi hilo liko katika hatua za kutoa fidia kwa wananchi ili kupisha maeneo ambayo yanastahili kujengwa kituo hicho.

Pamoja na maeneo hayo kukosa vituo, alisema jeshi hilo limeweka askari kwa ajili ya kutoa elimu kwa wananchi kuhusiana na huduma za awali za uzimaji moto pale majanga yanapotokea.

Alisema wananchi wanapaswa kutoa ushirikiano pale jeshi linapotoa elimu kuhusiana na jinsi ya kutoa huduma ya kwanza ya uzimaji moto.

Vilevile, alizitaka halmashauri zinapogawa maeneo, zikumbuke Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kuwa linahitaji maeneo kwa ajili ya kujenga vituo vya zimamoto ambavyo ni muhimu kuwapo katika maeneo mbalimbali wanayoishi watu.

Wakifanya hivyo, alisema watakuwa wamelisaidia kwa kiasi kikubwa jeshi kutokana na ukweli kwamba wanahitaji kuwa na vituo katika maeneo mbalimbali ili kukabiliana na majanga ya moto yanayotokea.

Kuhusu mamlaka husika kuwashauri wananchi kupeleka ramani katika jeshi hilo kabla ya kuanza ujenzi, alisema ni muhimu kufanya hivyo kwa sababu wanahitaji kuwashauri kuweka milango au dirisha la dharura ili kukabiliana na majanga ya moto pale yanapotokea.



Mkurugenzi wa asasi ya kiraia ya Women Wake Up (Wowap), ambaye pia ni Mbunge wa Viti Maalum, Fatuma Toufiq, akizungumza kwenye semina kuhusu ushirikiano wa kufanya kazi kwa pamoja, iliyoshirikisha asasi zisizo za kiserikali na vyombo vya habari, jijini Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Jiji lawapa mipaka wamachinga

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imewataka wafanyabiashara wadogo, maarufu kama wamachinga, kutokuweka meza na fremu za bidhaa zao katika maeneo ya barabara na yale yasiyo rasmi.

Badala yake, jiji limewataka wawe na vifaa vinavyohamishika ili kuwezesha maeneo hayo kuwa wazi mara wanapomaliza shughuli zao.

Rai hiyo ilitolewa na Ofisa Masoko wa Jiji hilo, James Yuna, alipokuwa akizungumza kwenye kikao kilichowahusisha viongozi wa wafanyabiashara hao.

Alisema badala ya kuweka fremu na meza hizo kwenye maeneo hayo wanatakiwa kuhakikisha wanatumia vifaa vinavyohamishika ili wanapomaliza maeneo hayo yanatakia kuwa wazi kwa ajili ya matumizi mengine.

Aidha, aliwataka pia wafanyabiashara hao kufuata na kuheshimu sheria, kanuni na utaratibu kama zilivyoelekezwa, ikiwamo kuhakikisha katika maeneo yao yanakuwa safi kwa muda wote.

Hata hivyo, aliwataka wafanyabiashara hao kuungana kwa pamoja ili wawe na chombo kitakachoshirikiana na halmashauri ya jiji kwa upande wa utendaji wao wa kazi wa kila siku.

Wakizungumza kwenye kikao hicho, viongozi wa wafanyabiashara hao walisema ni wakati wao sasa kuhakikisha wanaunda umoja utakaowawezesha kutatuliwa kero zao na halmashauri ya jiji.

Mrisho Baraka, Mwenyekiti wa Soko la Jioni eneo la Nyerere Square, alisema kuwapo kwa umoja huo kutasaidia kutatua changamoto wanazokabiliana nazo kwenye biashara zao.

Naye Anna Charles, alisema kuwapo kwa chombo hicho cha wajasiriamali kitawezesha kuwasilisha mahitaji yao kwa wenye mamlaka ya usimamizi kwa wakati.

# Wenye ulemavu waomba miundombinu rafiki kwao

**Na Peter Mkwavila,**

DODOMA

WATU wenye ulemavu mkoani Dodoma wameiomba serikali kuwaondolea vikwazo vinavyowakabili ikiwamo miundombinu rafiki ambayo kwa sehemu kubwa bado inasahaulika kwa upande wao.

Ushauri huo ulitolewa na Mchungaji Kiongozi Marcel Mushi wa Kanisa la Tanzania Assemblies of God (TAG) Mnadani Revival Temple jijini Dodoma.

Mchungaji Mushi alisema watu wenye ulemavu wana haki sawa kama ilivyo kwa wengine, hivyo wanatakiwa kuangaliwa kwa jicho la upendo na wanastahili kulindwa na kutunzwa.

Alisema walemavu wana haki ya kupewa huduma pamoja na kuondolewa vikwazo mbalimbali na kuwekewa miundombinu rafiki ili waweze kufikia maeneo wanayo hitaji.

Kwa mujibu wa Mchungaji Mushi, watu wenye ulemavu pamoja na hali walizo nazo pia wana uwezo wa kufanya shughuli mbalimbali ambazo zinaweza kuwaingizia kipato, hivyo wanatakiwa kuwezeshwa ili waondokana na dhana iliyojengeka kuwa wao ni ombaomba.

Kwa upande wake, Grence Masima akizungumza kwenye ibada hiyo aliwataka Watanzania kuondokana na unyanyapaa na ukatili dhidi ya makundi hayo badala yake waonyeshe upendo katika kuwatatulia changamoto wanazokabiliana nazo katika maisha yao ya kila siku.

Masima ambaye ni mtu mwenye ualibino aliyekataliwa na baba yake mzazi kutokana na ulemavu wake, alisema kuwa inasikitisha kuona bado kuna ukatili na unyanyapaa.





Mafundi wakiendelea na ujenzi wa barabara za juu "interchange', katika makutano ya Barabara ya Mandela, Morogoro na Sam Nujoma, katika eneo la Ubungo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Mtoto asimulia alivyobakwa na baba wa kambo

**Na Rahma Suleiman,**

ZANZIBAR

MAHAKAMA ya Mkoa ya Mwera Unguja, imeanza kusikiliza kesi ya mtoto mwenye umri wa miaka 13 anayedaiwa kutoroshwa na kubakwa na baba wa kambo.

Katika kesi hiyo, mashahidi wawili walifika kizimbani mbele ya Hakimu Said Hemed, akiwamo mtoto na mama mzazi wa mtoto huyo.

Shauri la kesi hiyo linamhusisha Abuu Ameir Sudi 'Maganga' (58), mkaazi wa Bwejuu Kusini Unguja ambaye anadaiwa kumtorosha mtoto huyo aliyekuwa chini ya uangalizi wa wazazi wake.

Mtoto huyo (jina limehifadhiwa) alidai mahakamani hapo kwamba alikwenda kwa mshtakiwa huyo ili kupata msaada wa kulipa fedha alizoambiwa na mama yake akazilipe baada ya kudaiwa kuwa ameziiba.

Alidai kuwa ushauri wa kwenda kwa mshtakiwa huyo ulitokana na rafiki zake ambao alikutana nao asubuhi na kuwaelezea yaliyomkuta nyumbani kwao.

Kwa mujibu wa mtoto huyo, alipofika nyumbani kwa mshtakiwa, alipiga hodi na kupokewa na mkewe na baada ya hapo, alitokea Maganga ambaye alimchukua na pikipiki na kwenda nae kwenye nyumba ya mawe.

Alidai kuwa alipofika huko mshtakiwa alimwamuru kuvua nguo na kumlazimisha kufanya naye ngono kisha kuondoka akiwa amemwacha mtoto huyo mahali hapo.

Alidai kuwa alivaa nguo zake huku akilia na kuanza kurandaranda ovyo mitaani.

Mtoto huyo alidai kuwa hakumbuki muda gani alitokea mjomba wake aliyetambulika kwa jina la Mrisho maarufu kama Gombe na kumpeleka nyumbani kwao.

Alipofika huko, alidai kuwa alihojiwa na dada yake Fatma kwa kutaka aeleze alikuwa wapi na akishindwa kueleza atapelekwa kituoni jambo ambalo lilimfanya ajieleze.

Baada ya kumweleza, alidai kuwa dada yake huyo alilia jambo ambalo lilisababisha mama mzazi wa mtoto kufika kisha naye kueleza kilichotokea na hatimaye kwenda katika kituo cha Polisi cha Paje kwa ajili ya kufungua jalada.

Alidai kuwa baada ya kufika kituoni walipewa karatasi ya kwenda Hospitali ya Makunduchi kwa ajili ya uchunguzi na baada ya kufika hospitali alichunguzwa na badaaye kuruhisiwa kurudi nyumbani kwao.

Naye mama wa mtoto huyo, alidai mahakamani hapo kuwa siku hiyo alimtaka mtoto wake azirejeshe pesa za Zainab na baada ya muda aliona mtoto wake hamwoni na kurejea kwa siku kadhaa ambazo hakujua ni ngapi.

Alidai kuwa baada ya mtoto wake kuwa haonekani, alihangaika kumtafuta mpaka siku ambayo aliletwa na mjomba wake na baada ya kumhoji alikataa kusema na badala yake akamwambia dada yake Fatma amhoji ndipo akadai kuwa aliingiliwa na mshtakiwa huyo.

Awali, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Safia Serembe, alidai mahakamani hapo kwamba mshtakiwa anadaiwa kutenda makosa mawili ambayo ni kumtorosha mtoto ambalo alitenda Mei 18, mwaka huu saa 8:00 mchana hadi saa 11:30 za jioni huko Bwejuu Wilaya ya Kusini.

Alidai kuwa mshtakiwa alimchukua mtoto wa kike mwenye umri wa miaka 13 aliye chini ya wazazi wake na kumpeleka kwenye nyumba yake nyingine

Bwejuu, kitendo ambacho ni kosa kisheria.

Aidha, alidai kuwa siku hiyo hiyo kati ya saa 11:30 za jioni hadi saa 3:00 usiku, alimwingilia kimwili mtoto wa miaka 13 kitendo ambacho ni kosa kisheria.

# Zanzibar kicheko ufaulu wa mitihani

**Na Rahma Suleiman,**

ZANZIBAR

KIWANGO cha ufaulu wa kidato cha sita kwa mwaka huu kimeongezeka katika Mkoa wa Mjini Magharib Unguja ikilinganishwa na mwaka jana.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkuu wa Mkoa huo, Ayoub Mohammed Mahmoud, alisema kwa mwaka jana wanafunzi waliyopata daraja la kwanza walikuwa 96 lakini kwa mwaka huu wameongezeka hadi 155 sawa na asilimia 90 ya ongezeko la ufaulu kwa mwaka jana.

Alisema kuongezeka kwa ufaulu huo kunatokana na ushirikiano mkubwa uliopo baina ya serikali, walimu, wazazi na walezi katika kuhakikisha wanawasimamia vyema wanafunzi hao ili kuona wanafanikiwa vizuri kwa kuwaongezea muda wa kupitia masomo yao.

"Waliopata daraja la pili kwa mwaka huu wa 2019 katika shule zilizomo kwenye mkoa wangu ni 476 wakati mwaka jana walikuwa 377," alisema.

Aidha, alisema licha ya ufaulu huo kuwa mzuri, pia kwa mwaka huu wanafunzi waliopata daraja sifuri wameongezeka na kufikia 30 kutoka 15 kwa mwaka jana na kwamba hali hiyo imetokana na kuongezeka kwa idadi ya watahiniwa. Hata hivyo, Ayoub aliwasihi wanafunzi hao ambao hawajafaulu kutovunjika moyo kwa kuwa bado wana fursa ya kufanya tena na wakafanikiwa.

"Hapa nipende kuwatia moyo wale vijana wetu ambao kwa bahati mbaya hawakufanikiwa kupata matokeo mazuri. Niwaambie tu bado fursa wanayo warejee tena mitihani yao naamini watafanikiwa," alisema Ayoub.

Alisema kuwa serikali imeongeza fursa ya elimu kwa wananchi wake yenye lengo la kuhakikisha kila mmoja anafanikiwa kimaisha kutokana na kupata elimu, hivyo ni vyema wazazi kuendelea kuwashajihisha watoto wao katika kutafuta elimu kwa manufaa yao na jamii.

"Serikali inaendelea kutimiza wajibu wake wa kuimarisha sera ya elimu ikiwa pamoja na kuboresha miundombinu na kujenga majengo mbalimbali na vifaa kwa matumizi ya wanafunzi," alisema.

# Waziri apigia chapuo matumizi maktaba

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, ameitaka bodi mpya ya Shirika la Huduma za Maktaba kutumia mbinu mbadala kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kutumia huduma za maktaba ili kujiendeleza kitaaluma.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa bodi hiyo katika ukumbi wa Wizara ya Elimu, Mazizini Mjini Unguja, alisema baadhi ya wananchi hawana uelewa juu ya umuhimu wa huduma hizo, hivyo aliwashauri kutumia vyombo vya habari kurahisisha kupatikana uelewa huo.

Alisema elimu ni jambo muhimu katika maisha ya mwanadamu, hivyo kuendeleza majukumu yao ni vyema kusimamia vyema sera ya shirika hilo ili kuhakikisha jamii ya Wazanzibari wananufaika na huduma zao.

Pia aliwataka kushirikiana katika utendaji wa kazi zao pamoja na bodi iliyomaliza muda wake pale watapohitaji, ili kuleta ufanisi katika kuendeleza huduma za maktaba.

Naye Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, aliwashauri wajumbe hao kuunda mtandao maalum utakaowasaidia wanafunzi na vijana kupata huduma za maktaba kwa urahisi kwa kutumia simu za mkononi.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Dk. Idrissa Muslim Hija, aliipongeza bodi iliyomaliza muda wake kwa kazi nzuri iliyofanya.

Alisema tayari sera ya shirika hilo imeshafanyiwa kazi ambapo imani yake ni kutumiwa vyema ili kuwa na huduma za maktaba zinazoridhisha katika nchi.

Mwenyekiti wa bodi aliyemaliza muda wake, Fatma Kingwabwa, alisema katika uongozi wake shirika hilo limekuwa na matatizo mbalimbali ikiwamo kutokuwapo uhamasishaji juu ya matumizi ya maktaba ambapo walimu nao pia hawahamasishi wanafunzi kutumia maktaba, ukosefu wa usafiri ambapo ameahidi kuendelea kutoa ushirikiano kwa bodi mpya ili kusaidia kupunguza matatizo hayo. Pia Mwenyekiti mpya wa bodi hiyo, Yahya Idris Abdulwakil, alisema watajitahidi kushirikiana na wajumbe wake ili kuhakikisha wanatekeleza yale waliyotakiwa kuyafanya ili kuliendeleza Shirika la Huduma za Maktaba.

# Wakazi Moro wahimizwa kujiunga CHF

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

SERIKALI mkoani Morogoro imewataka wakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro Vijijini, kuchangamkia fursa ya kujiunga na Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii (CHF) iliyoboreshwa ili kuwarahisishia kupata huduma za afya kutokana na mazingira ya miundombinu kuwa magumu.

Ushauri huo ulitolewa na Mkuu wa Mkoa huo, Dk. Kebwe Stephen, wakati wa ufunguzi wa kampeni ya uhamasishaji wa kujiunga na uanachama wa bima ya afya katika Kata ya Ngerengere.

Alisema CHF iliyoboreshwa imekuwa mkombozi mkubwa hasa kwa wananchi wanaoishi maeneo ya vijijini kwa kuwa inawahakikishia wateja wake upatikanaji wa huduma bora za afya hata pale unapokuwa hauna fedha.

"Mazingira ya vijijini wote tunayajua, sio kila wakati una pesa na ugonjwa hauna siku maalumu, muda wote unakupata hivyo tujiunge na mfuko huu wa CHF iliyoboreshwa ili tunapoungua kutokana na mazingira yetu tunatafuta pesa ya nauli na kwenda katika vituo vya afya na hospitali," alisema.

"Ni vizuri sasa kama serikali ya kijiji kutoa elimu kwa kaya pamoja na kuitisha mikutano na kueleza juu ya umuhimu wa CHF iliyoboreshwa kwa gharama ya shilingi 30,000 kwa mwaka mzima, ili kuondokana na changamoto mbalimbali wakati wa upatikanaji wa huduma za afya," alisema mkuu huyo wa mkoa.

Meneja wa Mradi wa Health Promotion and System Strengthen ( HPSS ) wa Tuimarishe Afya unaofadhiliwa na Serikali ya Uswisi, Dk. Haruni Machibya, alisema wameamua kuanzisha kampeni hiyo kutokana na wilaya hiyo kuwa chini katika huduma ya afya.

# Teknolojia mbegu za kisasa yasambazwa

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo (TARI) Ilonga wilayani Kilosa mkoani Morogoro, imeanza kwa vitendo mkakati wake wa kusambaza teknolojia za mbegu za kisasa kwa wakulima ili waondokane na kilimo cha mazoea na kulima kisasa.

Hatua hiyo pia ina lengo la kuongeza kasi ya kupatikana kwa malighafi zinazotokana na kilimo zitumike kwenye uchumi wa viwanda.

Kupitia mpango huo TARI Ilonga kwa kutumia watafiti wake imewakusanya wataalamu wa kilimo na ugani kutoka kata zote za Wilaya ya Kilosa na kuwapa mafunzo maalumu ya teknolojia za mbegu za kisasa zilizozalishwa katika taasisi hiyo kwenda kuwaelezea na kuwafundisha wakulima kuanza kuzitumia katika msimu wa kilimo.

Akizungumza na wataalamu wa kilimo kutoka kata zote za Kilosa, Mkurugenzi wa TARI Ilonga, Dk. Joel Meriyo, alisema wameamua kuanza kupeleka teknolojia hizo kwa wakulima waliopo ukanda wa mikoa ya mashariki na kwa kuanzia waanzana na Kilosa.

Dk. Meriyo ambaye pia ni mtaalamu wa masuala ya udongo nchini, alisema kupitia mpango huo watafiti wa TARI Ilonga wamejiwekea malengo ya kufikia wakulima katika kata zote za Kilosa na kuwapa elimu ya kilimo bora na kutumia teknolojia za kisasa za mbegu.

"Hakuna sababu ya wakulima wa Mkoa wa Morogoro kuwa maskini, tumeanza mpango kabambe wa kuwafuata huko walipo na kuwafundisha matumizi ya teknolojia za mbegu za kisasa ambazo zinaongeza mavuno maradufu na zile walizozizoea ili kuwa na uhakika na usalama wa chakula," alisema Dk. Meriyo.

Naye Mratibu wa Utafiti Kanda ya Mashariki kutoka TARI Ilonga, Meshack Makenge, alisema jukumu kubwa kwao ni kuzalisha mbegu za teknolojia ya kisasa na kuzisambaza kwa wakulima ili waweze kufanya kilimo cha kisasa chenye tija.

Makenge ambaye ni mtafiti wa kitaifa wa mazao ya mikunde, alisema TARI Ilonga, imepewa jukumu la kuzalisha mbegu za teknolojia ya kisasa kwa mazao ya nafaka, mbegu za mafuta za aina zote za alizeti na pamba, mbegu za mazao ya mizizi pamoja na mazao ya mkundekunde ambazo tayari zimeshazalishwa.

Ofisa kilimo, umwagiliaji na ushirika wa Wilaya ya Kilosa, Elina Dastan, alisema mkakati wa wilaya hiyo katika msimu ujao wa kilimo ni kuongeza uzalishaji wa chakula na ziada ili kusaidia mpango wa serikali katika kuelekea uchumi wa viwanda hivyo mafunzo ya teknolojia hizo watayafikisha moja kwa moja kwa wakulima.




Meneja Mauzo wa Kampuni ya Mantrac Tanzania, Butwa Sanga (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu uzinduzi wa mashine mpya za katapila ambao unatarajiwa kufanyika leo. Kutoka kushoto ni Msimamizi wa Idara ya Vipuri wa kampuni hiyo, Matiko Bugumia, Gary Martin kutoka kampuni ya CAT ambao ndio watengenezaji wa katapila na Meneja Biashara wa Mantrac Kanda ya Afrika Mashariki, Moataz Taha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makandarasi wawezeshwa kwa mashine za teknolojia

**Na Beatrice Philemon**

WADAU wa sekta ya ujenzi wamewezeshwa baada ya Kampuni ya Mantrac Tanzania kuleta mashine zinazotumia teknolojia ya kisasa ili kurahisisha ufanyaji kazi wa shughuli za ujenzi.

Pia zitawasaidia makandarasi kupunguza gharama za matengenezo pamoja na kuwasaidia kukabidhi mradi kwa muda uliopangwa.

Hayo yalisemwa jana na Meneja Mauzo kutoka Kampuni ya Mantrac Tanzania, Butwa Sanga, alipokuwa akizindua mashine inayojulikana kama 'New Generation Cat Excavators-320GC, 320 na 323' kwa ajili ya wadau wa sekta ya ujenzi.

"Hii ni mashine ya kisasa yenye teknolojia mpya tofauti na mashine za zamani, mashine hizi zina uwezo wa kuonyesha ubebe mzigo kiasi gani bila kuwa na mtu mwingine au kuwa na msaada wa mtu mwingine," alisema.

Alisema mashine ya sasa itakuwa na kamera nje, vioo vya kumfanya mtu aweze kuona mbali au kama kuna mtu asiweze kumgonga mtu, na mashine hizi zitakuwa sokoni ili kuondoa mashine zenye muundo wa zamani ili kusaidia makandarasi kufanya kazi zao kwa ufanisi na kwa muda uliopangwa.

Kwa mkandarasi au wadau wa sekta ya ujenzi wanaotaka kutumia mashine hizi, tayari mashine hizi zipo nchini.

Alisema mkandarasi anayetaka kutumia mashine hizi, zinatumia screen kuangalia upande unaotaka kwenda au unapotaka kupita bila kuongozwa na mtu mwingine kwa sababu ina kamera mbele inayokuonyesha kila upande usilete madhara au kumgonga mtu.

Vile vile, mashine hizi zinatoa vipimo halisi ni kiasi gani unatakiwa kubeba au uzito gani wa mchana au mawe unayotakiwa kubeba tofauti na mashine za zamani ambazo hazikuwa rahisi kuona vipimo au uzito.

Kadhalika, mashine hizi zinamsaidia mmiliki kubana matumizi ya mafuta kwa asilimia 20, na kwa upande wa matengenezo gharama za kununua vipuri kwa ajili ya matengenezo zinapungua kwa asilimia 25.

Alisema mashine za zamani zilikuwa na vipuri vingi vya kufanyia matengenezo. Alisema waendesha mashine 30 kutoka sehemu mbalimbali nchini wameshapatiwa mafunzo bure jinsi ya kutumia mashine hizo. "Hivi sasa mtu yeyote anayetaka kununua mashine hizi tunatoa mafunzo bure jinsi ya kutumia mashine hizo na tayari vipuri vyake vinapatikana hapa nchini," alisema Sanga.

Naye Mtaalamu Mwandamizi kutoka Kampuni ya CAT- Dubai, Gary Martin, alisema kuwa hizi ni mashine nzuri kwa wadau wa sekta ya ujenzi kwa sababu inapunguza gharama za uendeshaji kwenye mafuta na matengenezo.

Alisema wameamua kuja na mashine hizi ambazo ni mpya baada ya kusikia sauti za wateja wao kutoka Tanzania na Mashariki ya Kati, na mashine hizi zina kila kitu ambacho mwendesha mashine anahitaji katika shughuli zake za ujenzi.

Alisema mashine zinapunguza gharama za uendeshaji na zimetengenezwa kwa ajili ya matumizi ya kizazi kipya. Alisema mwendesha mashine hizi anaweza kuona kitu gani kipo nyuma ya mashine au pembeni ya mashine.

Aliwaomba wadau wa sekta ya ujenzi kutumia mashine hizo ili kurahisisha ufanisi wao wa kazi kwa sababu mashine hizi zipo nchini na vipuri vyake vinapatikana nchini.

# HABARI KIMATAIFA

## Ajinadi EU kwa tabianchi

**BERLIN, Ujerumani**

WAZIRI wa Ulinzi wa Ujerumani, Ursula Von der Leyen, aliyeteuliwa kugombea urais wa Kamisheni ya Umoja wa Ulaya (EU), ameahidi kuimarisha utekelezaji wa matarajio wa umoja huo yahusuyo mabadiliko ya tabianchi.

Kura ya Bunge ilitarajiwa kupigwa jana jioni. Waziri huyo mshirika wa karibu wa Kansela wa Ujerumani, Angela Merkel, aliteuliwa na viongozi wa EU mwezi huu, kuchukua nafasi ya Rais wa sasa wa umoja huo, Jean-Claude Junker, kuanzia Novemba Mosi.

Uteuzi wake unatakiwa kuthibitishwa na wingi wa kutosha wa wabunge wa Bunge la EU. Hata hivyo, bunge hilo limegawanyika juu ya uteuzi wake, hivyo hata uthibitisho wake kwa kiasi kikubwa umegubikwa na sintofahamu.

Hata baada ya uteuzi wake wiki iliyopita, bado pande za Wasoshaliti na Maliberali ambao wanashika nafasi ya pili ya tatu ya kuwa na wingi wa wabunge wanaokiunga mkono chama cha siasa kali za mrengo wa kati cha EPP cha Von der Leyen, wanataka ufafanuzi zaidi kutoka kwa mwanamama huyo.

## Ukimya wa madai 60 ya udhalilishaji

**LONDON, Uingereza**

TAKRIBAN madai 60 ya udhalilishaji wa kingono yaliyofanyiwa uchunguzi na polisi kwa miaka miwili, hayakuripotiwa kwenye takwimu rasmi nchini Uingereza, BBC imebaini.

Takwimu za mwaka 2017 na 2018 hazikuhusisha makosa kama mawasiliano ya kingono na watoto. Kundi la watetezi wa haki za binadamu wanasema Wizara ya Ulinzi haiweki rekodi ya shutuma hizi ''ipasavyo au kwa usahihi''.

Wizara imesema imejiridhisha kuwa takwimu sahihi zilikuwa zimechapishwa. Ripoti imedai idadi ya vikosi vya Uingereza inajihusisha na vitendo vya ukandamizaji, unyanyapaa na ikiwamo udhalilishaji wa kingono.

Wizara imesema imepokea mapendekezo yote 36 ya ripoti kwa ajili ya kuondokana na changamoto hizo. BBC pia iliongea na ofisa wa polisi wa zamani anayeamini kuwa mfumo wa haki ndani ya wizara unakosa uzoefu wa kufanya uchunguzi kuhusu udhalilishaji wa kingono.

Elizabeth (jina la kubuni) alijiunga na jeshi. Ameiambia BBC kuwa amekuwa akidhalilishwa na mwanajeshi.

# ZUMA: Kuna njama kuniangamiza kisiasa

**CAPE TOWN, Afrika Kusini**

ALIYEKUWA Rais wa Afrika Kusini, Jacob Zuma, ameliambia jopo la mahakama linalochunguza madai ya rushwa dhidi yake kuwa "kuna njama" inayolenga kumwangamiza kisiasa.

Zuma alisema hayo alipofika mahakamani kwa mara ya kwanza, huku wafuasi wake wakimshangilia alipoingia katika jengo hilo.

Zuma, 77, alilazimishwa kujiuzulu urais Februari mwaka 2018 akituhumiwa kwa ufisadi.

Wakati akijitetea, Zuma alisema madai hayo ya ufisadi ni njama ambayo imekuwako kwa muda mrefu ili kumharibia jina, mpango ambao umetekelezwa na wasimamzi wa chama cha ANC ili kumwondoa kwenye siasa za Afrika Kusini.

Alipoulizwa ni kwa nini anatoa madai hayo, alisema wenye kumpiga vita walidhani alikuwa na habari dhidi ya watu fulani, ambazo zingewazuia kutwaa nafasi za juu katika chama hicho.

Nafasi yake ilichukuliwa na aliyekuwa makamu wake wakati huo, Cyril Ramaphosa, ambaye aliahidi kukabiliana vikali na suala la rushwa nchini humo baada ya kuchukua nafasi ya Zuma.

Ramaphosa alielezea utawala wa miaka tisa ya Zuma kama "kupoteza muda". Mashtaka dhidi ya Zuma yanaangazia uhusiano wake na familia inayokabiliwa na utata ya Gupta, ambayo inatuhumiwa kwa kutumia vibaya ukaribu wao na rais kuingilia uteuzi wa mawaziri na kujipatia kandarasi za serikali kwa njia za kifisadi.

Pia anakabiliwa na tuhuma ya kupokea rushwa kutoka kwa kampuni ya Bosasa, ambayo inamilikiwa na familia ya Watson. Zuma amekanusha madai hayo yote.

"Nimeonewa na kutuhumiwa kuwa mfalme wa watu wafisadi," Zuma aliliambia jopo hilo linaloongozwa na Jaji Ray Zondo.

"Watu wamenibandika majina yote na sijawahi kujibizana nao kuhusiana na suala hilo," aliongeza.

*BBC*



Wabunge Rashida Tlaib, Ayanna Pressley, Ilhan Omar na Alexandria Ocasio-Cortez wakijibu mashambulizi ya 'kibaguzi' yaliyotolewa na Rais wa Marekani Donald Trump. **PICHA BBC.**

# Wabunge wataka maneno ya Rais Trump yapuuzwe

**NEWYORK, Marekani**

WABUNGE wanne walioshambuliwa na Rais wa Marekani, Donald Trump, katika mfululizo wa maandishi ya tweeter yanayodaiwa kuwa ya ubaguzi, wamepuuza maneno ya rais huyo wakisema ni kujaribu kuwaondoa katika umakini wao.

Wawakilishi hao, Alexandria Ocasio-Cortez, Ilhan Omar, Ayanna Pressley na Rashida Tlaib wamewataka watu wa Marekani kwenye mkutano wa waandishi wa habari "kutoyatilia maanani" maneno ya Rais Trump.

Trump alisema wanawake hao wanne waondoke nchini humo, na alitetea kauli zake na kukataa shutuma kuwa ni mbaguzi.

Wakizungumza na waandishi wa habari wanawake hao walisema, hivi sasa watu waweke akili zao kwenye sera za Marekani na si maneno ya Trump.

Ijumaa, wabunge hao walitoa ushuhuda mbele ya wabunge kuhusu hali za wahamiaji wanaoshikiliwa kwenye vituo ambavyo walivitembelea.

Wabunge wa Democrat kwa kiasi kikubwa wameushutumu utawala wa Trump hasa namna anavyodhibiti mpaka, wakisema wanawashikilia wahamiaji ambao sasa wana hali mbaya.

Trump aliwatetea maofisa wake mpakani. Utawala wake ulitangaza sheria mpya iliyoanza kutumika jana, inayokataa kutoa hifadhi kwa mtu yeyote anayevuka mpaka wa kusini ambaye hajaomba kupatiwa hifadhi kwenye "nchi ya tatu".

Baada ya ushuhuda huo Trump alitetea kuwa hali ya kituo imekuwa "ikishughulikiwa". Kisha akatuma mfululizo ujumbe wa twitter kuhusu wabunge hao.

"Kama huna furaha, ikiwa unalalamika kila kitu unaweza kuondoka," aliwaambia waandishi wa habari nje ya Ikulu.

Wakati wanawake hao walipokuwa wakiongea na waandishi Jumatatu, Trump aliandika tena ujumbe wa tweeter.

"Kama hauna furaha hapa, unaweza kuondoka! Ni uamuzi wako, ni uamuzi wako mwenyewe. Hii ni kuhusu mapenzi kwa Marekani," aliandika.

*BBC*

# HESLB yawafuata wakopaji jeshini

INATOKA UK. 3

ya kuomba kwa kutumia mtandao wetu ambao upo wazi hadi Agosti 15 na tunaruhusu maswali kutoka kwao na kuyajibu papo hapo," alisema.

Akizungumza baada ya mkutano huo, mwanafunzi Ngatowana Ndakwila Kiwanga, aliishukuru serikali na HESLB kwa kuandaa utaratibu wa kutembelea kambi za JKT na kuwaelimisha wanafunzi ili wawasilishe maombi kwa usahihi na hatimaye kutimiza ndoto zao za elimu.

"Mimi nimepata daraja la kwanza la pointi saba na nilikuwa nasoma HKL (Historia, Kiswahili na Kiingereza) na ingawa sijaomba hadi sasa, nitaomba na ninaamini nitapata mkopo na nitakuwa mwanasheria," alisema mwanafunzi mwenye ulemavu aliyemaliza kidato cha sita mwaka huu katika Shule ya Sekondari ya Benjamin Mkapa.

Mkurugenzi wa Utoaji Mikopo wa HESLB, Dk. Veronika Nyahende, alisema matarajio ya HESLB kwa mwaka huu ni kuona idadi ya wanafunzi wanaokosea kujaza fomu za maombi inapungua kwa kiasi kikubwa.

"Pamoja na elimu ya maelezo ya mdomo, tumewapa kitabu kidogo cha lugha ya Kiswahili chenye maswali na majibu kuhusu utaratibu mzima wa uombaji mikopo kwa lugha nyepesi... tunawasihi wasome na kuzingatia maelezo yote muhimu," alisema.

Mkuu wa Kikosi cha Jeshi hilo yenye kambi hiyo ya vijana takribani 3,000, Luteni Kanali Alex Malenda, alishukuru utaratibu ulioandaliwa na kueleza unastahili kupongezwa kwa kuwa utasaidia kupunguza muda unaotumika na wanafunzi kukamilisha maombi kwa kuwa wanakuwa hawajui mambo mengi.

HESLB ilianza kupokea maombi ya mkopo kwa njia ya mtandao Julai mosi na inatarajia kufunga Agosti 15, ili kuruhusu kazi ya uchambuzi wa maombi yaliyopokelewa na hatimaye kutoa mikopo kwa wanafunzi wenye sifa ifikapo mwishoni mwa mwezi Oktoba, mwaka huu.

# Mahabusi amlipua ofisa Magereza mbele ya JPM

INATOKA UK. 2

Mahabusi huyo alisema huku akikatisha maelezo yake na kuketi akiwa ameweka mikono kichwani.

Kutokana na maelezo ya mahabusi huyo, Rais Magufuli alilazimika kumhoji Ofisa Usalama wa gereza hilo ambaye alisema anatimiza wajibu wake vizuri na alishafanya ukaguzi na kuchukua vitu vyote visivyotakiwa kuingia gerezani, zikiwamo simu za mkononi.

Alisema alikusanya simu nne ambazo amezihifadhi Ofisi ya Mkuu wa Gereza na kwamba kazi hiyo amekuwa akiifanya kila siku asubuhi.

Ofisa huyo alijitetea kuwa mahabusi huyo aliamua kueleza mambo ya gereza hilo kwa kutaka kusikilizwa na Rais Magufuli.

Sehemu ya mahojiano ya Rais Magufuli na ofisa huyo ilikuwa hivi:

**Ofisa:** Huyu amesema kwa sababu ni miongoni mwa watu, wanaotaka asikilizwe yeye tu, anakuja na vitu viovu.

**Rais Magufuli:** Wewe hukutaka nimsikilize? Mbona wewe nimekusikiliza?

**Ofisa:** Namshukuru Mungu kwa kufanya hivyo, ameeleza ukweli, ameninua kwa kiasi fulani.

**Rais Magufuli**: Umejuaje kama amekuinua, nikikung'oa nyota zako hapo atakuwa amekuinua?

**Ofisa:** Kwamba mimi nafanya... (alikatishwa na Rais)

**Rais Magufuli:** Halafu wewe naona una kiburi.

**Ofisa:** Hapana mkuu.

**Rais Magufuli:** Unazungumza mbele yangu kuwa huyu amekuinua?

**Ofisa:** Kwamba nimesikika.

**Rais Magufuli:** Una uhakika gani mimi nitatoka na jibu gani kwako? Yaani unazungumza hivyo mbele yangu?

**Ofisa:** Nimekosa mkuu.

Rais Magufuli: Kwa hiyo, kuja kwangu hapa ilikuwa ni ili wewe uinuliwe?

**Ofisa:** Hapana mkuu.

**Rais Magufuli:** Amekuinua!

**Ofisa:** Niwie radhi mkuu.

**Rais Magufuli:** Mkuu wa Gereza... (aliita Rais Magufuli). Mimi nilikuja hapa kusudi huyu ainuliwe?

**Ofisa:** Nisamehe mheshimiwa.

**Ofisa:** Nisamehe afande.

**Rais Magufuli:** Eeeh! Nafikiri unajua nafanya mzaha.

Awali, Rais Magufuli alisema anafahamu katika gereza hilo kuna simu nyingi, dawa za kulevya aina ya bangi na mali nyingine ambazo zinaingia katika gereza hilo, huku akiahidi kuzifanyia kazi changamoto zinazowakabili askari magereza na wafungwa nchini.

**'HATA MIMI MFUNGWA MTARAJIWA'**

Hashim Kijuu, diwani mstaafu wa Kata ya Mbugani, alimweleza Rais Magufuli kuwa wafungwa na mahabusi wengi wamebambikwa kesi.

"Ninaomba mvumilie, hata mimi, hata sisi tuliopo hapa ni wafungwa au mahabusi wa baadaye, kufungwa au kuwa mahabusi, haina maana wewe kutopata haki yako ya utu wa binadamu, ndiyo sababu nimepita hapa leo," alisema Rais.

Kurwa Hemeli, mahabusi katika gereza hilo, alimweleza Rais Magufuli kuwa alikamatwa na mafuta ya dizeli madumu 16, akapelekwa Kituo cha Polisi Nyegezi ambako aliambiwa alipe Sh. milioni moja, lakini akawa na uwezo wa kulipa Sh. 200,000.

Alidai Sh. 200,000 zake zilikataliwa na kwamba askari walimpeleka kituo kikuu cha polisi ambako aliunganishwa na watuhumiwa wengine kwa kosa la mauaji.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya TPB, Sabasaba Moshingi (wa pili kulia), akipata maelezo kutoka kwa Mkuu wa Gereza la Mahabusu la Sumbawanga, Philemon Mrutu, kuhusu ujenzi wa mahabusu ya mkoa huo, kabla ya benki hiyo kukabidhi mifuko ya saruji 200 kusaidia ujenzi huo, mjini Sumbawanga wikiendi. Kushoto ni Kaimu Ofisa Magereza wa mkoa huo, George Millega na (kulia) ni Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Joachim Wangabo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mchungaji matatani tuhuma za kubaka, kumpa ujauzito bintiye

INATOKA UK. 3

mapenzi hadi kumpatia ujauzito.

Alisema Jeshi la Polisi lilipata taarifa kutoka kwa raia wema juu ya mchungaji huyo kumbaka mtoto wake na kumpa ujawauzito na kumsababishia kuacha masomo.

Kwa mujibu wa kamanda huyo, baada ya polisi kupata taarifa hizo, ndipo juzi walimkamata na kumweka chini ya ulinzi.

Kamanda Kuzaga alisema mtuhumiwa bado anaendelea kushikiliwa na polisi na anatarajiwa kufikishwa mahakamani ili kujibu tuhuma zinazomkabili.

Katika tukio lingine, Kamanda Kuzaga alisema walimu wawili wa Shule ya Msingi Kambuzi wilayani Mpanda wanashikiliwa kwa tuhuma za kubaka kwa nyakati tofauti na kumpa mimba mwanafunzi mwenye umri wa miaka 16 (jina linahifadhiwa).

Aliwaja watuhumiwa hao kuwa ni Ambukile Mwakapala (30) na John Ndenje (35) ambao wanatuhumiwa kufanyia mwanafunzi kitendo hicho.

Kuzaga alisema watuhumiwa wote wawili walikamatwa Julai 10, mwaka huu katika kijiji cha Kambuzi majira ya saa 5:00 asubuhi baada ya taarifa za kubakwa kwa mwanafunzi huyo kuwa zimefika kituo cha polisi.

Alisema watuhumiwa wote wawili wanashikiliwa na polisi na baada ya upelelezi kukamilika, watafikishwa mahakamani kujibu tuhuma dhidi yao.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## ELIMU/ MASOMO

**NAFASI ZA MASOMO,** Chuo cha Uuguzi na Ukunga MASSANA kilichopo dar es Salaam, Mbezi Beach Goba Road. Kinatangaza nafasi za masomo kwa ngazi ya Diploma na cheti yatakayoanza mwezi wa September 2019. Njoo tukujazie Form Kupitia Mtandao wa Nacte: 0713 321260/0769 666880

## VIWANJA/MASHAMBA

**VIWANJA VINAUZWA,** Viwanja Vinauzwa Kibaha Visiga, ukubwa ni mita 20 kwa 20 bei ni millioni moja tuu(1,000,000/=) unaweza kulipa kwa awamu ndani ya miezi mitatu. Huduma zote zipo. Mawasiliano: 0714 090008 au 0767 090008

**PLOT NA NYUMBA VINAUZWA**

Ploti na nyumba vinauzwa mtoni kijichi wilaya ya temeke. Ploti ni mbili kwa moja ni nzuri na kubwa saana kwa matumizi yote ya kibiashara na makazi. Mawasiliano: 0688 640101


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI


## VIWANJA VINAUZWA

Viwanja vifuatavyo ambavyo vipo kwenye eneo moja na vina Hati Halali vyenye jumla ya Mita za **mraba 12,169 vinauzwa.**

Ukubwa wa viwanja hivyo 4 ni kama ifuatavyo:-

1. **2,760 sqm**
2. **2,406 sqm**
3. **3,564 sqm**
4. **3,439 sqm**

Viwanja vipo eneo la Mbezi, Halmashauri ya Kinondoni.

**Kwa taarifa zaidi tafadhali wasiliana na namba +255 655 131 074**

615326202

## CHETI KIMEPOTEA




**BAZIL SAFARI NDEGE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2354/0010** kilichotolewa na **EAGLES SEKONDARI** mwaka 2011.

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.**

**Taarifa ya polisi: DAR/OST/RB/135801/2019.**

115325702

## KUPOTEA KWA CHETI



**Emanuel kabeya** anatangaza kupotea kwa vyeti vifuatavyo cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.1162/0039** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la taifa mwaka 2010 katika shule ya Sekondari Igurubi, Cheti cha kidato cha sita chenye **index namba S.0132/0611** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2013 katika shule ya Sekondari Milambo. Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa: **DOM/RB/9099/2017**

115325202


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz , au

piga simu: 0767 223311

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako la

Nipashe kila siku

NJOO UTANGAZE

BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.

E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# GWIJI

## ARSENAL ATAKA OZIL AUZWE

**LONDON, England**

GWIJI wa Arsenal, Marc Overmars amesisitiza kwamba klabu yake hiyo ya zamani inatakiwa kumuuza Mesut Ozil kipindi hiki cha majira ya joto ili kumnunua Hakim Ziyech kutoka Ajax.

Overmars kwa sasa ni mkurugenzi wa ufundi katika klabu ya Ajax, lakini anahisi kwamba washikabunduki hao watanufaika zaidi na huduma ya Ziyech kama wakimnunua.

Kiwango cha nyota huyo wa kimataifa wa Morocco, msimu uliopita kilikuwa bora zaidi kwake wakati Ajax ikitinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na thamani yake inatajwa kuwa ni pauni milioni 31.5.

"Hadi sasa nashangaa kwanini hawamfuati Hakim," alisema Overmars akinukuliwa na televisheni ya Voetbal.

"Nafikiri amecheza vizuri zaidi kila mwaka na takwimu zake ni nzuri. Klabu nyingi ssa zimeongezeka kumwania.

"Nafikiri Arsenal wangemuuza Ozil ili wamsajili Ziyech kwa sababu yeye ni bora kuliko Mesut Ozil.

"Niliwaambia muuzeni yeye (Ozil) na mtampata Hakim kwa nusu bei. Lakini wao (Arsenal) hawanisikilizi mimi. Hivyo, ataendelea kubakia hapa Ajax."

Ziyech amekuwa akihusishwa na mpango wa kutakiwa na klabu nyingi Ulaya kipindi hiki cha majira ya joto.

# EVERTON YAMSAJILI DELPH CITY

**LIVERPOOL, England**

KLABU ya Everton imetangaza kumsajili kiungo, Fabian Delph kutoka Manchester City kwa mkataba wa miaka mitatu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 29, ambaye alijiunga na City akitokea Aston Villa mwaka 2015, amesaini kwa ada ya awali ya pauni milioni 8.5 na baadaye watamaliziwa pauni milioni 1.5.

Mara baada ya kusajiliwa hapo ameiambia tovuti ya Everton kwamba: "Kila wakati nilipokuwa nikicheza dhidi ya Everton, iwe ugenini au nyumbani, kitu cha kwanza kwenye akili yangu ni hisia za mashabiki wake.


"Maana mashabiki wake wanaipenda klabu yao na wana molari kubwa na wachezaji wanapokuwa dimbani na hilo limekuwa likinivutia mno na najisikia fahari kuwa hapa."

Delph aliongeza: Nina furaha kubwa kukamilisha usajili huu, kwa hakika nitajitolea kwa hali na mali kuisaidia timu hii.

"Matumaini yangu ni kwamba nitapata mafanikio makubwa na timu hii yenye mashabiki bora pamoja na wachezaji, nitafanya kitu maalumu kwao."

Delph alikuwa sehemu ya kikosi cha City kilichotwaa mara mbili mfululizo taji la Ligi Kuu England na kocha wa Everton, Marco Silva ana matumaini dhidi yake makubwa.

"Wakati nikiangalia aina ya wachezaji ninaotakiwa kuwaleta hapa kwenye kikosi, napenda zaidi wale wenye uzoefu na ubora dimbani. Na Delph ni mmoja wao," alisema Silva.



# Mtoto wa Zidane asajiliwa Ureno

**LISBON, Ureno**

MTOTO wa kocha wa Real Madrid, Zinedine Zidane, Enzo Zidane amejiunga na klabu ya Desportivo das Aves ya nchini Ureno baada ya kuachiwa na Lausanne.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 awali alikuwa akiwaniwa na wapinzani wa Aves, timu ya Vitoria de Guimaraes kabla ya kuzidiwa kete.

Klabu hiyo ilitangaza ujio wa Enzo kwa kuposti video katika ukurasa wake wa mtando wa kijamii wa Twitter Jumatatu.

Msimu uliopita Enzo alicheza mechi 34 wakati akiwa kwa mkopo kule Rayo Majadahonda iliyopo Ligi Daraja la Pili nchini Hispania.

Enzo alikulia kwenye akademi ya Juventus kabla ya kujiunga na Real Madrid mwaka 2004.

Aliichezea Real Madrid katika ngazi mbalimbali za timu ya vijana, kabla ya kuingizwa timu B na baadaye akacheza kwenye timu ya kwanza dhidi ya Cultural Leonesa mwaka 2016, katika mchezo ambao alifunga bao.

Enzo aliondoka Real kwenda Alaves mwaka 2017, na alicheza mara mbili kwenye La Liga kabla ya kwenda Lausanne.

Zidane ana watoto wengine watatu wanaocheza soka.

Luca mwenye umri wa miaka 21 ni golikipa na ameichezea Real Madrid mara mbili, kwa sasa anacheza kwa mkopo Racing Santander.

Wakati huo huo, Theo mwenye umri wa miaka 17 anacheza nafasi ya kiungo na Elyaz mwenye umri wa miaka 13 anacheza nafasi ya beki katika timu ya vijana ya Real Madrid.



## HABARI MICHEZO



# DE GEA

## KUTIA SAINI MKATABA UNITED - SOLSKJAER

**PERTH, Australia**

OLE Gunnar Solskjaer amethibitisha kwamba, David De Gea yupo kwenye nafasi nzuri ya kutia saini mkataba na Manchester United.

Mchezaji huyo raia wa Hispania anakaribia kukubali kusaini mkataba wa miaka mitano ambao utamfanya alipwe pauni 375,000 kwa wiki na Solskjaer ana matumaini kuwa dili hilo litatangazwa hivi karibuni.

"Tuna tumaini kufikia makubaliano na David kama nilivyosema mara nyingi," amesema Solskjaer akiwaambiwa waandishi wa habari kwenye uwanja wa kriketi wa Waca juzi Jumanne.

"Hilo litakuwa juu ya David na klabu kutangaza wakati jambo hilo litakapokuwa tayari."

De Gea alikaa nje wakati United ikiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Perth Glory Jumamosi na leo Jumatano atakuwa dimbani kucheza na Leeds United kwenye uwanja wa Optus.

Solskjaer pia anatarajia Romelu Lukaku kuwa fiti kwa ajili ya mchezo wa pili wa kipindi hiki cha maandalizi ya msimu mpya wa Ligi Kuu England.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji, ambaye amekuwa akihusishwa na mpango wa kutua kwa miamba wa Ligi Kuu Italia, Inter Milan, aliukosa mchezo dhidi ya Perth Glory kutokana na majeruhi, lakini alifanya mazoezi na timu hiyo Jumatatu tayari kwa ajili ya mchezo dhidi ya Leeds.

Eric Bailly na Victor Lindelof pia wanaweza kuwa fiti baada ya kuukosa mchezo dhidi ya Perth.

Luke Shaw aliumia misuli ya nyama za paja na anaweza kuwa fiti kwa ajili ya mchezo wa leo Jumatano.

"Wote tulikuwa kwenye mazoezi, na hakuna yeyote aliyekosekana, wachezaji wote 24 pamoja na magolikipa," alisema Solskjaer.

"Lee Grant bado hayupo fiti na pengine. Rom yuko fiti. Luke alifanya mazoezi Jumatatu, lakini sidhani kama atacheza mchezo ujao."

Lukaku amesafiri kwenda Australia na United licha ya kuhusishwa na mpango wa kutakiwa na kocha, Antonio Conte pale Inter Milan.

Miamba hao wa Serie A bado hawajawasilisha ofa maalumu kwa ajili ya kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 na Solskjaer anajiamini kwamba mchezaji huyo wa zamani wa Everton atabakia hapo Old Trafford msimu ujao.

"Siku tukapoanza msimu mpya nina uhakika kila mmoja atakuwapo kwenye kikosi na kila kitu kitakuwa sawa," alisema Solskjaer.

"Tunataka kuwa na timu imara pamoja na wachezaji ambao wataisaidia klabu yetu kwa ajili ya msimu ujao."

## JUVENTUS YAMALIZANA NA MATTHIJS DE LIGT

**ROME, Italia**

KLABU ya Juventus imefikia makubaliano ya kumsajili Matthijs de Ligt kutoka Ajax kwa ada ya pauni milioni 67.5, kwa mujibu wa Sky Sports.

Miamba hao wa Italia wamefikia makubaliano na wakala wa beki huyo wa Uholanzi, Mino Raiola na jana alitarajiwa kuwasili mjini Turin kwa ajili ya kufanyiwa vipimo vya afya.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19 ameripotiwa kwamba, atasaini mkataba wa miaka mitano wenye thamani ya pauni milioni 10.8 kwa mwaka.

Wiki iliyopita De Ligt aliondoka kwenye kikosi cha Ajax kilichokuwa kinasafiri kwenda Austria kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya wa Ligi.

Nyota huyo amekuwa akiwania na klabu kadhaa za Ulaya zikiwamo Manchester United na Barcelona, lakini Juventus imeshinda kwenye mbio za kuwania saini yake.



## WAKALA AKATAA BALE KWENDA SPURS

**MADRID, Hispania**

MPANGO kwamba Gareth Bale anaweza kurudi Tottenham kipindi hiki cha majira ya joto zimepuuziwa na wakala wa mchezaji huyo, Jonathan Barnett.

"Hakuna kilichobadilika," amesema wakala wa Bale akinukuliwa na gazeti la Daily Mail la Uingereza baada ya gazeti la Marca la Hispania kuripoti juzi kwamba mchezaji huyo anarudi jijini London.

"Bale hatakwenda Tottenham yeye bado ni mchezaji wa Real Madrid na hakuna kilichobadilika hadi sasa, huo ndio ukweli uliopo."

Mchezaji huyo ambaye jana alisherehekea kutimiza umri wa miaka 30 nchini Canada bado anataka kuendelea kuichezea klabu hiyo ambapo amebakiwa na miaka mitatu kwenye mkataba wake.

Kushindwa kwa Bale kusajiliwa na klabu nyingi ni kutokana na mshahara wake, kwani hadi sasa hakuna klabu ambayo imefikia mwafaka wa kuweza kumlipa mshahara wa pauni milioni 17 kwa mwaka.

Licha ya kocha, Zinedine Zidane kutaka Bale auzwe kwani hayupo kwenye mipango yake, lakini Rais wa Real Madrid, Florentino Perez, ambaye alizungumza na mchezaji huyo Jumatatu amebainisha kwamba ana furaha na mchezaji huyo.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# NEYMAR ASISITIZA KUONDOKA PSG

Mshambuliaji huyo Mbrazil afunguka alipokuwa akizungumza na bosi...

**PARIS, Ufaransa**

NEYMAR ameiambia Paris Saint-Germain kuwa anataka kuondoka klabuni hapo, taarifa za Sky Sports zimeeleza.

Mchezaji huyo nyota kutoka Brazil aliingia katika mgogoro na klabu yake hiyo baada ya kuchelewa kuripoti katika muda uliopangwa kwa kuanza maandalizi ya msimu mpya, lakini hatimaye Jumatatu wiki hii amejiunga na kikosi cha timu hiyo.

Vile vile imeelezwa kuwa mshambuliaji huyo ametumia muda wake kufanya mazungumzo na Mkurugenzi wa Michezo wa PSG, Leonardo kuhusu hatima yake.

Sky Sports imeandika kuwa PSG ilijaribu kumshawishi mshambuliaji huyo kubadilisha uamuzi wake wa kutaka kuondoka klabuni hapo, lakini Neymar hakuwa tayari kukubali na pia kuweka wazi anataka kuelekea katika klabu gani.

Barcelona inatajwa kuwa ndiyo klabu inayoongoza katika mchakato wa kumwania Neymar, ingawa usajili walioufanya wa Mfaransa Antoine Griezmann wa pauni milioni 108, unaweza kufanya mbio za kumrejesha Mbrazil huyo zikamalizika.

Leonardo alikiri kuwa mapema wiki hii kulikuwa na mazungumzo kuhusiana na makubaliano binafsi kati ya Barcelona na mchezaji huyo kuhusu uhamisho, lakini inaonekana kama wanaweza kukutana na kikwazo cha kufikia mapendekezo ya kufanikisha usajili huo.

Klabu hiyo ya Katalunya ilikubali kumsajili Mfaransa huyo kwa kuweka kipengele cha mkopo wa pauni milioni 31.5 ikimjumuisha Neymar kuwa sehemu ya usajili huo.

Miaka mwili iliyopita, Neymar aliondoka Barcelona kwa dau lililoweka rekodi ya dunia la pauni milioni 198, lakini sasa ameweka wazi kwamba anataka kurejea klabuni hapo.

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 27, alikosa nafasi ya kuisaidia Brazil katika kampeni za kuwania ubingwa wa Copa America ambalo ilichukua kutokana na kuwa majeruhi, lakini sasa amerejea kibaruani na kuanza maandalizi ya msimu mpya. Mvurugano uliingia katika hatua nyingine Jumatatu wakati wa mahojiano, ambapo Neymar alirekodiwa akizungumza na chombo cha habari cha Brazil, lakini mahojiano hayo yaliibwa.

Mahojiano hayo yalitakiwa yazungumzie kuhusu hatima yake hapo PSG, hata hivyo aliweka wazi kile ambacho anakitaka kuhusu hatima yake.

## KWA UFUPI

**SPURS YAJITOSA KWA BALE**

TOTTENHAM imesema iko tayari kuilipa Real Madrid kiasi cha pauni milioni 54 ili kumsajili mshambuliaji wake wa zamani, Gareth Bale (30), lakini Spurs imewaeleza vigogo hao wa Hispania haina uwezo wa kumlipa nyota huyo wa Wales mshahara wa pauni 600,000 kwa wiki. ***(Marca, via Express)***

**NEYMAR ASISITIZA KUONDOKA**

MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain na Timu ya Taifa ya Brazil, Neymar (27), amezungumza kwa mara nyingine na Mkurugenzi wa Michezo wa timu hiyo, Leonardo kumweleza nia yake ya kutaka kuondoka klabuni hapo. ***(ESPN)***

**NEWCASTLE KULIPA FIDIA**

NEWCASTLE United itailipa Sheffield Wednesday pauni milioni 4 kama fidia ya kumchukua kocha wake wa zamani, Steve Bruce, ambaye anajiandaa kutangazwa kuwa mwalimu mpya wa Magpies. ***(Sun)***

**SHEFFIELD YAIBOMOA NEWCASTLE**

WALIOKUWA wasaidizi wa Steve Bruce katika kikosi cha Newcastle United, Steve Agnew na Stephen Clemence, nao pia wanatarajiwa kuondoka Sheffield Wednesday na kujiunga na kocha huyo kwenye klabu mpya ya St James' Park. ***(Newcastle Chronicle)***

**FERNANDES AKARIBIA UNITED**

MANCHESTER United inatarajia kuwasilisha ofa rasmi ya kumwania kiungo wa Sporting Lisbon na Timu ya Taifa ya Ureno, Bruno Fernandes (24), ndani ya muda wa wiki tatu. ***(Independent)***

**ALDERWEIRELD ANUKIA ROMA**

MKURUGENZI wa Roma, Gianluca Petrachi, amethibitisha kuwa klabu yake inataka kumsajili beki wa Tottenham na Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Toby Alderweireld, ambaye ana umri wa miaka 30. ***(Football Italia)***

**ALDERWEIRELD, ERIKSEN KAMBINI**

BEKI Toby Alderweireld na kiungo raia wa Denmark, Christian Eriksen (27), wanatarajia kusafiri na kikosi cha Spurs leo kuelekea Singapore kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya, licha ya kutofahamu hatima yao. ***(Evening Standard)***

**BAYERN YAKOMAA NA SANE**

BAYERN Munich inajipa matumaini kuwa itakamilisha mchakato wa kumsajili winga wa Manchester City Mjerumani Leroy Sane (23), kwa dau la pauni milioni 100 katika kipindi hiki cha majira ya joto. ***(Sky Germany, via Mail)***

**ARSENAL, CELTIC KUTETA**

ARSENAL bado wanatarajia kufanya mazungumzo na Celtic kwa ajili ya kumnasa beki wa kushoto wa timu hiyo ambaye ni raia wa Scotland, Kieran Tierney (22), baada ya ofa yao ya pili kukataliwa kutokana na kuamini nyota huyo thamani yake itakuwa ni pauni milioni 25. ***(Evening Standard)***

**OZIL AIKWAMISHA ARSENAL**

ARSENAL itamkosa kiungo mchezeshaji wa Lyon na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Nabil Fekir (25), kwa sababu imeshindwa kuachana na kiungo wa zamani wa Ujerumani, Mesut Ozil, ambaye ana umri wa miaka 30. ***(L'Equipe, via Sun)***

**UNITED YAIKATALIA INTER**

INTER Milan ina wasiwasi wa kulipa ada ya pauni milioni 75 kwa mkupuo ili kumsajili straika wa Manchester United Mbelgiji Romelu Lukaku (26). Inter waliomba kumnasa nyota huyo kwa mkopo wa miaka miwili, ambapo pia watakuwa wanalipa ada kwa awamu tatu, lakini United wameweka wazi wanataka kulipwa dau hilo mara moja. ***(Star)***

**LINDELOF AICHAGUA UNITED**

BEKI wa Timu ya Taifa ya Sweden, Victor Lindelof (24), amesema kuwa atakuwa na furaha zaidi endapo atakuwa mchezaji wa Manchester United, licha ya wakala wake kusema kwamba anatakiwa na Barcelona. ***(Mirror)***

HABARI MICHEZO

# MJINI UNGUJA WAPITISHA KATIBA MPYA 'KINYONGE'

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MKUTANO Mkuu wa Chama cha Soka Wilaya ya Mjini Unguja umepitisha katiba mpya, lakini wajumbe wake wa mkutano huo wamesema kuwa wanahitaji "huruma" kutokana na kipengele cha kiwango cha elimu wanachotakiwa kuwa nacho wagombea wa nafasi nne za juu za uongozi.

Katiba mpya inataka mgombea wa nafasi ya uenyekiti, makamu mwenyekiti, katibu mkuu, katibu msaidizi na mweka hazina wawe na kiwango cha kuanzia kidato cha nne.

Awali wajumbe hao walikataa kuipitisha katiba hiyo kutokana na kutoridhika na kiwango cha elimu cha kidato cha nne ambacho kimetajwa kwenye katiba hiyo mpya.

Hata hivyo, katiba mkutano uliofanyika jana, wajumbe hao kwa kauli moja walikubaliana kuipitisha katiba hiyo mpya ambayo itatoa nafasi kwa shughuli nyingine za chama chao kuendelea.

Akizungumza mbele ya Rais wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Seif Kombo Pandu, ambaye ndiye aliitisha mkutano huo kwa mara ya pili, kwa niaba ya wenzake, Ramadhani Suleiman, alisema kuwa walikubali kupitisha katiba lakini wakatoa angalizo la kufuatwa kwa katiba "mama" ya nchi inayosema kiwango cha elimu cha mgombea wa nafasi yoyote ni kujua kusoma na kuandika.

"Tunaipitisha kwa vile ndio lishaharibika, lakini tunachoomba hiki kiwango cha elimu kiwe huru na kisiwe na masharti," alisema Suleiman, ambaye ni Katibu wa Timu ya West Coast.

Suleiman alisema kuwa wanafahamu uongozi wao unataka mabadiliko lakini mabadiliko ya aina hiyo yanataka muda na si "kukurupuka".

Alisema pia suala la elimu ni muhimu lakini linataka kujengewa taaluma na kutoa nafasi kwa viongozi wa vilabu kupatiwa elimu ili kuongeza uzoefu na kufanya kazi zao kwa weledi.

"Bado hatujawa na taaluma kubwa kuhusu hilo, kwa hiyo tunataka twende taratibu na tunafanya hivi kwa kuilinda kada yetu," Suleiman alisema.

Mapema Rais Pandu aliwataka wajumbe hao kukubaliana na mabadiliko kwa mustakabali wa soka la Zanzibar.

Alieleza kuwa wilaya hiyo ndio wilaya "mama" kisoka visiwani hapa na haitawezekana kuona wilaya nyingine zinacheza mpira isipokuwa Wilaya ya Mjini.




Mkurugenzi wa Maendeleo wa Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA), Vivian Shalua (kushoto), akizungumza kuhusu maandalizi ya onyesho la vazi la kitenge litakalofanyika Jumamosi kwenye Viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam. Wa pili kushoto ni Rais wa Shirikisho la Sanaa za Ufundi nchini, Adrian Nyangamalle na mbunifu wa mavazi, Ally Rehmtullah. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Mwakyembe mgeni onyesho la vitenge

**Na Shufaa Lyimo**

WAZIRI wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, anatarajia kushiriki katika onyesho maalumu la mavazi ya vitenge litakalofanyika Jumamosi kwenye Viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam, imeelezwa.

Onyesho hilo litakaloshirikisha wanamitindo zaidi ya 40, limeandaliwa na mbunifu wa mavazi hapa nchini, Ally Rehmtullah kwa kushirikiana na Kampuni ya Hightech Wear na Flygle ya China.

Akizungumza jana jijini, Rehmtullah, alisema lengo la onyesho hilo ni kuitangaza nchi kwenye vazi la kitenge na pia kudumisha ushirikiano baina ya Tanzania na China pamoja na kutangaza biashara ya mavazi.

"Hili ni onyesho litakalo wajumuisha wanamitindo takribani 40 watakaonyesha mavazi mbalimbali ya vitenge, tumeamua kushirikiana na kampuni ya "JININGA" katika kuandaa onyesho hili la vazi la kitenge kutokana na kampuni hii kuwa msambazaji mkuu wa aina hiyo ya nguo hapa nchini Tanzania na Afrika kwa ujumla," alisema Rehmtullah.

Alisema ili kuimarisha ushirikiano na wadau mbalimbali wa ndani na nje na nchi katika masuala ya ubunifu wa mavazi, mitindo na ushonaji, kampuni yake itashirikiana na kampuni hiyo kutengeneza nguo kutoka China.

"Kampuni yetu inaamini kuwa kupitia onyesho hili, hamasa itaongezeka kwa kuwa kila washiriki kuanzia washonaji, wanamitindo, watengenezaji wa vitenge kutoka China, na hadhira ya kariba mbalimbali, wataongea na vyombo vya habari kuhusu vivutio tulivyonavyo na umahiri wa Watanzania kuhusu ubunifu wa mavazi wa kutumia vitenge," aliongeza Rehmtullah.

Naye Msemaji wa Hightech Wear na Flygle Tanzania, Aoron Tian Zhonghua, alisema wamekuja nchini kuwekeza kama walivyofanya katika nchi nyingine barani Afrika na pia waliamua kushirikiana na Rehmtullah ili kuongeza soko la biashara kupitia vazi la kitenge.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Sanaa Baraza la Sanaa la Taifa (Basata), Vivian Shalua, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika shughuli hiyo, alisema lengo kuu la onyesho hilo ni kuwaweka karibu wabunifu wa mavazi na wanamitindo na watengenezaji wa vitenge kutoka China na kutoa nafasi wawekezaji hao kujifunza mambo mema yaliyoko nchini Tanzania.

"Lengo kubwa la onyesho hili ni kufungua viwanda ili tualike wawekezaji waweze kufungua viwanda ndani ya Tanzania na pia kutambulisha zaidi vazi la vitenge nchini na kuthamini vazi la vitenge ambalo litakuwa la nguo za aina mbalimbali," alisema Shalua.

## Wawakilishi waenda Arusha kupambana

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya soka ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar inatarajia kusafiri kuelekea jijini Arusha kwa ajili ya kucheza mchezo maalum dhidi ya wenyeji wao klabu ya wazee, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha wa Baraza la Wawakilishi, Saleh Machupa, alisema kuwa timu hiyo inaondoka Visiwani hapa leo ikiamini wanakwenda kuwawakilisha vema na baraka zote za Wazanzibar.

Machupa alisema kuwa timu yake imejiandaa vema ili kuhakikisha wanaibuka na ushindi katika mchezo huo wa kirafiki.

Kocha huyo aliongeza kuwa wachezaji wake walianza mazoezi mapema ya kujiandaa na mechi hiyo mapema, lengo likiwa ni kuibuka na ushindi katika mchezo huo, huku pia akieleza wanamichezo wengine kutoka visiwani hapa pia watachuana katika mchezo wa netiboli.

"Timu yetu imefanya mazoezi kwa muda wa mwezi mmoja sasa, lengo ni kuhakikisha tunapata ushindi katika mchezo huo na kurudi nyumbani na kikombe, ninaimani tutarudi na ushindi mzuri kutokana na maandalizi makubwa tuliyofanya," alisema Machupa.

## Tigo kupeleka watano Afcon

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kuwezesha wateja wake watano kushuhudia mechi za ufunguzi za fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon), kupitia promosheni yake inayoendelea ya SOKA LA AFRIKA, jana Tigo imetangaza washindi wengine watano watakaokwenda Misri kushuhudia mechi ya fainali ya michuano hiyo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Meneja Mawasiliano wa Tigo, Woinde Shisael, aliwataja washindi hao kuwa ni pamoja na Kaunda Petro kutoka Zanzibar, Mohabe Senso (Dar es Salaam), Jafari Zitto, (Tanga), Shabani Msafiri (Dar es Salaam) na Lukundo Sikombe wa Arusha.


"Tigo tunayo furaha kuona promosheni hii ya SOKA LA AFRIKA inawezesha wateja wetu wengine kujishindia safari ya kwenda kuona mechi za fainali ya Kombe la Mataifa ya Afrika sambamba na kuwezesha wateja kujishindia fedha taslimu kwa siku, wiki na kwa mwezi kuanzia Sh. 100,000 hadi Sh. milioni 10. Vile vile tumefanikisha dhamira yetu ya kuwashukuru kwa kuendelea kutuunga mkono kwa kununua bidhaa na kutumia huduma zetu," alisema Shisael.

Kupitia promosheni hii itakayodumu kwa kipindi cha miezi mitatu washiriki wataendelea kujishindia zawadi za fedha taslimu kila siku, kwa wiki na kwa mwezi. Ili kushiriki kinachotakiwa ni kutuma neno SOKA kwenda namba 15670 au tembelea tovuti ya www.tigosports.co.tz na kujibu maswali kuhusiana na michuano hiyo ya Afcon itakayomalizika keshokutwa.

# Michezo

Jumatano Julai 17, 2019

Nipashe

## Wakala akataa Bale kwenda Spurs

HABARI UK 29




Mshambuliaji wa Paris Saint-Germain, Neymar akiwa katika mazoezi ya viungo kwa ajili ya kujiandaa na msimu mpya wa 2019/20. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA SC YASISITIZA KUMKATAA KILOMONI

●●●Magori aonyesha barua kutoka Rita, mwenyewe aziruka nyaraka hizo...

**Na Faustine Feliciane**

KUFUATIA kuzungumza taarifa mbalimbali zinazotofautiana uamuzi uliofanyika wa mabadiliko ya mfumo wa uendeshwaji, uongozi wa Simba umesema kuwa, Hamisi Kilomoni si mmoja wa wadhamini wa klabu hiyo, imeelezwa.

Hata hivyo Kilomoni ameibuka na kusisitiza kuwa bado anatambua yeye ni mdhamini wa klabu hiyo, kwa sababu hajapata barua yoyote inayobatilisha uteuzi wake.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Crescentius Magori, alisema kuwa Kilomoni aliondolewa rasmi kwenye orodha ya wadhamini wa klabu hiyo tangu Oktoba 12 mwaka 2017 na anakosea kuendelea kujitambulisha kwamba yeye ni mdhamini.

Magori alisema kuwa mzee Kilomoni alivuliwa ujumbe wa bodi ya wadhamini na kitendo cha kuendelea kujitangaza kwamba bado ni mdhamini ni kosa.

Alisema kuwa klabu ilitoa taarifa za mabadiliko hayo kwa wakili beki huyo wa zamani wa Simba na wanachomtaka ni kutulia ili asichukuliwe hatua zaidi za kinidhamu.

"Barua zote tunazo hapa na nimekuja nazo, napenda kuwaambia wanachama kuwa suala la mzee huyu (Kilomoni), tunalifunga rasmi leo (jana)," alisema Magori.

Alisema kuwa uongozi wa klabu hiyo umeamua kulipeleka suala la Kilomoni kwenye Kamati ya Maadili ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) ili achukuliwe hatua.

Kilomoni aliliambia gazeti hili kuwa hajawahi kupata barua yoyote kutoka kwa Msajili wa Vyama vya Michezo inayoeleza kuondolewa kwenye nafasi hiyo.

"Si mimi wala wakili wangu aliyeandikiwa barua hiyo, hizo taarifa si za kweli, na wanazidi kukoroga mambo hao watu (viongozi wa Simba), mimi nitatoa taarifa wiki ijayo kujibu hayo waliyoyasema," alisema Kilomoni.

Wakati huo huo, Simba ilitangaza rasmi kuongeza jezi ya tatu ambayo itaanza kutumika katika msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo ni rangi ya kijivu.

Magori alisema uamuzi huo unazingatia kanuni za Shirikisho la Soka Afrika (CAF) katika mashindano yake, kila timu kuwa na jezi huru isiyofungamana.

"Kwa miaka mingi imezoeleka jezi zetu za nyumbani ni nyekundu na nyeupe kwa michezo ya ugenini, jezi za kijivu tutazitumia pale ambapo jezi zetu zitagongana kwenye mchezo na timu pinzani," alisema Magori.

Aliongeza kuwa Simba imekamilisha usajili wake kwa asilimia 90 na kutaja idadi ya wachezaji waliosaini mikataba ni 26, huku akisema kwamba nafasi moja iliyobakia ili kukamilisha kikosi cha watu 27 wataijaza hivi karibuni kama walivyokusudia.

## Urikhob aongeza makali Yanga

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI mshambuliaji mpya wa kimataifa wa Yanga, Sadney Urikhob, kutoka Namibia amewasili nchini jana kuanza kuitumikia timu yake mpya, uongozi wa mabingwa hao wa kihistoria wa Ligi Kuu Tanzania Bara, umesema maandalizi ya 'Siku ya Mwananchi' yako katika hatua za mwisho.

Urikhob alipokelewa na viongozi wa klabu hiyo na tayari ameshaelekea mkoani Morogoro kujiunga na wachezaji wenzake kwa ajili ya kufanya mazoezi ya kujiandaa na msimu mpya.

Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, alisema kuwa kambi yao inaendelea vema na wanaamini malengo waliyonayo ya kufanya vema katika Ligi Kuu na michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika yatatimia.

Alisema kuwa Siku ya Mwananchi ambayo itamalizika kwa mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya AS Vita kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), itakuwa na vionjo mbalimbali na kuwataka mashabiki wa klabu yao wajitokeze kuona wachezaji wao wapya walioasajiliwa.

## Chirwa aipeleka Azam nusu fainali

**Na Adam Fungamwango**

WAKITOKEA nyuma, mabingwa watetezi wa mashindano ya Kombe la Kagame, Azam FC wamefanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo baada ya kuifunga TP Mazembe mabao 2-1 katika mechi ya robo fainali iliyochezwa jana kwenye Uwanja wa Nyamirambo jijini Kigali, Rwanda.

Kwa ushindi huo, Azam FC ambayo inaushikilia ubingwa wa mashindano hayo kwa mwaka wa pili mfululizo, itakutana na mshindi wa mchezo wa robo fainali nyingine itakayochezwa leo kati ya wenyeji, APR FC dhidi ya AS Maniema ya Kinshasa.

Iparm Jiovani alikuwa wa kwanza kufunga bao katika mchezo huo dakika ya 21 huku Azam iliwachukua dakika tano tu kusawazisha kupitia kwa mchezaji wake mpya iliyomsajili akitokea Mbeya City, Idd Suleiman 'Nado' huku Mzambia Obrey Chirwa akifunga goli la ushindi dakika ya 69.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >